

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA PILI

Kikao cha Kumi – Tarehe 13 Februari, 2021

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2021 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Bill, 2021*).

MHE. MOHAMED O. MCHENEGRWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2021 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Bill, 2021*).

NAIBU SPIKA: Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji kwa ajili ya hii hoja tullyonayo. Tutaanza na wachangiaji upande wa Serikali halafu Bunge litakaporejea atakuja Mheshimiwa Waziri kuhitimisha hoja.

Mheshimiwa Pauline Gekul, dakika kumi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya njema siku ya leo na kupata nafasi katika Bunge lako Tukufu. Pia nitoe pole katika familia ya mwenzetu Mheshimiwa Nditiye kwa msiba ambao umetukumba. Nasi sote ni njia yetu, zaidi sana ni kuombeana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvubi, naomba nijibu hoja kadhaa za Wabunge ambazo wamezitoa wakati wanachangia Mpango na zaidi ya Wabunge 25 walichangia katika Wizara yetu. Sisi tumepokea kama Wizara, maoni ya Waheshimiwa Wabunge ambayo wameyatoa kwa lengo la kuboresha utendaji kazi katika Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uvubi, kwa sababu muda ni mchache, niende moja kwa moja; nitakuwa nakwenda kwa hoja zile ambazo zimesemwa kwa ujumla wake; lakini zile ambazo pia zinahitaji majibu, Wizara yetu iko tayari kujibu kwa maandishi na kuwapatia Waheshimiwa Wabunge pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja kubwa kwa upande wa uvubi ilikuwa ni kuboresha uvubi wa bahari kuu. Katika Mpango huu, Serikali imejipanga; tunafahamu kwamba tuna

Mpango wa Miaka Mitano na Mpango wa Mwaka Mmoja. Wizara yetu imebahatiwa katika Mpango huu wa Mwaka Mmoja kuingiza mambo kadhaa ambayo yakienda kuanza sasa yatakwenda kuboresha uvuvi wa bahari kuu. Jambo la kwanza ni suala la ujenzi wa bandari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe, Serikali ilishaanza upembuzi yakinifu kuangalia maeneo mbalimbali ambayo Bandari ya Uvuvi itajengwa. Pia Serikali ikishirikiana na wenzetu wa Italia wameshaanza na zaidi ya Shilingi za Kitanzania bilioni 1.4 zilitengwa na shilingi milioni 700 zilishalipwa kwa kampuni hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upembuzi yakinifu, eneo la bandari ambalo sasa Serikali tunaenda nalo ni eneo la Bagamoyo pale Mbegani. Kazi hii inaendelea. Muda wowote upembuzi yakinifu ukikamilika sasa tunaenda kuwa na *actual design* ya bandari hii na kazi hii ianze ili tunapoenda kwenye uvuvi wa bahari kuu, bandari iwe imeshaanza kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi walichangia ni suala la ununuzi wa meli, kwamba tunapokwenda sasa kwenye uvuvi wa bahari kuu Serikali ihakikishe kwamba tunajipanga kununua meli zetu. Bahati nzuri wenzetu wa *IFAD* katika Mfuko ule wa Maendeleo wa Kilimo pamoja na Mifugo na Uvuvi wameshatukubalia kwamba watatupatia fedha kwa ajili ya ununuzi wa meli hizo na meli hizi nane; nne zitakuwa upande wa Zanzibar na nne zitakuwa upande wa Bara. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Zanzibar wameshatoa vigezo, wanahitaji meli za namna gani, nasi Bara tayari tunafahamu ni meli za namna gani, kwa vipimo vipi. Pia wenzetu hawa watatupatia Dola za Kimarekani milioni 58 ambazo sasa sisi Uvuvi tutakuwa na gawio letu hapo kwa ajili ya ununuzi wa hizi meli. Kwa hiyo, niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba kazi hii inaanza sambamba ikiendelea na upande wa ujenzi wa bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kazi hii itakapoanza, pande zote mbili za nchi yetu watashirikishwa. Pia usimamizi huu utaendelea kufanyika na mamlaka ya uvuvi wa bahari kuu ambayo sasa inaendelea na kanuni zake tumeshazitunga, tunasubiri Mawaziri wa pande zote mbili waweze kusaini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa jumla kuhusu uvuvi, kulikuwa na tatizo la tozo. Kwamba wavuvi wetu wengi wanahangaika na tozo, lakini maeneo mengine inawezekana hawatendewi haki. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza kuhusu suala la kanuni zetu ambazo tumezitunga za mwaka 2020 ambapo maeneo mengi zimekwenda kugusa wavuvi na zimesababisha sintofahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijulishe Bunge lako Tukufu kwamba Wizara hii ni sikivu; Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara, tumeangalia kwa upya kanuni hizo, lakini pia yale maeneo ambayo yalikuwa yanasurya wavuvi, mfano uvuvi wa *ring net* katika bahari kuu, tumeyafanya kazi nanyi mmeona. Kwa upande wa Tanganyika, suala la wavu wa dagaa, tumefanya kazi na tuliwashirikisha pia. Kwa hiyo, tutaendelea kuboresha taratibu masuala ya uvuvi na tutawashirikisha Waheshimiwa Wabunge; na baada ya Bunge pia tutafika kwenye maeneo yenu ili pasiwepo na matatizo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwa upande wa mifugo. Kwa upande wa mifugo, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia kwa upana wake, suala la Serikali kuwekeza katika mifugo. Tumepokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge katika maoni yao tuliyoyapokea wamehitaji Serikali iwekeze katika ujenzi wa miundombinu ya mifugo kote nchini. Sisi kama Serikali, tumejipanga, kwa kuanzia tu, tumeita kikao cha wadau wote ambao wanajihusisha na uzalishaji na uchakataji wa nyama. Tuna viwanda kama tisa katika nchi yetu. Nafahamu kwamba hoja kubwa ni kuangalia hizi tozo

ambazo zinasababisha viwanda vyetu vinashindwa ku-perform waki-*compete* na nchi za wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumeshapitia hizo tozo na katika Bunge lijalo la Bajeti, tutapendekeza mabadiliko mbalimbali ili kuhakikisha mifugo yetu inachakatwa ndani ya nchi. Haturidhishwi ng'ombe, mbuzi na kondoo kutoroshwa. Mwaka 2019/2020 tulikuwa na ng'ombe milioni 1.4 wanatoroshwa au wanasafirishwa wakiwa wazima kwenye nchi za wenzetu, halafu wao wanachakata, wanauzu hizo nyama wakati ng'ombe wametoka kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi tozo tutazipitia kwa upya tuone kiasi gani tunaweza kuzirekebisha ili viwanda vyetu vya ndani viweze kufanya kazi sawa na viwanda vya nchi za wenzetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kwa upande wa mifugo ni suala la kuongeza malisho. Wizara katika kuhakikisha...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, dakika tano.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii angalau kutoa ufanuzi wa hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, kwa maana ya 2021/2022 – 2025/2026 pamoja na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wakati wanachangia waligusia mambo mengi sana ambayo yanasisimamiwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI. Nami kwa niaba ya Waziri, Mheshimiwa Suleiman Jafo, naomba nitoe baadhi ya ufanuzi katika mambo ambayo tumeyasikia na tunaendelea kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo Waheshimiwa Wabunge walizungumzia ni mapendekezo ya kuiongezea fedha *TARURA* ili waweze kujiwezesha kujenga hizi barabara za vijiji. Kwa hiyo, kitu kikubwa ambacho Waheshimiwa Wabunge wanapaswa kufahamu, ni kwamba Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa kushirikiana na *TARURA* pamoja na *TANROAD*, imeandaa andiko linalopendekeza upya kupitia chanzo hiki cha mafuta ili tuone kama kinaweza kikasaidia. Pendekezo hili tunakwenda kuliwasilisha Serikalini kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Serikali inaendelea kupitia *formula* wa mgao wa fedha chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, kupitia Bodi yake ya Mfuko wa Barabara. Kwa hiyo, hili tuliona tulizungumze kwa sababu ni Wabunge wengi walikuwa na nia njema kutaka kuona kuna ongezeko la mapato kwenye Mfuko wa *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la lingine ni kwamba watu wa *TARURA* hawawajibiki katika Halmashauri kwa maana ya Madiwani. Nieleze tu kwamba, Mwongozo wa Wakala wa Barabara Vijiji na Mjini, unaelekeza vizuri kabisa kwamba Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambao ultolewa na Katibu Mkuu mwaka 2018, inaitaka *TARURA* kufanya kazi moja kwa moja na Serikali za Mitaa. Pia Mheshimiwa Waziri alishalitolewa mwongozo kwamba miradi mingi inapaswa kuibuliwa na Madiwani ambapo watashirikiana na *TARURA* ili kuitengenezea bajeti na hivyo iwe inatekelezeka. Kwa hiyo, bado msimamo wa Serikali uko pale pale kwamba *TARURA* itaendelea kufanya kazi na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, lilikuwa ni kuimarisha miundombinu. Hili tumelipokea, nafikiri litakuwa

affected zaidi baada ya yale mapendekezo ya awali ya ongezeko la mapato ambayo tunayapeleka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya nne, Waheshimiwa Wabunge walieleza kuhusu uendelezaji wa Mradi wa Jiji la Dar es Salaam kwa maana ya *DMDP*. Kwa kifupi tu ni kwamba Serikali inaendelea kukamilisha utaratibu kwa ajili ya uendelezaji wa mradi huu na kwa awamu ya pili tunatarajia huu mradi wa *DMDPutatumia* dola za Kimarekani milioni 120.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la afya, Waheshimiwa Wabunge walipongeza jitihada kubwa ambayo imefanyika katika ujenzi wa Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali katika ngazi za Wilaya na wakataka kuhakikisha kwamba Serikali inamaliza miradi yake kama ambavyo ilikuwa imepangwa hususan yale maboma ambayo yamebuliwa na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze tu kwa kifupi kwamba kwa mwaka 2021, Serikali imetenga zaidi ya shilingi bilioni 27.5 kuhakikisha kwamba tunakamilisha maboma 555 ya zahanati zote nchini. Kwa hiyo, tumeamua tuliseme. Tumetenga shilingi bilioni 33.5 kuhakikisha tunanunua vifaa tiba katika hospitali 67 za halmashauri ambazo zilikuwa zimejengwa katika mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la elimu, Waheshimiwa Wabunge walieleza kwamba pamoja na jitihada nzuri ambazo Serikali imezifanya kwenye kujenga miundombinu mizuri, lakini walikuwa wanataka ihakikisha kwamba inaongeza idadi kubwa ya Walimu katika shule zetu. Sasa katika kukidhi jambo hilo, tueleze tu kwamba Serikali itaendelea kuajiri Walimu kama ambavyo tumefanya mwaka 2020, tulitangaza ajira 13,000; ajira 8,000 tayari zilikuwa zimeshatolewa na 5,000 ziko katika hatua ya mwisho. Vile vile ni kwamba tutaendelea kufanya hivyo, kulingana na mahitaji kama ambavyo tumeyaainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Waheshimiwa Wabunge walikuwa wamezungumzia ushirikishaji wa

wananchi kwenye shughuli za kiuchumi. Sasa hili tumelainisha vizuri kabisa kwamba kwa kushirikiana na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, tumeandaa Mkakati wa Miaka Mitano, kwa maana ya 2017 mpaka 2025 kuhakikisha kwamba tunawa-*accommodate* wananchi wote. Ndiyo maana unaona Serikali imeanzisha utaratibu wa kutumia *force account* ku-*accommodate* wananchi wa kawaida kushiriki katika uchumi wa nchi yao.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni miradi ya maendeleo...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Silinde, kengele imegonga. Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofii)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, dakika nne na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, dakika nne.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii. Kwanza nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia na kutoa maoni katika masuala yanayohusu sekta ya Kilimo. Sisi kama Wizara tunachukua sehemu kubwa na maoni yao na mabadiliko makubwa watayaona katika bajeti tutakayokuja nayo katika Bunge lijalo Mwenyezi Mungu akijalia. *(Makofii)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu niweze kutoa *highlight* katika baadhi ya maeneo. Hatua ya kwanza, Waheshimiwa Wabunge wamechangia sana kuhusu suala la udongo, ugani na mbegu na hasa za mafuta. Kuhusu suala

la ugani na suala la kupima afya ya udongo, Wizara tutakuja katika bajeti ijayo na mpango wa kuanzisha *Agricultural Centre* katika kila halmashauri na tutagawa katika kila Halmashauri, *lab equipment* ambayo ni *mobile equipment* itakayotumika kupima afya ya udongo na kutoa huduma ya afya ya udongo kwa wakulima bure ili kila mkulima aweze kupimiwa kipande chake cha ardhi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni teknolojia rahisi,; kama Wizara tumeamua kuchukua hatua hii kwa sababu sasa hivi mkulima kupima afya ya udongo, kila *sample* inamgharimu kati ya shilingi 40,000/= mpaka shilingi 100,000/= kutokana na umbali wa eneo na maabara anayotumia.

Kwa hiyo, tutatumia *simple technology, lab equipment* ambayo itakwenda kufanya *soil analysis* na *soil profile* na kumpatia hati mkulima kumwonyesha kwamba udongo wako huu una sifa hizi na unafaa kwa zao hili na unatakiwa kutumia hivi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya pili katika hizi *Agricultural Center* tutakazoweka katika kila Wilaya, tutagawa pikipiki 7,000 kwa Maafisa Ugani wa Nchi nzima katika msimu ujao na kila pikipiki tutaifunga *GPS*. Sasa hivi tumeanzisha ile *call centre* hapa Wizarani ambayo *GPS* hizi zitakuwa *monitored from the centre* kuweza kujua Afisa Ugani kama anafanya kazi katika eneo lake na tutawapatia *ipad* ambayo watakuwa wanajaza taarifa za *call sheet* za kila siku kuonesha wame-*visit* shamba gani na kumtembelea mkulima gani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo wameongelea sana Waheshimiwa Wabunge ni suala la *research and development* na mbegu. Tumeamua kama Serikali suala la *research and development* kutegemea *donor funding*, halitakuwepo. Tutaanzisha *Research Fund* ambayo ipo kwa mujibu wa Sheria ya *TARI* ili kuweza ku-mobilize fund kwa ajili ya *research and development*. Kwa kuanza katika bajeti ijayo tutaleta mpango wa kuzalisha tani 5,000 za *OPV* za alizeti ili katika msimu ujao wa kilimo tuweze kuwagawia

wakulima na tuweze kupata *metric tonnes*, 123,000 za mafuta za alizeti kutokana na *input* ya hii *seed*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la pembejeo, tumeamua kubadili mfumo na nataka niwahakikishie Wabunge tumefanya *pilot* kwenye pamba na tutaifanya kwenye korosho msimu ujao. Mwaka huu kwenye pamba tumewagawia wakulima mbegu bure. Tumewagawia wakulima dawa bure na gharama za dawa hizi tunazipata kutokana na mjengeko wa bei. Tutafanya hivyo hivyo kwenye korosho, tumeshatangaza *tender* safari hii tutagawa dawa za korosho kwa wakulima bure na tutawapatia dawa hizo na tumefanya kwa *bulk procurement* na hii itatupunguzia gharama na tunatarajia *sulphur* safari hii itapungua bei itakayoenda kwa wakulima na tuta-recovergharama kutoka kwenye mjengeko wa bei. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu zao la chai; tumeanza mchakato wa kuweka soko letu Dar es Salaam ambalo litakuwa ni kwa ajili ya kuuza zao la chai moja kwa moja, lakini vile vile Kiwanda cha Mponde nacho kitafunguliwa na mwaka huu tutasafirisha korosho zote kwa kutumia gunia za katani. Nitumie Bunge hili kumwambia mwekezaji ambaye ana viwanda viwili vyaa magunia cha Morogoro na Kilimanjaro tunampa kazi, akishindwa tutapeleka mapendekezo Serikalini kumnyang'anya viwanda hivi tuwape wawekezaji wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *irrigation* tutatumia...

(*Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Muda umekwisha Mheshimiwa, ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: ... tutatumia mfumo wa *force account* na hii itaonekana katika Halmashauri kama tunavyojenga miradi mingine ya shule. Kwa hiyo nataka niwaambie tu Wabunge kwamba waisubiri bajeti ya Wizara

ya Kilimo, Mwenyezi Mungu akitujaalia. Ahsante sana.
(Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Angeline Mabula, Naibu Waziri wa Ardhi, Maendeleo ya Makazi. Dakika nne.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mungu kwa fursa ambayo nimeipata kuweza kuchangia katika Bunge lako lakini pia kwa sababu muda ni mfupi niwashukuru sana wachangiaji ambaao wamechangia kwenye Wizara yetu ni takriban Wabunge tisa ambaao wamechangia. Hoja kubwa ilikuwa ni suala la kupima ardhi yote ya Tanzania kama ambavyo waliomba, lakini pia wakasema wigo wa ukusanyaji wa mapato nao bado hautoshelezi. La tatu likawa ni katika kupanga mijji kama ambavyo inaonekana tulivyoanza katika ile Magometi Quarter, Wilaya ya Kinondoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane kweli na Wabunge jinsi walivyosema mpaka sasa ni takriban asilimia 25 tu ya ardhi yote nchini ambayo imepimwa. Kwa hiyo asilimia 75 yote inaonekana hajapimwa na mpaka sasa tulichowenza kupima ni viwanja 2,349,626, mashamba 28,312 na kutoa hati 1,559,509, ukiangalia kwa watu wachache kama hao bado ni tatizo kweli. Mkakati tulionao kama Wizara tumeona tutatumia *approach* moja ambayo inasema *fit for purpose* ambayo imetumika katika maeneo mengine na imeweza kuleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo tunachofanya sasa ni kuwajengea uwezo wataalam wetu tulionao. Tunao wataalam wachache, tunatakiwa kuwa na wataalam 2,500 kwa nchi nzima, lakini tulionao mpaka sasa ni 1,400. Kwa hiyo 1,400 hawawezi kukidhi haja katika suala zima la upangaji, upimaji na kumilikisha, lakini tunasema tutajengea uwezo wapima wakati ambaao tutakuwa tunawaita *para surveyors*, watajengewa uwezo ili waweze kusaidia katika hili jambo la upimaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tutatumia vyuo vyetu tulivyonavyo; Chuo cha Morogoro pamoja na Chuo cha Tabora katika suala zima la upimaji. Tumejaribu katika kipindi kilichopita kutumia makampuni kwenee zoezi la upimaji shirikishi, lakini kati ya makampuni 134 tuliyo *yoga-engage* ni makampuni 34 tu ambayo yamefanya vizuri. Makampuni mengine yote yameshindwa na mikataba tumewanyang'anya.

Sasa tunachofanya ni kuelekeza kwa sababu tayari mikoa yote ina ofisi na ina wataalam wa kutosha wawewe kuunga nguvu katika mikoa yao jinsi walivyo kuitia ofisi za halmashauri zote, tumeshatambua wale watumishi tulionao kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama ni suala la kupima, kupanga na kumillkisha tutalifanya kama operesheni maalum kwamba wataungana ngazi ya mkoa kwa sababu mikoa yote ina vifaa na kuna baadhi ya wilaya zina vifaa. Kwa hiyo tunaunda timu ndani ya mkoa mmoja, wanaanza wilaya moja baada ya nyingine. Kwa hiyo katika hili tumeomba pia ushirikiano wa ma-RASpale kuweza kuongeza nguvu katika suala zima la kuunda timu kwenda katika wilaya moja baada ya nyingine. Kwa kutumia *approach* hiyo itakwenda kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika suala zima hilo la kupanga makazi kama tulivofanya Magomeni *Quarter* ambayo aliomba Mheshimiwa Mtemvu wa Dar es Salaam linawezekana kwa sababu pia wenzetu wa Morocco, Ethiopia wamefanya hivyo. Ni ule utayari tu wa halmashauri zenyewe kuweza kuwashawishi wananchi katika yale maeneo yakaondolewa yale makazi ambayo si mazuri ambayo ni ya kawaida sana wakajengewa makazi mengine kama ilivyo Magomeni *Quarters*, halafu wale wanakuwa wa kwanza kupewa kipaumbele kuweza kumiliki maeneo yale ambayo yatakuwa yamejengwa na sehemu nyingine kama ni Halmashauri zinaweza zikatumia kwa kazi nyingine. Kwa hiyo hii pia itatusaidia kuondoa adha ya majengo au nyumba zingine ambazo ziko mjini lakini hazifanani na mijji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la ukusanyaji wa maduhuli kama hamjapima, hamuwezi kukusanya, lakini bado tuna madeni mengi ambayo tunadai na tumeweza kusambaza *notice* na sasa tutasimamia sheria kwa ukaribu zaidi. Ukishapewa *notice* ndani ya siku 14 unatakiwa upelekwe kwenye Baraza, ukishindwa basi tunanadi vitu vyako na kama umepewa *notice* miezi sita kinachofuata ni kunyang'anywa ule umiliki bila kupewa taarifa, kwa sababu tayari utakuwa ulishapewa *notice*. Kwa hiyo hilo litatusaidia pia katika watu. Pia wale ambao wenye viwanja ambavyo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa, kengele imeshagonga ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja.

Walio pimiwa viwanja lakini hawataki kumiliki mwaka jana tulibadili sheria hapa, Kifungu Na. 33 (1) kilibadilishwa kwa hiyo hata kama hauna hati, sisi tunaanza kutoza kodi kwa sababu tulishakupa *grace period* ya siku 90 uweze kuomba kumilikishwa. Sasa kama hujamilikishwa maana yake tutaanza kutoza kodi katika viwanja vyote na tumeshaanza, uwe una hati au huna hati utakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo rai yangu ni...

MWENYEKITI: Mheshimiwa, ahsante sana. Shukrani.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: ... wananchi kushirikiana na Halmashauri zote. Na tunatambua namna ambavyo TAMISEMI wameanza na sisi vile vile tunatumia watendaji wa mitaa kuweza kuwatambua wadeni wetu kuweza kukusanya kodi na kuweza kuangalia namna bora ya kupata takwimu sahihi zitakazotuwzesha pia kuweza kupata mapato ya nchi. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Afya, Dkt. Dorothy Gwajima. Dakika tano.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru kupata fursa hii kuweza kuchangia, nitachangia maeneo machache ya dawa na bima kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa dawa, tumepokea malalamiko mengi yanayohusiana na ukosefu wa dawa na tunakiri kuyapokea malalamiko hayo na sisi tunapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba sasa Wizara imechukua mwelekeo mpya wa kihistoria wa kuboresha upatikanaji wa dawa nchi hii ili huu wimbo ukosefu wa dawa ufikie tamati. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mabadiliko gani? Tumeamua kwa dhati kama wazalendo kuanza sasa kununua dawa sio kwa *middle men*, sio kwa washitiri yaani unaletewa dawa unanunua kwa mtu wa tano aliyenunua kutoka kiwandani. Tunakwenda kiwandani huko huko kuzinunua hizi dawa na hivi ninavyosema *MSD* tayari imeshapeleka *order* toka Novemba mwaka jana kuititia bilioni 43 zilizokuwa zimetolewa na Serikali na makontena yako bandarini yanakuja mapema Machi yanafika. Yakifika hizo dawa zitakuwa nyangi na zitasambazwa na vituo vitanunua kwa bei nafuu dawa hizo tofauti na awali. Kwa hiyo kuanzia Machi mwanzoni hapa dawa zitakuwa zimeingia nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hilo, *MSD* imechukua mwelekeo sasa wa kuanza kutengeneza dawa kuititia viwanda vyake, imeongezea hilo jukumu na linaendelea kukamilishwa ili lianze. Hata hivyo, kuna vile viwanda ambavyo Serikali tulikuwa tuna-share ndogo, kwa mfano pale Keko, *shares* zimepanda mpaka asilimia 70 na tayari *MSD* alishazalisha *dose* milioni 25 za *erythromycin* mwaka jana Desemba na kuzisambaza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunahamasisha wawekezaji wa viwanda vyaa dawa nchini waache kuwekeza

Ulaya maana gharama inakuwa kubwa, wanakuja kuwekeza hapa nchini kwetu. Sambamba na hilo, sisi wenyewe tumefanya mabadiliko makubwa kwenye Hospitali zetu za Kanda, Taifa pamoja na Hospitali za Mikoa zinachukua *direction* ya kutengeneza zile dawa na vifaatiba vidogo vidogo ambavyo viko ndani ya uwezo wetu. Yote hii ni kupunguza mzigo mkubwa wa Serikali kununua vitu hivi kutoka kwa *middle men*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la vifaa. Kwenye *direction* hii tulioichukua vifaatiba vikiwemo vyâ *dialysis* vinavyotesa sana wananchi pamoja na kwamba tunaimarisha suala zima la kinga, watu wasipate magonjwa haya yasiyoambukiza, lakini gharama zitashuka kutoka 300,000 mpaka 100,000 kwa maamuzi haya ambayo tumeyachukua. Hata ule mpango wa *SADC* kuanza kuipa *contract MSD*sasa utatekelezeka vizuri. Sambamba na vifaa hivyo kutakuwepo na uwekezaji kwenye *oxygen plants* ili tuache kuwa tunanunua *oxygen* kutoka kwenye maeneo ambayo ni bei ghali sana kwa sababu tutawekeza na *ku-produce* hapa nchini na vifaa vyâ uzazi na watoto na *ICU*, yaani kwenye yale magonjwa ambayo ni *very critical*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo kuhusu vituoni; dawa zinapotea sana, tunafanya ukaguzi wa kihistoria nchi hii. Tunaomba ushirikiano wa Wabunge na Bunge lako Tukufu. Tutachukua maamuzi ya kihistoria vile vile; kwa wale wanaodokoa dawa na kupoteza dawa sambamba na kuhujumu mapato yatokanayo na ukusanyaji wa dawa. Kwa hiyo tunapodhibiti kuanzia kwenye *production*, tunakuja kudhibiti kwenye matumizi, tutakuwa tumehitimisha wimbo wa upungufu wa dawa katika nchi hii na tutaulizana kwani mwanzoni ilikuwaje? Utakuwa ni wakati muafaka ambapo nchi imefunguka chini ya kiongozi wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli anayetupa ujasiri, maana vita sio wingi wa silaha, ni ule ujasiri wa kutumia silaha uende mbele. Kwa hiyo, nathibitisha kwamba suala hili linakwenda vizuri na kuanzia Machi tutegemee dawa, tamati ya ukosefu imefikiwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Bima ya Afya kwa wote tumelipokea kwa mikono miwili, tunakamilisha huu Muswada ambao utaingizwa huko Bungeni ili tuwe na Bima ya Afya kwa wote na hii itachangia sana kumaliza matatizo ya wananchi wetu wengi wanaoshindwa kupata huduma stahiki mahali popote. Tunapofanya haya mabadiliko yanakwenda sambamba na kusogeza hizi huduma karibu na wananchi. Kwa mfano huduma za *dialysis*, sasa hivi tunaanza kuongelea kwenye hospitali za mikoa, kwa sababu baadhi ya hospitali za mikoa kama kumi zimeshapelekewa mashine. Tulishindwa kuzianzisha kwa sababu ya gharama ya kuvipata hivi vifaa. Kwa hiyo kuelekea Machi tutakuwa tayari tunaanza kutoa hizo huduma kwa sababu tuna *access* ya dawa na vifaa kwa bei rahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea mambo mengine yote, tutayafanya kazi na kuyaleta kwenye Bunge lako Tukufu la Bajeti kipindi kinachokuja. Hivyo, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, dakika tano.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutujaalia afya njema na uzima. Pia tuwe pole katika mzigo uliotufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutambua michango iliyotolewa katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sillo Daniel Baran pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika mjadala huu wa hoja kwa kuzungumza na kwa maandishi hapa Bungeni. Tunawashukuru wote kwa maoni yao na ushauri wao waliotupa kwa ajili ya kuboresha Mpango wa Tatoo wa Maendeleo wa Taifa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026) pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2021/2022; ushauri wao tumeupokea tunawashukuru sana wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Kiongozi wa Shughuli za Bunge hapa Bungeni Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusimamia na kuwakilisha Serikali hapa Bungeni. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Phillip Mpango Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano na maelekezo mazuri anayoendelea kunipa katika kutimiza majukumu yangu kama Naibu Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kumshukuru Mheshimiwa Mwigulu Nchomba, Waziri wa Katiba na Sheria kwa kuwasilisha hoja hii kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango na kuniongoza vyema katika kufuatilia michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Fedha wakiwemo Makatibu, Wakuu wa Idara, watumishi wote wa taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara ya Fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya ya utangulizi, napenda kuchangia hoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza, Serikali iongeze juhudhi katika upatikanaji wa fedha za ziada na ugharamiaji wa miradi ya maendeleona lizingatie upande wa Sekta Binafsi, kiwango kimeshuka kiasi cha triliioni nne kwa Serikali na kimeongezeka kwa triliioni 15.2. Kwa hivyo ni vyema Mpango huu wa Taifa kuendelea kutatua changamoto za upatikanaji wa fedha za ugharamiaji Mpango ili kufikia malengo na shabaha tuliojiwekea. Ufanuzi, Serikali itahakikisha kuwa rasilimali zote za utekelezaji wa Mpango zinapatikana kama ilivyopangwa ili kuhakikisha malengo ya utekelezaji wa Mpango yanafanikiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vya fedha vya ugharamiaji ni pamoja na Mapato ya Ndani na yasiyo ya ndani, misaada, mikopo nafuu, hati fungani na amana za Serikali; Mikopo ya kibiashara, ubia kati ya Serikali na Sekta

Binafsi; Utekelezaji wa moja kwa moja wa taasisi na mashirika ya umma (*Joint venture*) na utekelezaji wa moja kwa moja wa Sekta Binafsi. Katika kuhakikisha hilo vyombo mbalimbali vya ugharamiaji mapato, vimeambatanishwa katika sehemu ya sita ya kitabu cha Mpango kulingana na eneo la ugharamiaji na aina kubwa za miradi au programu, fursa za kiuchumi, kijamii zilizopo na vihatarishi vya Mpango. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja namba mbili; Serikali ihakikishe kuwepo na upatikanaji wa taarifa endelevu za utekelezaji miradi na bajeti, dhidi ya hatua na malengo ya Mpango. Ufanuzi, katika kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa uchambuzi wa kina wa Taarifa za utekelezaji miradi, Serikali imeandaa Mifumo mbalimbali ya Kielektroniki (*GEPG*); Mfumo wa Msaada na Ununuzi wa Serikali (*TANEBS*); Mfumo wa Uhasibu Serikalini (*MUSTE*); Mfumo wa Uandaaji wa Usimamizi wa Bajeti (*CBMCS*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mifumo hii Wizara na Idara na Taasisi na Serikali zitaendelea kutoa takwimu sahihi za utekelezaji wa miradi ili kusaidia ufanyaji na tathmini za ufanisi. Aidha, Serikali imeanza maandalizi ya kuanda mwongozo wa Kitaifa na ufuatiliaji wa tathmini za miradi mbalimbali ya maendeleo ili kuweka miongozo rasmi katika shughuli za ufuatiliaji na tathmini na kuwezesha mchakato shiriki katika ubia na uandaaji wa taratibu na usimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja namba tatu, Serikali ihakikishe inaelekeza Mpango Mkuu kulingana na sheria, kanuni na taratibu. Ufanuzi, ushauri umepokelewa Serikali itaendelea kutekeleza Mipango ya Maendeleo kwa kutimiza sheria, kanuni na taratibu zilizopo katika Sheria ya Bajeti. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa ufanuzi huo, naomba kuunga mkono hoja na kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Ahsanteni sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Mipango imemaliza kazi zake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Sasa nimwite Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Katiba na Sheria, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, aje ahitimishe Hoja yake. (*Makof*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kuhtimisha Hoja nillioitoa hapo tarehe 8 Februari, 2021. Awali ya yote, nikupe pole wewe mwenyewe pamoja na Mheshimiwa Spika na sote hapa Bungeni kwa ajili ya kuondokewa na mpPENDWA wetu ambaye tumekuwa naye muda wote hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotangulia kusema hapo tarehe 8 Februari, 2021 niliwasilisha katika Bunge Iako Tukufu Mapendekezo ya Mpango wa Tatoo wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 hadi 2025/2026, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ya Mwaka 2021/2022 na Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti kwa Mwaka 2021/2022 ambapo Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kuyajadili kwa siku takribani tano na kuiwezesha Serikali kupata maoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru sana wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Spika kwa kuendesha mjadala huu kwa ustadi mkubwa ambaotunauhitimisha hii leo. Aidha, napenda kuchukua fursa hii pia, kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijijini, kwa maoni na ushauri mzuri waliloutoa kwa ajili ya kuboresha mapendekezo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri kwa ufanuzi walioutoa pamoja na michango ambayo wametupenyezea ya kuendelea kuboresha mpango huu, nikitambua mchangwa Naibu Waziri aliyeleta mapendekezo kuongeza masuala yanayoongelea upande wa watu wenye ulemavu. Aidha, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango waliyochangia na hadi sasa imefikia Wabunge 164 waliochangia; kati yao 153 wakiwa wamechangia kwa kuzungumza na 11 wakiwa wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba, kusudi la mjadala huu ilikuwa ni Wabunge waweze kutoa maoni yao, ili tuweze kuboresha mapendekezo haya na sisi kwa niaba ya Wizara tuseme tumeyapokea, kwa niaba ya Serikali tuseme tumeyapokea. Yale ambayo moja kwa moja yataenda kuboresha Mpango tutayafanya kazi kwa namna hiyo na yale ambayo yanahitaji ufanuzi mengine tutafafanua hapa na mengine tutaleta kwa maandishi kwa kuzingatia kwamba, michango imekuwa mingi san ana michango mingi imekuwa na manufaa makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie kwa kufanua michache tu ile ambayo inahitaji ufanuzi na ile yote ambayo inaboresha Mpango na mapendekezo haya tutaenda kuitumia kwenye kupendekeza, ili tuweze kuleta tena, kama taratibu za kibunge zinavyosema. Moja ya hoja ambayo ningependa sana kuitolea ufanuzi ili kuweka kumbukumbu sawa ni ule mjadala uliokuwa unahusisha masuala ya tafsiri ya uchumi wa kati, maana yake na kwa mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ilikuwa inatolewa hoja kana kwamba, kipato kile kilichopimwa ni kidogo sana, lakini lingine ilikuwa inatiliwa mashaka tu dhana yenyewe ya kwamba, tuko uchumi wa kati. Napenda kiliarifu Bunge lako tukufu kwamba, kwanza utaratibu wa kuingia uchumi wa kati ni utaratibu ambao unazingatia vigezo. Tanzania kuingia

uchumi wa kati haikutuma maombi kwamba, tunaomba na sisi tuingie tuwe nchi ya kipato cha kati. Hatukufanya *application* na wala Tanzania kuingia kipato cha kati hakulipia, ni tofauti na utafiti unaweza uka-*commission team* kwamba, nifanyieni utafiti huu mniletee ripoti; hatuklipia kwamba, tunalipia ili mtufanyie utafiti mtuambie kama tumeshafika uchumi wa kati ama la. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ni jambo linalozingatia vigezo tena vigezo vyenyewe vimezingatiwa na taasisi kubwa zinazoheshimika duniani, *World Bank, IMF* na wachumi wote ambao wameitangaza Tanzania kwamba, ni ya uchumi wa kati wala sio washabiki wa CCM. Ni taasisi za wasomi waliobobea na hawajaanza kwa kuitangaza Tanzania, zipo nchi ambazo ziliwahi kufika kule na zimefika kule kwa kuzingatia vigezo. Vigezo vyenyewe hata hapa sisi ukianza kuangalia tangu tumeanza kutekeleza Mpango mpaka tumefika hapa ni vigezo ambavyo tofauti zinaonekana na vigezo hivyo kwa yule ambaye atafanyia tathmini Tanzania yetu kiungwana, lazima atafikia katika majawabu ya aina hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale waliokuwa wanasema kiwango chenyewe kile tulichofika ni kidogo sana, kwanza hawaitendei haki nchi yetu na pili hawamtendei haki Rais wetu, kwa sababu, tulitarajiwa tufike by 2025 tumefika mapema kabla ya muda ule. Tumefika mapema kabla ya muda ule kwa sababu ya ujasiri na uthabiti wa Rais wetu kwamba, kuna mambo ambayo yametekelawa kwa kasi kubwa na kwa kiwango kikubwa kuliko ambavyo yalikuwa yakitekelawa kwa muda mrefu tangu tumeweka mpango ule. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano ukiangalia vigezo ambavyo huwa vinatumika, pato la mtu mmoja mmoja kufikia wastani wa dola za Kimarekani 1,036; la pili, kupungua kwa utegemezi wa bajeti na kuongeza fedha kwenye matumizi ya huduma za kijamii. Mengine ni kuboreshwa kwa miundombinu katika nchi husika. Ukienda kwenye wastani ambao waliutumia na ndio wakatoa

majawabu yale, utaona kwamba, wastani wa pato la mtu mmoja mmoja *GNI per capita* uliongezeka kutoka Sh.990,462 sawa na dola za kimarekani 980 kwa mwaka 2015 hadi kufikia Sh. 2,577,967 sawa na dola za kimarekani 1,000,080 kwa mwaka 2019, hivyo, kuvuka kigezo kile kilichowekwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kupungua kwa utegemezi wa kibajeti. Ninyi wenyewe ni mashahidi, kama ninyi mnasema wale watu wamesema tu kama na Benki ya Dunia na *IMF* imeshakuwa umoja wa vijana na wengine UWT, angalieni ninyi wenyewe utegemezi wa bajeti ulivyopungua. Mwaka 2015/2016 bajeti yetu tuliyokuanayo ilikuwa takribani triliioni kama 22 hivi, hivi tunavyoongea tumeshavuka triliioni 34 na utegemezi umepungua zaidi, lakini si hayo tu ambayo tunayataja kwa bajeti kwa ujumla wake, nendeni mkaangalie sasa kwenye huduma ambazo wao ndio wanapima ambazo zimetuvusha kwa kiwango kikubwa, nendeni mkaangalie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye afya, katika miaka mitano takribani triliioni moja imeenda kujenga vituo vya afya vile na imetengeneza wastani wa kila tarafa ina kituo cha afya ambacho kinaweza kikatoa huduma kwa akinamama, kwa watoto, *theatre*, maabara, pamoja na vitu vingine vyote vya muhimu vinavyotakiwa. Ukienda kwenye umeme zaidi ya vijiji 10,000 vimewaka, ndani ya miaka mitano na zaidi ya triliioni tatu zimekwenda tena ni fedha za bajeti yetu. Ukienda kwenye miundombinu ambayo na yenyewe ni msingi mkubwa wa kujenga uchumi unaojitegemea, zaidi ya triliioni 8.6 zimekwenda kutengeneza miundombinu ya aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye utawala bora karibu triliioni moja. Ukienda kwenye usafiri wa majini karibu triliioni moja. Wewe unayepinga kwa nini unaona sifa kuitwa maskini? Yaani wenzako wamekuangalia wakaona wewe umeshaondoka kwenye umaskini, wewe unajisikia bora zaidi wakuone wewe ni maskini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, angalia nchi inayoweza kutoa bilioni 24 kila mwezi kupeleka elimu kwa watoto wake

na hajakwama. Angalia nchi inayoweza kutoa takribani bilioni 700 kulipia watoto kwenye elimu ya juu, tunaita mikopo, lakini kimsingi ni bajeti ya Serikali kwa sababu, hawakopi benki hawa ni bajeti ya Serikali. Mambo mengi yamebadilika, hata jana tu simba kushinda kule ni uchumi wa katii, ndio maana hawakuwahi kushinda siku zilizopita, viwango vyao vilikuwa vya kiuchumi wa katii. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokisisitiza kwamba, vigezo vyote ambavyo nchi ya uchumi wa kipato cha katii inatakiwa kufika, Tanzania imevifikia na tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa sababu ya uthabiti wake tumeweza kuyafikia haya na wale wapiga ramli wanaosema hatutaweza, niwaambieni tunasonga mbele haturudi nyuma, tunakwenda Kaanani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mazoea, mtu allyezoea sana kuitwa maskini, aliyezoea, bado anahitaji tiba kwenye *mindset* kuona kwamba, ye ye hayuko kwenye umaskini. Ni kama kuku aliyefungwa miguuni muda mrefu, kuku aliyefungwa miguuni muda mrefu hata ukimwondolea kamba anaendelea kuegama hivyo hivyo akidhania bado amefungwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wengine wakiambiwa ni wastani wa pato la Taifa limegawanywa kwa uwiano wa wananchi waliopo wanadhani pakigawanywa hivyo kila mtu anapelekewa fedha nyumbani; kwa sababu, tunasema tunagawanya pato, wanadhania wataletewa kila mmoja nyumbani. Si hivyo, huu ni wastani na kama wewe hautashiriki kwenye kuzalisha, kama wewe hautafanya kazi ni dhahiri hautapata hela, kwa sababu, haujazalisha. Wewe ambaye hufanyi kazi na hupati hela ndiye unayetuchelewesha tusiende kwenye takwimu kubwa zaidi ile ambayo tunatakiwa tuifiki. Huo ndio utaratibu na hivyo ndivyo uchumi unavyosema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wengine wanawaza changamoto tu za maisha kwamba, sasa hivi mambo mengi ambayo ni ya kimaendeleo ndio yanatufanya tuwe na

matumizi mengi, ndio inafanya wachukulie kwamba, huo ndio ugumu wa maisha. Hebu fikirieni zamani kabla ya changamoto za maendeleo bajeti zilikuwa zinaenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hatukuwa na simu, kwa hiyo, hakukuwepo na mambo ya simu yenyewe, *air time*, wala *MB*. Tulikuwa tunakula chakula kilichosagwa kwenye jiwe na mama zetu na dada zetu waliokuwa wanasaga tulikuwa hatuwalipi, tulikuwa hatutumii gharama ya kwenda kulipia mashineni. Tulikuwa hatuna umeme kwa hiyo, tulikuwa hatuunganishi hatuna gharama ya umeme, tulikuwa hatuna *TV*, hatuna *ving'amuza*. Tulikuwa tunachota maji kwenye madimbwii, tulikuwa hatulipii, sasa unatakiwa ulipie na bili ya maji na umeme. Tulikuwa tunalima tu ardhi ina rutuba kwa hiyo, tulikuwa hatutumii mbolea tunatumia samadi, hatutumii mbegu tunaanika tu mbegu zile.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, sasa hivi hizi changamoto zote ambazo ndio maendeleo yenyewe zimesababisha bajeti *constraint*, yaani fedha yako ile igawanyike kwenye matumizi mengi, hiyo ndio tunaenda kusema hakuna maendeleo ni maisha mabaya. Ni tafsiri mbaya na wengine waliokuwa wanatafsiri walikiri wenyewe, nilimsikia Mheshimiwa Halima akisema kama bajeti hii imeandikwa na Dkt. Mpango Gwiji wa Uchumi ambaye anatambulika na Benki ya Dunia na *IMF* na vyuo vyote vya duniani, yeche ni nani hata aseme lingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, alikuwa anawaambia kwa lugha nyingine kwamba, yale anayoyasema yeche kwenye *area* hii yapuuzeni haelewi kitu. Ukweli ni haya ambayo yameandikwa kitaalam na ninyi mnatakiwa mwelekee katika mwelekeo wa aina hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hii ya *Stiegler's Gorge* kule ambayo ilikuwa inasemwa, *Mwalimu Nyerere Power Station*; watu wanaenda kusema tu kwenye asilimia eti ni asilimia 25 tu, hata reli ya katika wanasema eti imeshajengwa tu ni kiwango hiki hapa tu. Fuatiilieni hata historia, reli ya katika hii hapa ilijengwa kwa takribani miaka 10. Tena kipindi hicho

hakukuwepo na fedha zinazokwenda kwenye elimu bure, hakukuwepo na fedha zinazojenga hospitali nyingi hivi, hakukuwepo na fedha zinazojenga lami kilometra 13,000, hakukuwepo, hata *population* yenye we iliyokuwa inahudumiwa na Serikali ilikuwa ndogo tu, lakini leo hii ukianzia kule kilometra 300 za kwanza ni asilimia 90. Hata kile ambacho kinachelewesha ni utaratibu wa kujenga kwa uimara zaidi, lakini mambo yote yameshakamilika mpaka mwisho. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda *Stieglers Gorge* hivyo hivyo, *Mwalimu Nyerere Power Station* ile, wana sema ni asilimia 25 tu, lakini nendeni mkaangalie fedha iliyowekwa pale ni triliioni 1.9. Kwa hiyo, vingine ni kiutaratibu kwa sababu, hatupimi kwa kumwaga tu fedha, kuna shughuli zinafanywa tena kwa uthabiti mkubwa. Haya ni mambo ambayo napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Rais na wale wasioyapongeza haya, watoto wao watakuja kuwasuta kwamba, aliwahi kupita Rais mmoja akiitwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli alifanya mambo makubwa haya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo liliongelewa sana lilikuwa hili jambo la matumizi ya kutumia *task force* kwenye makusanyo ya mapato. Kwanza Waheshimiwa Wabunge niwaombe sana kwenye hili jambo tunapoliongelea hili la makusanyo tunatakiwa twende kwa tahadhari sana. Mwenzenu nina kumbukumbu nzuri kabisa kwa sababu, niliwahi kuwa Naibu Waziri wa Fedha wakati awamu inapita inamalizikia na Awamu hii ya Tano inaingia; natambua kazi kubwa waliyofanya Serikali ya Awamu ya Tano kwenye mambo ya makusanyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna kipindi tumekipita ambacho ulipa kodi, elimu ya mlipa kodi, uhiari na uzalendo, lilikuwa jambo kubwa na gumu sana kwa watu wetu, kwa walio wengi, hasa wafanyabiashara wakubwa, hasa walipakodi wakubwa. Ukwepaji wa kodi, nendeni mkafuatile *Hansard* za Bunge lile liliopita, fuatilieni *Hansard* muone kilio kikubwa kilikuwa wapi? Kilio kikubwa kilikuwa walipa kodi hasa wakubwa hawalipi kodi ipasavyo; walipakodi

waliokuwa wanabeba nchi ni watumishi wa umma kwa kiwango kikubwa na walipakodi wadogowadogo na baadhi yao walipa kodi wakubwa waliokuwa waaminifu, kulikuwepo na kiwango kikubwa sana cha ukwepaji wa kodi, kikubwa mno na kulikuwepo na Serikali buba, Serikali ikipanga namna ya kukusanya kodi kulikuwa na *reaction* ya Serikali moja buba; ipo kule tu yenyewe ipo tu, mkipanga bajeti ina-*hire* ndege inakuja, hii haitatekelezeka, ilikuwa namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujasiri wa Rais wetu pamoja na ubunifu wa Waziri wetu katika kumsaidia Rais pamoja na timu yake ya wataalam wakiwepo *TRA* wamepiga hatua kubwa sana. Sasa, sasa hivi hili jambo linaloanza kujitokeza la kwamba, *task force* ndio zinakusanya na *TRA* imeacha majukumu yake, naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, *TRA* bado wanaendelea kukusanya mapato wao wenyewe. Pale ambapo inatokea *task force* inakusanya kunakuwepo na hatua zinazofuatwa. Moja, kunakuwa na taarifa kwamba, kwa mlipakodi huyu kuna viashiria vya kutokulipa kodi ipasavyo. Baada ya hapo kunatumwa timu ya kwenda kukagua, timu ya kawaida tu ya kwenda kukagua ambayo ni Mamlaka ya Mapato, ni wataalam wao. Wakishakagua wanaambizana, wanaelekezana kwa mujibu wa sheria, sheria zetu mlipakodi mnajadiliana katika yale makadirio, wanakubaliana na wakati mwingine wanasainiana, inatokea hataki kulipa ama inatokea amekata rufaa. Hili lilikuwa linatumika sana miaka kadhaa ile iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwa mtu akiona anataka kudaiwa kodi anaenda anai-*park* mahali pale panaitwa *appeal*, ana-*park* mahali hapo halafu maisha yanaendelea. Akitoka hapo anaipelea *tribunal* ana-*park* hapo maisha yanaendelea. Sasa inatokea uamuzi umeshafanyika kwamba, anatakiwa alipe ama inatokea pana taarifa zinazoonesha kuna ukwepaji mkubwa, hapo ndipo kwa kukwepa, kwa kuondokana na uwezekano wa kufanya kazi kwa mazoea, kwa kukwepa na kuondokana kwa uwezekano wa vitendo vya rushwa kuweza kutumika katika masuala haya ya ku-*bargain* rushwa, ya ku-*bargain* fedha za kodi, timu

maalum inapelekwa na Kiingereza chake ndio hiyo inaitwa *task force* ambayo kiongozi wao anazingatia ile miiko ambayo inatakiwa itumike katika kukusanya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Bunge lako tukufu lilikuwa likisisitiza panapokuwepo na *operation* iсиende taasisi moja wala asiende mtu mmoja, ndio tunavyotumia hata kwenye *operation* zingine, tunatengeneza *team* ambazo ni *multidisiplinary* ili kuweza kuchangia uzoefu, lakini pia na kuzingatia maadili ya kwenda kufanya jukumu lile pasiwepo na rushwa, pasiwepo na uonevu, lakini pia pawepo umakini mkubwa zaidi katika jambo lile. Hicho ndicho ambacho kimekuwa kikifanyika katika jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais amelisisitiza sana jambo hili kwamba mara zote mfanyakibashara anayefanya kazi zake ama biashara zake ambazo zimenyooka asibughudhiwe, ameshawaambia hata wafanyakibashara wenye kwenye vikao vile, ameishaikelekeza Wizara, ameshawaelekeza Mamlaka ya Mapato, wazingatie miiko hiyo. Kinachofanyika ni pale panapotokea sasa kuna watu wasiozingatia taratibu wa kulipa kodi, panapotokea watu wanakwepa kodi, panapotokea watu wanafanya njama na njama ziko nyingi sana za kukwepa kodi. Ndio Kamishna wa Mamlaka ya Mapato kwa kutumia sheria inayomruhusu kutengeneza kikosi kazi kama ambayo mnajua, Sura ya 348 ya Sheria ya Utawala wa Kodi inampa mamlaka Kamishna kuunda vikosi na kushirikisha taasisi zingine za umma, Kifungu cha 64 vifungu vidogo mpaka 67 vinampa mamlaka ya kutengeneza vikosi kazi ambavyo vinaweza kwenda kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge kwa mazingira haya kwamba tuna miradi tunatekeleza, kuna wengine wasiotutakia mema hata wasingepeenda tutekeleze, hatuwezi kutekeleza kwa kuomba hela, hatuwezi kuitekeleza kwa kukopa mikopo ya kibiashara halafu tukatekeleza miradi mikubwa ya kiwango hicho, lakini pia hatuwezi tukatekeleza hata hii miradi mingine yote hii tunayoitekeleza bila kuzingatia suala la kulipa kodi. Nitoe rai

kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania wote tuendelee kujenga uzalendo kwa Taifa letu, maendeleo yetu yatakuja kwa sisi kulipa kodi. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na timu yake pamoja na *TRA* waendelee kufanya kazi kwa kuzingatia maadili pamoja na miongozo ambayo inawaongoza katika kutekeleza majukumu yao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kutoa rai kwa Watanzania tulipe kodi na kwa wale ambao walizoea kukwepa kodi kuwaachia mzigo watu wengine na kupata mapato hayo ambayo yalitakiwa yakasaidie huduma za jamii wakayageuza yawe ya kwao, niwahakikishie mazingira ya yao kufanya ukwepaji wa aina hiyo yataendelea kuwa magumu tu, kwa mtu anayepanga kufanya biashara kwa kukwepa kodi mazingira hayo yataendelea kuwa magumu tu kwa sababu haturudi tena kule, tunataka tujenge utamaduni wa watu kulipa kodi kwa sababu hiyo ndiyo inayotufanya nchi yetu iweze kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Wabunge wenzangu wa CCM Watanzania wengi hawakumchagua Rais kwa sababu ya rangi ya nguo aliyovaa, walimchagua kwa sababu wameona miradi hii iliyotekelezwa haijawahi kutekelezwa kwa kiwango kikubwa cha kiasi hiki. Mtu yejote akitushauri tuache kujitegemea, mtu yejote akitushauri tuache kutekeleza miradi, tunatakiwa tuchukulie huyu mtu anataka kutukwamisha kwenye nia yetu hii ya kuwatumikia Watanzania na llani yetu tulioitengeneza ya mwaka huu ni kubwa kuliko ile ambayo tulitengeneza kwa wakati ule. Nini kinachowau ma wengine huku ni uchache wenu, mmejua tumefanya makubwa tumeingia wengi kwa sababu ya ushindi huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo ningependa nilifafanue kuna hoja ilitolewa kuhusu mfumuko wa bei hii na yenye kuna hoja ilitolewa kuhusu *misinterpretation* ina *tafsiri* ambazo zinakinanza. La kwanza, mfumuko wa bei siyo bei, *inflation rate is just a rate is percentage rate showing how quickly the prices are changing.*

WABUNGE FULANI: Kwa Kiswahili.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mfumuko wa bei ni kile ile kasi ya kile kiwango cha bei zinavyobadilika, siyo bei zenyewe. Ukienda tu ukasema mimi jana nimeenda nikakuta bei imeshakuwa hivi, bei iko hivi, ukilinganisha na ya mwaka jana ama ya mwaka juzi, sijui wengine wanachukuliwa ya mwaka gani, ule si mfumuko wa bei, zile ni bei na bei zingine zinatokana na *seasonalities*, ni kubadilika kwa majira. Kwa mfano bei ya alizeti wakati wa mavuno na bei ya alizeti wakati ambao siyo wa mavuno, ni vitu tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo unailinganisha tu mavuno ya mwaka jana na mavuno ya mwaka huu yalikuwaje na mmevuna kwa kiwango gani. Kwa mfano mwaka ule uliokuwa na mafuriko makubwa sana umeathiri kilimo, kwa hiyo kuna baadhi ya mazao yanayotokana na kilimo cha aina hiyo kama dengu, maeneo yale yaliyokuwa yanalinwa ikitokea pamekuwa na mafuriko kote hayajatoka vizuri, *definitely* mwaka kama ule karibu na kilimo kingine kutakuwepo na tofauti ya bei. Ttunachokisemea kama Serikali ni kwamba ile kasi ya kubadilika kwa bei kwa mazao yaliyo mengi na kwa bidhaa zilizo nydingi zinazotumika kwenye viashiria, kwa kipindi chote hicho imekuwa imara. Hicho ndicho tunachopima kwenye mfumuko wa bei na hatufanyi mfumuko wa bei uwe imara kwa kutumia Jeshi wala Polisi, tumetengeneza miundombinu ambayo inafanya ule uimara wa bei katika bidhaa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, wale waliokuwa wanabeba vitunguu kutoka Manyara kuleta Dodoma kabla ya miaka mitano walikuwa lazima wazungukie Singida waje hapa. Wale waliokuwa wanabeba bidhaa kutoka Mbeya, Njombe, Iringa kuleta Dodoma ilikuwa lazima waende Morogoro ndiyo walete hapa. Kwa kutengeneza miundombinu inayopunguza gharama za uzalishaji na gharama za usafirishaji, kunatengeneza bei ziwe imara, zikishakuwa imara hicho ndicho tunachokipima kwa sababu zinasawazisha kutoka kwenye wingi kwenda kwenye

upungufu, hiyo ndiyo mikakati na ndiyo maana tunasema miundombinu hii inaenda kumsaidia mwananchi moja kwa moja kwenye maisha yake. Hili ilimekuwa likifanyika, kwa hiyo tusije tukachukulia kwa dhana finyu ambayo inawaletea hamaki wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu nimeisikia kengele imegonga, niende hoja moja ya mwisho wakati namalizia malizia. Lingine ambalo liliijitokeza kwa kiwango kikubwa liliikuwa suala la deni la Taifa. Nishukuru na nipongeze hoja ya Kamati wameleta kiashiria kile walichokisema cha kuangalia mapato, hicho huwa kinatumika tunapoangalia masuala ya ndani, lakini kwenye vigezo vile vinavyotumika ambavyo ni *standard* na vimewekwa *standard* ili uweze kulinganisha na maeneo mengine, niwatoe hofu kwamba uchambuzi wa deni la Taifa unatumia *model* ambayo ni ya Shirika la Fedha la Dunia na viashirilia vyote vinaonesha deni ni himilivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, deni la nje kwa pato la Taifa ukomo wake huwa ni 55%, sisi tuko 17.3%. Thamani ya deni la nje kwa mauzo ya bidhaa na huduma za nje ya nchi ukomo wake huwa ni 240%, sisi tuko 113.2% tu. Uwiano wa malipo ya madeni ya nje kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi ukomo wake huwa ni 21%, sisi tuko 14% tu na uwiano wa malipo ya madeni ya nje na mapato ya ndani ambapo kwa mwaka huwa ni 23% sisi tuko 13.7%. Kwa hiyo haya mambo yote yanafanyiwa tathmini na pale tunapokwenda kwenye masuala yanayohusu mikopo ya ndani ambapo soko la fedha la ndani bado lina ukwasi wa kutosha huwa tunazingatia kile kigezo ambacho kimewekwa cha ukomo katika masuala haya ya kukopa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba hoja zenu zote mlizozitoa tunazizingatia, tumezipokea na majina yenu yote yameingia kwenye *hansard* (Kumbukumbu Rasmi za Bunge) na sisi tumepokea na zile hoja zenu zitachambuliwa moja baada ya nyiningine na zingine zitakwenda kuboresha Mpango na zingine ambazo zinahitaji ufanuzi ambazo nitakuwa kwa

ajili ya muda sijagusa, mtaletewa kwa maandishi ili muweze kuona ni kitu gani ambacho Serikali imekieleza kwenye jambo milihitaji ufanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hili ndiyo Bunge la kwanza kwa Mpango huu tunaoupanga na kwa awamu hii, niwaombe tuendelee kutoa uongozi, tumsaidie Mheshimiwa Rais. Kwa sisi ambao tumefanya naye kazi, Mheshimiwa Rais wetu uzalendo wake kwa Taifa hili ni wa kiwango cha juu sana na Watanzania wanakiona. Nia yake kwa maisha ya Watanzania ni ya kiwango cha juu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefuatilia sana hizi siasa, nilikuwa napenda siasa tangu niko shule ya msingi. Afrika hapa kupata Rais ambaye *24 hours* na kwa mwaka mzima na kwa awamu nzima anashughulika na maisha ya watu wake tu, tuwe wa kweli *its very rare*, ni ngumu kupata kitu cha aina hiyo. Kuna marais wako, sitaji nchi hizo, Afrika hapa hapa, wanaongoza nchi wakiwa hoteli huko nchi za Ulaya, yuko hoteli na mke wake huko wanaongoza, wako nje, wa kwetu hata akipata likizo unamwona yuko Chato tu na anaendelea kufanya kazi hapo hapo anashughulika na maisha ya Watanzania. Fedha zote zinakwenda kwenye mambo ya maendeleo.

Kwa hiyo hata hapa ambapo unaona namna hii tulivyofanya hapa, mlivyoona hii miradi na miaka mitano hiyo mpaka tukaweza kuingia kwenye kipato cha kati na tukaweza kutengeneza maendeleo kwa kiwango kikubwa hivyo unaweza ukaona ni *commitment* ambayo imetokea kwa maaana hiyo na sisi kama viongozi tuendelee kuunga mkono shughuli hizi maendeleo yanapotokea ni yetu sisi sote na sisi tutaingia kwenye *record* ya kuwa tulichangia pale ambapo tulikuwa na nafasi hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa, nimetoa ufanuzi huu naomba sasa kutoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(*Makofi*)

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, tukae sasa. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Ahsanteni sana. Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, wewe pamoa na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango na timu yenu yote, tunawapongeza kwa kazi nzuri mliyoifanya, mlileta hapa mapendekezo ya Mpango wa muda mrefu na muda mfupi na yote yamejadiliwa kwa kirefu sana na Wabunge na kwa mujibu wa kanuni yetu ya 113 wamewapa mapendekezo yao, wamezungumza mambo mengi. Baadhi ya hoja hizo leo asubuhi mmepata fursa ya kutoa ufanuzi, lakini kwa maelekezo mliyyoatoa hoja nyingi walizozitoa Waheshimiwa Wabunge zitaiwezesha Serikali kwenda kuangalia huu Mpango ambao haya Mapendekezo ambayo wameyatoa, mtayaweka sasa kwenye Mpango na kwa mujibu wa kanuni zetu tutawasikia mwezi wa tatu mkituletea huo Mpango sasa ambao ndiyo umekamilika.

Waheshimiwa Wabunge tulitarajiwa na tunatarajiwa tuendelee kutoa maoni ili Serikali iweze kutimiza majukumu yake. Sasa katika michango tuliyokuwa tunatoa niseme wazi hatukufanikiwa sana kueleza vyanzo vingine vipya vya mapato, hatujasema sisi Wabunge na ilikuwa ni kazi yetu. Katika kipindi hiki cha siku tano tulitakiwa tuwaambie Serikali tunapendekeza vyanzo vingine vipi. Sasa hiyo fursa bado ipo kadri tunavyoendelea huko tunavyokutana na hawa wapiga kura wetu mawazo yao tuyasikilize, kwa sababu sisi ni wawakilishi wao, tuwasikilize, tuyalete, ili Serikali waweze kuyafanya kazi, kwa sababu la sivyo tutakuwa kila wakati tunalalamika kwamba vyanzo ni vile vile, wakati hata sisi hatujafanya kwa sehemu yetu. Kwa hiyo tuendelee kutoa hayo mawazo yetu.

Sasa kwa utaratibu, hoja ikiletwa hapa huwa inahojiwa ili Bunge liafiki, lakini sasa kanuni yetu 113 hapa

tulikuwa tunatoa mapendekezo yetu au mawazo yetu kwenye mapendekezo ya Serikali. Kwa hiyo hakuna uamuzi unaofanywa wakati huu, uamuzi utakuja kufanywa baadaye Serikali itakapoleta Mpango. Sasa yalikuwa ni mapendekezo kwa hiyo hoja hii haitahojiwa. Kwa hivyo tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu.

NDG. NENELWA MWIHAMBI - KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali
wa Mwaka 2021 (*The Written Laws Miscellaneous
Amendment Bill 2021*)**

(Kusomwa Mara ya Pili)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimwite tena Waziri wa Katiba na Sheria, lakini sasa anakuja kwa nafasi yake kama Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba atuletee hoja yake.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuleta hoja kwako kama ambavyo tumeletewa mezani na *Order Paper* yetu asubuhi ya leo na tulivyoweza kuiweka mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana tena katika Mkutano wa Pili wa Bunge. Naomba pia nichukue nafasi hii kumshukuru tena Mwenyezi Mungu kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu pia nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea

kuiongoza nchi yetu kwa malengo, ujasiri, uzalendo wa hali ya juu. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Dkt Hussein Ally Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Mawaziri wote kwa ushirikiano wao wanaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Spika na wewe mwenyewe kwa kuiongoza na kusimamia vikao vyta mijadala ndani ya Bunge kwa umahiri na kwa kuzingatia kanuni zilizotungwa na Bunge hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao katika kutunga sheria pamoja na kusimamia Serikali ipasavyo. Naishukuru Ofisi ya Bunge na Wabunge wote kwa ushirikiano walioipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika maandalizi ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa nimetoa utangulizi huo, nitumie sasa fursa hii kwa kukupa pole wewe mwenyewe pamoja na Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuondokewa na Wabunge wenzetu. Niwape pole sana moja kwa kuondokewa na Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla ambaye alikuwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Manyara, ambaye alitutoka tarehe 20 Januari, 2021 na Mheshimiwa Nditiye ambaye alifariki tarehe 12 Februari, 2021 hapa Dodoma. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu Dkt Evaristo Emmanuel Longopa kwa kuendelea kutekeleza vema majukumu yao ya kazi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ikiwemo kuandaan

Muswada huu ambao ulisimamiwa kwa karibu sana na ndugu Njole wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu akishirikiana na Waandishi wa Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tunatambua na tutaendelea kuwahakikishia kuwa tuatekeleza majukumu yetu kwa weledi, ufanisi na kwa kuweka mbele maslahi ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize shukrani zangu kwa kuishukuru sana Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria inayoongozwa na Mwanasheria nguli, Mwenyekiti wake Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Najma Giga, Mbunge wa Viti Maalum kwa ushirikiano wao na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu mbele ya Kamati hiyo.

Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana kuchambua Muswada huu kwa makini na kusikiliza na kuchambua maoni yaliyokuwa yamewasilishwa na wadau mbalimbali walioitwa mbele ya Kamati hiyo na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta jedwali la marekebisho wa kuzingatia ipasavyo ushauri muhimu uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya ya utangulizi kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 99, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2021 usomwe kwa mara pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2021, unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria kuu tatu zilizoainishwa kwenye Sehemu ya Pili hadi Sehemu ya Nne ya Muswada. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa matumizi ya lugha ya Kiingereza kama lugha ya sheria na lugha ya mahakama. Kwa upande mahakama na kwa upande wa mabaraza na vyombo vingine vya utoaji haki na badala yake kutumia lugha ya Kiswahili kwa sababu Kiswahili ndio lugha ya Taifa lugha ambayo inaeleweka na inayotumika katika shughuli za maendeleo hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, matumizi ya Kiswahili kama lugha ya sheria na lugha ya mahakama yatasaidia kuboresha upatikanaji wa haki hapa nchini. Sheria zinazorekebishwa kupitia Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

- (i) Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura Na.1.
- (ii) Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216.
- (iii) Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Nne, ambapo Sehemu ya Kwanza inaweka masharti ya awali ikijumuisha jina la Muswada na masharti ya utangulizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura Na.1 ambapo kifungu cha 84 kinarekebisha ili kuondoa matumizi ya lugha ya Kiingereza kama lugha ya sheria za nchi hii na badala yake kutumia lugha ya Kiswahili ambayo ndio lugha ya Taifa. Aidha, marekebisho haya yanaelekeza sheria zote zilizotungwa awali kwa lugha ya Kiingereza kutafsiriwa kwenda lugha ya Kiswahili. Vilevile inapendekezwa kuongeza kifungu kipycha 84A kinachoelekeza kwamba lugha ya mahakama, mabaraza na vyombo vingine vyote vya utoaji haki itakuwa ni Kiswahili. Lengo la marekebisho hayo ni kuwezesha kutumika kwa lugha ya Kiswahili ambayo ndio lugha ya Taifa katika utungaji wa sheria na utoaji wa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na marekebisho haya sehemu hii ya Muswada inapendekeza masharti yatakayowezesha pale inapoonekana inafaa sheria iliyotungwa kwa lugha ya Kiswahili kutafsiriwa kwenda lugha ya Kiingereza iweze kufanyika hivyo. Hali kadhalika vyombo vya utoaji haki vinaweza kutumia lugha ya Kiingereza pale itakapoonekana ni muhimu kufanya hivyo kwa maslahi ya utoaji haki katika mashauri husika. Endapo chombo cha utoaji haki kitalazimika kutumia lugha ya Kiingereza tafsiri ya

mwenendo na uamuji kuhusiana na shauri husika litatolewa mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Waziri mwenye dhamana ya sheria anapewa mamlaka ya kutunga kanuni ili kubainisha mazingira ambayo lugha nyingine inaweza ikatumika katika kutunga sheria. Hivyo hivyo, Jaji Mkuu anapewa mamlaka ya kutunga kanuni kwa ajili ya kutoa mwongozo ili kubainisha mazingira ambayo lugha ya Kiingereza inaweza kutumika katika mfumo wa utoaji wa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu na Sehemu ya Nne zinapendekeza kurekebisha Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216 na Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11 kwa kufuta vifungu vinavyoweka masharti kuhusu lugha ya Mahakama. Mapendekezo haya ya marekebiso yamezingatia marekebiso yaliyofanywa kwenye Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura Na.1 ambapo yameweke misingi kwamba lugha ya mahakama, mabaraza na vyombo vingine vyote venye jukumu kutoa haki itakuwa ni Kiswahili. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena naomba Bunge lako Tukufu Ilijadili Muswada huu wa Sheria ya Marekebiso ya Sheria Mbalimbali ya Mwaka 2021 (*The Written Laws (Miscellaneous) Amendments Act of 2021*) na kuitisha katika hatua ya Kusoma kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebiso yanayopendekezwa yawe sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(*Makof*)

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

No. 2

2021

BILL SUPPLEMENT

to the Gazette of the United Republic of Tanzania No.2. Vol.102 dated 5th February, 2021

Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) ACT, 2021

ARRANGEMENT OF SECTIONS

Section Title

PART I PRELIMINARY PROVISIONS

1. Short title.
2. Amendment of certain written laws.

PART II

AMENDMENT OF THE INTERPRETATION OF LAWS ACT, (CAP. 1)

3. Construction.
4. Amendment of section 84.
5. Addition of section 84A.

PART III

AMENDMENT OF THE LAND DISPUTES COURTS ACT, (CAP. 216)

6. Construction.
7. Repeal of sections 32.

PART IV

AMENDMENT OF THE MAGISTRATES' COURTS ACT, (CAP. 11)

8. Construction.
9. Repeal of section 13.

NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the general public together with a statement of its objects and reasons.

Dodoma,
5th February, 2021

JOHN W. H. KIJAZI
Secretary to the Cabinet

A BILL *for*

An Act to amend certain written laws.

ENACTED by the Parliament of the United Republic of Tanzania.

PART I PRELIMINARY PROVISIONS

Short title 1. This Act may be cited as the Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2021.

Amendment of certain written laws 2. The written laws specified in various Parts of this Act are amended in the manner specified in their respective Parts.

PART II AMENDMENT OF THE INTERPRETATION OF LAWS ACT, (CAP. 1)

Construction Cap. 1 3. This Part shall be read as one with the Interpretation of Laws Act, hereinafter referred to as the “principal Act”.

Amendment of section 84 4.-(1) The principal Act is amended in section 84, by-
(a) deleting subsection (1) and substituting for it the following:
 “(1) The language of laws of the United Republic shall be Kiswahili.”;
(b) adding immediately after subsection (1) the following:

Written Laws (Miscellaneous Amendments)

“(2) Laws of the United Republic that are currently in the English language shall be translated into Kiswahili.

(3) Notwithstanding subsection (1), where circumstances so requires, laws may be translated into English language.”;

- (c) renumbering subsections (2) and (3) as subsections (4) and (5) respectively;
- (d) deleting the word “English” appearing in subsection (5) as renumbered and substituting for it the word “Kiswahili”; and
- (e) adding immediately after the renumbered subsection (5) the following:

“(6) The Minister responsible for legal affairs may make regulations prescribing circumstances and conditions where a law may be in a language other than Kiswahili language.”.

Addition of section 84A 5. The principal Act is amended by adding immediately after section 84 the following:

“Language of courts, etc **84A.**-(1) Notwithstanding any other written law the language of courts, tribunals and other bodies charged with the duties of dispensing justice shall be Kiswahili.

(2) Notwithstanding subsection (1), courts, tribunals and other bodies charged with the duties of dispensing justice shall use the English language as may be determined by the presiding officer where the interests of justice so requires.

(3) Subject to subsection (2), where English language is used in dispensation of justice, that language shall be translated and authenticated in Kiswahili language.

(4) The Minister responsible for legal affairs may, in consultation with the Chief Justice, make regulations for better carrying out the provisions of this section.”.

Written Laws (Miscellaneous Amendments)

PART III
AMENDMENT OF THE LAND DISPUTES COURTS ACT,
(CAP. 216)

Construction Cap. 216 **6.** This Part shall be read as one with the Land Disputes Courts Act, hereinafter referred to as the “principal Act”.

Repeal of section 32 **7.** The principal Act is amended by repealing section 32.

PART IV
AMENDMENT OF THE MAGISTRATES’ COURTS ACT,
(CAP. 11)

Construction Cap. 11 **8.** This Part shall be read as one with the Magistrate’s Courts Act, hereinafter referred to as the “principal Act”.

Repeal of section 13 **9.** The principal Act is amended by repealing section 13.

OBJECTS AND REASONS

This Bill proposes amendment of three laws, namely the Interpretation of Laws Act, Cap.1, the Land Disputes Courts Act, Cap. 216 and the Magistrates’ Courts Act, Cap. 11.

This Bill is divided into Four Parts as follows:

Part I deals with preliminary provisions which include the title of the Bill and the manner in which the laws proposed to be amended are amended in their respective Parts.

Part II of the Bill proposes to amend the Interpretation of Laws Act, Cap.1, where section 84 is proposed to be amended in order to declare Kiswahili as the language of the laws of the country and the language to be used in the administration and dispensation of justice. This amendment is necessitated in cognizance of the use of Kiswahili as a National language vastly used in the day to day activities. Thus, its use will facilitate the realization of access to justice by all. The amendment further gives power to the Minister responsible for justice in consultation with the Chief Justice to determine circumstances and conditions, where the dispensation of justice may be made in a language other than Kiswahili. The amendment also gives power to the Minister responsible for legal affairs to

determine circumstances and conditions where a law may be in a language other the Kiswahili.

Part III and Part IV of the Bill proposes to amend the Land Disputes Courts Act, Cap. 216 and the Magistrates Courts Act, Cap 11. The amendment intends to repeal sections which provide that the language of court or, as the case may be, tribunal shall be English or Kiswahili. The proposed amendments intend to reflect the amendments made in the Interpretation of Laws Act which declared the language to be used in the administration and dispensation of justice is Kiswahili.

MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza marekebisho katika Sheria **Tatu** ambazo ni Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1, Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216 na Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Nne kama ifuatavyo:

Sehemu ya Kwanza ya Muswada inaanisha masharti ya utangulizi ambayo ni jina la Muswada na tamko kuhusu marekebisho ya sheria mbalimbali zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho kupitia Muswada huu.

Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1. Inapendekezwa kufanya marekebisho katika kifungu cha 84 ili kuondoa matumizi ya lugha ya Kiingereza kama lugha ya sheria na lugha ya mahakama na badala yake kutumia lugha ya Kiswahili kwa sababu Kiswahili ndio Lugha ya Taifa, lugha ambayo inaeleweka na inatumika katika shughuli zote za maendeleo nchini. Hivyo, kutumika kwake kutasidua katika upatikanaji wa haki nchini. Marekebisho haya yanakusudia kuimarissha mfumo wa upatikanaji haki kwa wananchi ambao ndio watumiaji wa sheria husika. Aidha, Waziri wa Sheria anapewa mamlaka ya kutunga kanuni ili kubainisha mazingira ambayo lugha nyingine zinaweza kutumika katika kutunga sheria au katika mfumo wa utajiri haki.

Sehemu ya **Tatu** na Sehemu ya **Nne** zinapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216 na Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11 kwa kufuta vifungu vinavyoweka sharti kuhusu lugha ya mahakama. Mapendekezo haya yamezingatia marekebisho yaliyofanywa kwenye Sheria ya Tafsiri za Sheria ambayo imeweza msingi wa lugha ya mahakama, mabaraza na vyombo vingine vyenye jukumu la kutoa haki kuwa ni Kiswahili.

Dodoma
1 Februari, 2021

ADELARDUS L. KILANGI
Mwanasheria Mkuu wa Serikali

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. PROF.
ADELARDUS L. KILANGI, THE ATTORNEY GENERAL AT THE SECOND
READING OF THE BILL ENTITLED “THE WRITTEN LAWS
(MISCELLANEOUS AMENDMENTS) ACT, 2021”**

(Made under S.O. 99(10))

A Bill entitled “The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2021” is amended as follows:

- A:** By deleting Clause 1 and substituting for it the following:
“ Short title and commencement **1.** This Act may be cited as the Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2021 and shall come into operation on such date as the Minister may, by Notice published in the *Gazette*, appoint.”.
- B:** By deleting Clause 4 and substituting for it the following:
“ Amendment of section 84 **4** .-(1) The principal Act is amended in section 84, by-
(a) deleting subsection (1) and substituting for it the following:
“(1) The language of laws of the United Republic shall be Kiswahili.”;
(b) adding immediately after subsection (1) as amended the following:
“(2) Laws of the United Republic that are currently in the English language shall be translated into Kiswahili.
(3) Without prejudice to subsection (1), where circumstances so require, laws enacted in Kiswahili may be translated into English language.”;
(c) renumbering subsections (2) to (4) as subsections (4) to (6) respectively;
(d) deleting subsections (5) and (6) as renumbered and substituting for them the following:
“(5) Where a written law is translated and there occurs a conflict or doubt as to the meaning of any word or expression, the language of the enacting version shall take precedence.”
(6) The Minister responsible for legal affairs may make regulations prescribing circumstances and conditions where a law enacted in Kiswahili may be translated in English.”.
- C:** In Clause 5 by deleting the proposed section 84A and substituting for it the following:
“ Language of courts, etc **84A.**-(1) Notwithstanding any other written law, the language of courts, tribunals and other bodies charged with the duties of

dispensing justice shall be Kiswahili.

(2) Without prejudice to subsection (1), courts, tribunals and other bodies charged with a duty of dispensing justice may, where the interests of justice so require, use English language in the proceedings and decisions.

(3) Where English language is used in the proceedings and decisions, such proceedings and decisions shall be translated and authenticated in Kiswahili language.

(4) Where proceedings or a decision is translated in Kiswahili language and there occurs a conflict or doubt as to the meaning of any word or expression, the language which the proceedings or decision was recorded shall take precedence.

(5) The Chief Justice may, in consultation with the Minister responsible for legal affairs, make rules for the better carrying out of the provisions of subsections (2), (3) and (4).”.

Dodoma,
....., 2021

AG

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeiungwa mkono na tutaendelea sasa na utaratibu wetu, nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kukupa pole wewe pamoja na Bunge letu lote Tukufu kwa kuondokewa na mwenzetu Mheshimiwa *Engineer* Nditiye ambaye kwangu mimi hakuwa rafiki tu, alikuwa ni mtu wangu wa karibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe taarifa yote ya Kamati iingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa hapo mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa uniruhusu kwa mujibu wa kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, niwasilishe maoni na ushauri wa Kamati ya Bunge, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2021 (*The Written Laws (Miscellaneous) Amendment Act of 2021*). Aidha, katika uwasilishaji huu ili kubainisha misingi ya maoni haya itaelezwa kwa muhtasari mambo makuu matatu: Jambo la kwanza ni kuhusu mahudhui ya jumla ya Muswada kama ilivyozingatiwa wakati wa majadiliano kwenye Kamati; Jambo la pili, ni namna Kamati ilivyofanyia kazi Muswada huu; na Jambo la tatu, ni yatokanayo na uchambuzi wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, maudhui ya jumla ya Muswada; kwa ujumla maudhui ya Muswada kama yalivyordhiwa na Kamati yanapendekeza marekebisho katika sheria tatu kama zilivyoainishwa na mtoa hoja. Lengo la marekebisho haya ni kutambua rasmi matumizi ya lugha ya Kiswahili kama lugha ya sheria na lugha ya mahakama kwa madhumuni ya kuimarisha misingi ya utoaji haki katika mfumo wa kisheria nchini kwa kuwawezesha Watanzania walio wengi kuzitambua haki zao zilizoainishwa katika sheria mbalimbali na kuelewa hatima na taratibu za ufuatiliaji wa haki hizo katika vyombo vyao utoaji haki kwa kutumia lugha

ya Kiswahili ambayo ndiyo lugha ya Taifa inayoeleweka kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, namna Kamati ilivyofanya kazi; katika kutekeleza masharti ya 97(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, tarehe 11 na 12 Kamati ilikutana katika Ofisi ya Bunge hapa Dodoma ambapo ilijielekeza katika shughuli mbalimbali za kiuchambuzi kama ilivyoanishwa katika taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yatokanayo na uchambuzi wa Kamati na mantiki ya matumizi ya lugha ya Kiswahili katika uandishi wa sheria na shughuli za mahakama hapa nchini. Kamati imetathimini na kubaini kuwa kukua na kuenea kwa lugha yoyote duniani kunategemea mambo mbalimbali kama vilevile lugha hiyo kutumika katika maeneo ya mifumo rasmi kwenye jamii inayohusika. Kiswahili ni miuongoni mwa lugha ambazo zinakua kwa kasi duniani na chimbuko lake likiwa ni hapa hapa Tanzania. Historia ya Tanzania toka ukoloni hadi uhuru inabainisha kuwa matumizi ya lugha ya Kiswahili yaliwasaidia wapigania uhuru wetu walioongozwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na wazee wetu wengine kutimiza ndogo ya Watanzania ya kupata uhuru, kwa nguvu ya umoja wa kitaifa kutokana matumizi ya lugha ya Kiswahili badala ya kutegemea lugha ya kigeni au lugha za makabila ambazo zilishindwa kuwaunganisha Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo mwaka 1962, mara baada ya uhuru wa Tanganyika, Tanganyika kuwa huru, Kiswahili kilitangazwa kuwa lugha ya Taifa kama moja ya nguzo muhimu ya kutambua utu wa Mtanzania, utaifa na umoja wetu kama Taifa lililo huru. Hatua hiyo ilikiagiza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kitivo cha sheria kupata kamusi ya kwanza ya kisheria iliyotafsiri misamiati ya kisheria ya Kiingereza kuwa lugha ya Kiswahili ilioandikwa na A. B. Weston mnamo mwaka 1968. Kamusi hiyo ni ishara muhimu sana ya dhamira njema na ya uzalendo chini ya Serikali ya Awamu ya Kwanzza katika kuhakikisha kuwa mifumo ya sheria nchini inaandaliwa na kutekelezwa kwa lugha ya

Kiswahili kama lugha iliyoeleweka kwa Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kuhakikisha kuwa lugha ya Kiswahili inatumika kama lugha ya kutumiwa na mifumo ya sheria na vyombo vya kiutawala Tanzania, Katiba ya nchi ya mwaka 1977 iliandikwa kwa Kiswahili na kifungu cha 4 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya kwanza kinaitafsiri na kuitambua Katiba kama Katiba ilyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Hivyo ni dhamira yetu kwamba lugha ya Kiswahili ni lugha yenyewe kubeba utaifa wetu kwa ustawi wa jamii ya Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, hukumu ya Mahakama Kuu Kanda ya Musoma Mjini *Division* ya Kazi katika shauri la maombi ya marejeo namba 23 ya mwaka 2020 baina ya *North Mara Gold Mine Limited* na Gerald Nzumbi, iliandikwa na kutolewa kwa lugha ya Kiswahili tarehe 4 na tarehe 22 Januari, 2021 pamoja na hukumu nyininge za Mahakama ya Kazi, ikiwemo ya muasisi wa Kiswahili nchini marehemu Jaji Mwipopo, Jaji Rweyemamu na Majaji wengi waliopita. Ni hatua muhimu katika historia ya mapinduzi ya kifikra na kisheria kuhusu umuhimu wa mifumo yetu ya utoaji nchini kwa mawasiliano katika shughuli mbalimbali za kiserikali na zisizo za kiserikali, bado imekuwa ikitumika sambamba na lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huu wa lugha kutumika sambamba kwa lugha rasmi nchini unaakisiwa katika tasnia zote za hapa nchini. Miongoni mwa tasnia ambayo imeathiriwa na utaratibu huu ni tasnia ya sheria hapa nchini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya matumizi ya lugha katika tasnia ya sheria nchini; uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa tasnia ya sheria ambayo inahusika moja kwa moja katika utoaji haki, matumizi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza yanaonekana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa kutunga sheria; Kamati imebaini kuwa katika mchakato wa utungaji wa sheria hapa nchini hatua zifuatazo zimekuwa zikifuatwa ambayo lugha ya Kiingereza na Kiswahili zinatumika katika hatua tatu muhimu zifuatazo:-

- (i) Uandishi wa Miswada, unatumia lugha ya Kiingereza;
- (ii) Mjadala wa Miswada Bungeni, unatumia lugha ya Kiswahili ambao unatambulika chini ya kanuni 168(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020;
- (iii) Mjadala wa Muswada ukishakamilika sheria inayotungwa, hutungwa kwa lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, maoni ya Kamati ni kwamba, Bunge lako Tukufu kama chombo cha uwakilishi wa wananchi, mara zote limekuwa likiendesha shughuli zake za msingi kwa lugha ya Kiswahili kama lugha ya Taifa inayoeleweka kwa wananchi kwa lengo la kuzingatia haki ya msingi ya wananchi kufuatilia na kuelewa mambo mbalimbali ya kitaifa yanayohusu Taifa lao na ustawi wao kupitia Bunge lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, utoaji haki mahakamani na kwenye vyombo vingine vya utoaji haki; Kamati imebaini kuwa tangu nchi hii ipate uhuru, lugha ya Mahakama katika ngazi ya Wilaya hadi Mahakama ya Rufaa ni Kiingereza japo mashauri yanaweza kuendeshwa kwa lugha ya Kiswahili, lakini mwenendo wa uamuzi uandikwa kwa lugha ya Kiingereza isipokuwa kwa mahakama ya za mwanzo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, mafunzo ya sheria; Kamati imebaini kuwa mafunzo ya sheria katika taasisi zote za elimu ya sheria hapa nchini kuanzia kiwango cha Astashahada hadi Shahada ya Uzamivu ndani ya na nje ya nchi yanatumia lugha ya Kiingereza. Hata mafunzo ya umahiri katika uandishi wa sheria ambayo yanatolewa katika nchi

ya Jumuiya ya Madola yanatolewa kwa kufundishwa stadi za kuandika sheria kwa lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mazingira haya tathmini na mjadala wa Kamati imebaini mambo makuu manne ambayo yanaweza kulisaidia Bunge lako Tukufu kukubaliana na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu umuhimu wa maudhui wa Muswada huu. Mambo hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Tangu nchi hii ipate uhuru, lugha rasmi ya kisheria Tanzania ni Kiingereza kwa sababu sheria zote isipokuwa Katiba na baadhi ya kanuni na vitabu vingi vya sheria vimeandikwa katika ya lugha ya Kiingereza ambayo ueleweka kwa Watanzania walio wachache;

(ii) Kuwepo kwa hisia mionganini mwa Wanasheria na jamii kwa ujumla kwamba tafsiri ya sheria kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili inaweza isiakisi maudhui yaliyomo ndani ya sheria hizo;

(iii) Changamoto ya rasilimali watu na fedha kwa ajili ya kufanya tafsiri ukalimani na kuandika sheria kwa lugha ya Kiswahili, mfano unaonekana pale Tume ya Kurekebisha Sheria ilipoanza zoezi la kutafsiri sheria nchini kwa Kiswahili, lakini zoezi hili halijakamiliika mpaka sasa; na

(iv) Matumizi ya lugha ya Kiingereza katika kufundisha na kujifunza kuleta ugumu wa kutekeleza maarifa hayo ya sheria kwa lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya kukabiliana na changamoto hizo; Sura ya Saba, ibara ya 145D ya llani ya yetu ya Chama Cha Mapinduzi, chama tawala kilianisha dhamira yake ya dhati ya kuimarisha mfumo wa utoaji haki kwa kuazimia kufanya maboresho katika utendaji wa mfumo wa mahakama na vyombo vingine vya maamuzi pamoja na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Sura ya Sita, Ibara ya 119 ya Ilani ya CCM 2020 - 2025 inaanishwa utekelezaji wa Ibara ya 145D ya Ilani ya CCM ya mwaka 2015 - 2020 kwa kuonesha jinsi Serikali ya Awamu ya Tano ilivyotekeleza matakwa ya ilani hiyo kwa kupitia hatua mbalimbali ikiwemo kuanza kutafsiri sheria 157 kutoka lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili ikilinganisha na sheria 50 zilizokuwa zimetafsiriwa hadi kufika mwaka 2010. Pia Ibara ya 120G katika Sura ya Sita ya Ilani ya CCM ya mwaka 2020 – 2025, imeainishwa dhamira ya kuimarisha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kutoa huduma ya kimahakama na kwenye uandishi wa nyaraka za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huo, hatua ya Bunge la Kumi na Mbili ya kuboresha na kupitisha Muswada huu ni sehemu ya utekelezaji wa dhamira ya Chama Cha Mapinduzi kwa lengo la kuhakikisha wananchi walio wengi wanatambua haki zao kupitia sheria zenye lugha ya Taifa wanayoilewa na namna ya kupata haki hizo kwa kupata fursa ya kufuatilia taratibu za kimahakama na kusoma nyaraka zake zinazowahusu zilizoandikwa kwa lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhusiano uliopo baina ya matumizi ya lugha inayoeleweka kwa wananchi na misingi ya kimataifa ya utawala wa sheria na haki za binadamu; uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa misingi ya Kimataifa ya haki za binadamu na utawala wa kisheria imeianishwa uhusiano ulipo baina ya matumizi ya lugha inayoeleweka kwa wananchi na uwezekano mkubwa wa upatikanaji wa haki za kisheria katika mifumo ya kisheria kwenye nchi inayohusika. Misingi hiyo ya matumizi ya lugha inayoeleweka kwa wananchi walio wengi katika mifumo ya utoaji haki, imeainishwa katika Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la Mwaka 1948 (*The Universal Declaration of Human Right 1948*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 2 ya Tamko hilo inatamka kuwa: “*Watu wote wanastahili kupata haki bila kubaguliwa kwa misingi ya lugha.*”

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 10 inatamka kuwa: "*Watu wanastahili kupata haki kwa uendeshaji wa mashauri ikiwa ni pamoja na kupata tafsiri ya lugha wanayoilewa endapo lugha iliyotumiwa ya mahakama haieleweki ikiwa ni pamoja na haki ya maudhui ya kimantiki ya nyaraka za kimahakama zinazowahu.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Ibara ya 19 inatamka kuwa: "*Watu wote wana haki ya uhuru wa kutoa maoni, mawazo yao ya lugha wanayoilewa kwa chombo cha mawasiliano katika jamii zao.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 27 *The United Nation International Convinent on Civil and Political Rights* iliyoadhimiwa na Umoja wa Mataifa mwaka 1966 inatamka kuwa: "*Watu hawawezi kunyimwa haki zao kwa kigezo cha matumizi ya lugha wasiolelewa.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo Tanzania kama moja ya wanachama wa mikataba hiyo ya kimataifa, ni dhahiri ni kwamba hatua ya matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mfumo wa usimamizi wa sheria ya haki nchini ni sehemu ya utekelezaji wa misingi mbalimbali ya kimataifa kama hiyo ambayo Tanzania ni mwanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, mifano ya Mataifa mengine kuhusu dhana ya matumizi ya lugha inayoeleweka kwa wananchi katika vyombo vya kiutawala; Ireland; Kamati imebaini kuwa Ibara ya 8 ya Katiba ya Ireland ikisomwa pamoja na Sheria ya Lugha Rasmi ya Nchi hiyo ya mwaka 2003 inatamka wazi kuwa lugha ya kia-Irish inatambuliwa kuwa ni lugha ya Taifa rasmi namba moja na kwamba lugha ya Kiingereza itakuwa lugha ya pili ya nchi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Katiba hiyo imeanisha shughuli zote za Serikali katika vyombo vya umma zitatekelezwa kwa matumizi ya lugha ya kia-Irish ikiwa ni pamoja na matumizi ya lugha hiyo ya Taifa katika alama zote za usalama barabarani

Mheshimiwa Naibu Spika, Finland; Kamati imebaini kuwa Ibara ya 17 ya Katiba ya Finland imezuia kabisa ubaguzi wa wananchi wake kwa kigezo cha matumizi ya lugha ya Mtaifa mengine au lugha wasizozielewa vizuri.

Kwa hiyo, katika nchi hiyo lugha inayotumika katika shughuli zote za kiserikali na vyombo vyake ni lugha ya *Ki-Finnish*, na *Ki-swedish* kwa kuzingatia mwingiliano wa kijamii na kitamaduni wa nchi hizo mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kamati ni kuwa Tanzania haitakuwa nchi ya kwanza katika kuifanya lugha ya Taifa ambayo ni lugha ya Kiswahili kuwa lugha rasmi katika mifumo ya kisheria na vyombo vya utoaji haki hapa nchini, kwa kuwa hatua hiyo ni sehemu ya utekelezaji mmojawapo ya misingi ya umuhimu wa haki za binadamu na utawala wa sheria kwa ustawi wa Watanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati, baada ya kuzungumzia masuala ya awali yaliyojenga msingi wa maoni ya Kamati, sasa naomba nitoe maoni na ushauri wa Kamati ambao kwa kiasi kikubwa yamezingatiwa na Serikali wakati wa mashauriano kama yanayoonekana kwenye jedwali la marekebisho lilitowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na lilitosomwa na Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilikuwa na maoni mahususi katika kila ibara za Muswada huu na kutoa mapendekezo ya marekebisho kwa kutoa hoja na kukubaliana na kuboresha masharti yafuatayo:-

(a) Ibara ya tano ya Muswada inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha 84(a) sehemu ya pili kwa kuondoa maneno ya ufunguzi *notwithstanding subsection one* na badala yake kutumia maneno; *without prejudice a subsection one*, lengo la maboresho haya ni kuondoa mkanganyiko unaojitokeza kwa kuzingatia na lengo la Muswada la kutumia Kiswahili kuwa ni lugha ya sheria nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo maboresho haya yanawainisha masharti ya kifungu cha 84(1) kuhusu ulazima wa kutumia lugha ya Kiswahili pamoja na masharti ya fasili ya (2) na sehemu ya tatu ya kifungu hicho. Fasili ya (4) ya kifungu cha 84 inapendekezwa iboreshwé kwa kumpa Jaji Mkuu mamlaka ya kutunga kanuni za uendeshaji wa mashauri kwa lugha ya Kiswahili Mahakamani baada ya Waziri mwenye dhamana ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la maboresho haya ni kuzingatia misingi ya Kikatiba kuwa Jaji Mkuu ndio Kiongozi wa Mhimili wa Mahakama na ndiye aliyekasimiwa mamlaka ya kutunga kanuni za uendeshaji bora wa shughuli za Mahakama hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maboresho yote ya msingi yaliyopendekezwa katika Kamati kama yanavyoonekana kwenye jedwali ni makubaliano kati ya kamati na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa jumla; Kamati ilikuwa na maoni ya jumla kama ifuatavyo:-

(a) Kamati ilikuwa na maoni ya maboresho ya jumla katika ibara ya nne ya Muswada kwa kubainisha kipindi cha mpito ya mambo yanayopaswa kuzingatiwa katika kipindi hicho, kwa mfano ibara ya nne ya Muswada inapendekeza maboresho ya marekebisho katika kifungu cha 84 cha Sheria Tafsiri ya Sheria Sura ya Kwanza kwa kueleza kuwa sheria zote zilizopo katika lugha ya kingereza hivi sasa zitatafsiriwa kuwa katika lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo mapendekezo hayajabainisha muda wa kuanza na kumalizika kwa hatua hii. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa baada ya mashauriano na Serikali, Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati ya kuzingatia kwenye jedwali la marekebisho la Serikali kwa kuweka kifungu kinachompa Waziri mamlaka ya kutangaza tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hii.

(b) Kamati inashauri kuwa kuwepo na mwongozo maalum utakaoainisha namna mashauri yanayoendelea mahakamani hivi sasa namna yatakavyoshughulikiwa.

(c) Taasisi pamoja na taratibu nyingine zitakazo husika katika kutafsiri sheria zilizopo zibainishwe mapema.

(d) Serikali ione ulazima wa kuanisha Sera ya Lugha nchini kwa kuzingatia lugha ya kujifunza kwenye taasisi ya sheria ili kuendana na mazingira ya sasa kwa kuzingatia marekebisheso haya.

(e) Marekebisheso ya kuondoa makosa ya kiuchapaji katika baadhi ya ibara ya Muswada yazingatiwe kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisheso.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; kwa mara nyingine tena naomba nikushukuru sana wewe kwa niaba ya Mheshimiwa Spika kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Katiba na Sheria ili iweze kufanyia kazi jukumu ambalo limetekeliezwa na Kamati kwa wakati na kwaufanisi uliokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, Mbunge pamoja na watendaji wote bila kumsahau Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali yaani *CPD* kwa usikivu na ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanya kazi maoni na mapendekezo ya Kamati kama yalivyoainishwa katika jedwali la marekebisheso.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutambua na kuwashukuru sana wadau mbalimbali waliofika na kutoa maoni na ushauri wao mbele ya Kamati pamoja na wengine waliotoa maoni kwa maandishi, maoni yao yalikuwa ni msaada mkubwa kwa taarifa hii.

Kwa namna ya kipekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa weledi,

uvumilivu, umahiri na kujituma kwao wakati wa uchambuzi wa Muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuboresha Muswada huu, naomba majina yao yote yaingizwe kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge yaani *Hansard* pamoja na taarifa yote hii iliyowasilisha maoni ya Kamati naomba majina yao kama yanavyosomeka yaweze kuingia kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa uongozi dhabiti uliofanikisha uratibu wa shughuli hizi za Kamati, nawashukuru pia watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiwemo Wakurugenzi wa Idara ya Kamati, Ndugu Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerard Magili, Washauri wa Bunge wa mambo ya Sheria Ndugu Prudence Rweyongeza, Ndugu Stephano Seba Mbutu na Ndugu Rehema Kipera.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa nawashukuru sana Makatibu wa Kamati wakiongozwa na Ndugu Stanslaus Kagisa na Ndugu Danford Mpelumbe pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Rachel Masima waliofanikisha kazi ya uchambuzi, ushauri na uratibu wa shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.
(*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nimeshaletewa majina hapa ya wachangiaji, tutapata wachangiaji wa chache sana siku ya leo, tutaanza na Mheshimiwa Najma Giga, atafuatiwa na Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mheshimiwa Edward Olelekaita ajiandae na kila mmoja anachangia dakika tano na kengele itagongwa mara moja, kila mtu ajikadirie muda wake kwa sababu hakuna ule wa niongezee dakika moja nimalizie. Mheshimiwa Najma.

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi nitangulie kusema kwamba

tuwe pole kwa msiba wa mwenzetu aliyetutangulia mbele ya haki na sisi Mwenyezi Mungu atujalie hatma njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile ni dakika tano basi moja kwa moja mimi naomba niende kwenye Muswada huu wa Sheria ambao umeletwa mbele yetu Sheria ya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali ya mwaka 2021 ambayo inakwenda kubadilisha vifungu vitatu Tafsiri ya Sheria Sura Kwanza; Sheria ya Mahakama ya Mgogoro wa Ardhi na Sheria ya Mahakama za Mahakimu Mura ya Pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili siyo la ajabu na wala siyo geni katika ulimwengu huu kwa sababu tunaelewa siyo Tanzania ni miongoni mwa nchi za Jumuiya ya Madola ambazo muda mrefu tumekuwa tukitumia mienendo katika sheria zetu za mahakama na maeneo mengine ya sheria kwa lugha ya kiingereza lakini pia na Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hizi ambazo nyingi zimetawaliwa na koloni la Uingereza ambazo tulikuwa tukizitumia muda mrefu toka wakati huo wa enzi za ukoloni mashitaka mengi yalikuwa yakiendeshwa kwa lugha za kienyeji pamoja na kwamba lugha ya kiingereza ilikuwepo ndiyo *official*. Lengo jamaa na lugha ya rasmi. Kwa hiyo jambo hili ni zuri kwetu litaleta mambo mengi ya faida mimi naweza nikasema mawili tu kwa muda ni mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza tutarahisisha katika utoaji haki. Watanzania walio wengi asilimia kubwa sana wanatumia lugha ya Kiswahili, hawaelewi lugha ya kigeni au ya kitaalamu ambayo inatumika katika sheria zetu. Kwa hiyo itarahisisha namna gani mtua ataweba kupata haki yake kwa urahisi kwa lugha ya Kiswahili kwa kuelewa yale ambayo yanayoendeshwa na yanayotolewa. Lakini hii itakuwa ni endelezo kwa sababu mahakama zetu kama ambavyo wamezungumza wenzangu Waziri wa Katiba na Sheria na Mwenyezeki wa Kamati kwamba mashauri mengi yameshakuwa yanaendeshwa kwa Kiswahili kuanzia ngazi za chini hadi Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hata ukienda kwenye Mahakama nyingine kubwa hukumu zinatolewa kwa Kiswahili, kwa hiyo siyo jambo kubwa sana. Lakini tukija kwenye mifano mingine mimi nitaenda mfano mmoja wa nchi za Jumuiya ya Madola yaani India. India bahati nzuri kwenye Katiba yao Ibara ya 348(2) wamepewa ruhusa Magavana kuomba ruhusa ya kutumia lugha zao za kienyeji kwa Mheshimiwa Rais na hata hivyo nimeona mfano mmoja Haryana wameshaomba mwaka 2020 kwa Mheshimiwa Rais ili watumie lugha ya Hindi katika Mahakama zao. Kwa hiyo hili siyo jambo la ajabu ni jambo la kawaida na kwetu hapa kwa hiyo litakuwa ni jambo la kawaida kabisa kwa sababu Katiba yetu ya Tanzania nayo imetoa ruhusa hiyo Ibara ya 67 sifa za Mbunge awe anajua kusoma na kuandika Kiswahili ama Kiingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tutasema siku moja tuamue kutoa hoja kwa lugha ya kiingereza shughuli itakuwepo, kwa sababu hata Wabunge pamoja na usomi wetu, lakini tumeshazoea kutumia lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo hili ni jambo ambalo lazima tulitilie mkazo.

Lakini faida nyingine ni *promotion* ya lugha ya Kiswahili yaani kuiendeleza na kuikuza lugha ya Kiswahili, lugha ya Kiswahili inatumika na watu zaidi ya milioni 100 katika dunia hii kwa hiyo kuna nchi nyingi ambazo zinatoa taarifa zake kwa lugha za Kiswahili; kuna BBC London tunajua tuna Deutch Welle Ujeruman, kuna Iran, nchi nyingi sasa hivi zinazungumza Kiswahili na zinatoa taarifa ya habari kwa lugha ya kiingereza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia utakuta Mabunge yetu haya *SADC* tayari tumeshatoa fursa hiyo, lakini hata na maeneo mengine mengi tutaweza kuzungumza, *East Africa Community* tayari inatumia Kiswahili. Kwa hiyo niseme tu ushauri uliotolewa na Kamati ni mzuri kwa sababu muda ni mfupi, lakini tusifikirie kwamba itakuwa ni jambo rahisi najua tutakuwa na gharama zitakuwepo za kutafsiri lugha hii kuingia Kiswahili haina shida jambo zuri lote linatakiwa gharama, lakini pia na muda kama alivyosema Mwenyekiti wangu lazima

tuanze vile vitu vya vipaumbele kwanza tutizame nini tunaanza nacho kwa awamu alafu baadae tunaendelea na vingine hadi tutaflikia mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, na pia wataalamu wetu wasiwe na hofu ya kutafsiri lugha kutoka kiingereza kuja Kiswahili. Kiswahili ni lugha ya kirafiki kabisa jamani ni lugha nzuri ambayo inaenda kwa namna zote lazima tukubaliane kwamba asilimia 30 ya maneno ya Kiswahili yanatokana na lugha za kigeni tumeyatoho kutoka kwenye lugha za Kiarabu, Kihindi na Kingereza, lakini pia tuna asilimia kama kumi kutoka nchi za Kiafrika kwa maana *bantu languages* au lugha za kibantu tuna maneno mengi tumeyatoho kama asilimia kumi.

Kwa hiyo, haitakuwa tatizo tukiona kuna tatizo wanasheria/wasomi kwamba lugha hii kwamba tunashindwa kuitafsiri basi tutohoe tu kwa mfano naweza kutumia neno moja *locus stand* tukiitafsiri kwa urefu wake itakuwa ni shida kwamba lazima mtu awe na haki ya uwezo wa kufikisha shauri mahakamani au kulismamia, litakuwa ni neno refu kwa hiyo tukishindwa tuna sema hana *locus* ama anayo *locus*. Kwa hiyo nafikiri tutaelewana kwa sababu sote tunakubaliana hapa kwa maneno mengi tunayotumia hata katika ibada zetu makanisa na misikiti malaika, shetani, thawabu, dhambi zote zinatokana na lugha za kigeni lakini tumezitoho zimekuwa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana, naomba tuupitishe Muswada huu kwa heshima zote. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Shukrani sana. Natamani kusikia michango ambayo ni Kiswahili mwanzo mwisho bila mtu kuchanganya ili sisi wenyewe tuanze hapa jamani. Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Olelekaita, Mheshimiwa Joseph Tadayo, ajiandae.

MHE. NG'WASI D. KAMANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ya mimi pia kupata kuchangia

juu ya Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2021, ambao lengo lake kuu ni kuhakikisha kwamba lugha ya Kiswahili inakuwa lugha ya sheria katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa lugha yetu ya Kiswahili kama ilivyowasilishwa katika maoni ya Kamati ni lugha ya Taifa na ni lugha ambayo ilikuwa na msingi mkubwa sana katika kutuunganisha kupigania Uhuru. Kwa hiyo lugha hii inajenga dhana nzima ya uzalendo kati yetu sisi Watanzania na kuzidi kuitangaza na kuitangaza nchi yetu katika nchi zote za kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ametangulia kusema msemaji aliyejita kwamba kigezo cha Mbunge katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kujua kusoma na kuandika. Lugha ya kiingereza ni lugha ambayo tumeipokea, ni lugha ya kimapokeo kutoka katika nchi zingine, kwa maana ya kwamba kigezo cha kujua kusoma na kuandika kinajumlisha tu kujua lugha yetu ya Taifa. Hivyo sheria zikiletwa kwa lugha ya Kiswahili katika Bunge hilli tukufu na amini hata sisi Wabunge tutapata nafasi nzuri zaidi ya kusoma sheria hizo, kuzielewa na kuweza kuzichangia kwa manufaa mazima ya Watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukipitisha pia sheria hii na kuifanya lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya kisheria hii nayo itakuwa inajumlisha kabisa haki ya Mtanzania kuweza kuelewa mambo yote yaliyomzunguka, wote tunafahamu kwamba kila kinachofanyika katika nchi yetu kinafanyika kwa misingi ya sheria, kama Mtanzania hata pata nafasi ya kusoma sheria na akazielewa kwa sababu anashindwa kuelewa lugha iliyotumika kuziandika sheria hizo maana yake moja kwa moja tunamzuia Mtanzania huyu kuelewa haki zake na wote tunafahamu kwamba *ignorantia juris non excusat* kwamba *ignorant of law is not an excuse*. Sasa Watanzania wasipoelewa lugha zao maana yake tunaweza moja kwa moja kuwakosesha haki zao za msingi kabisa za kuendelea na maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kama tulivyoeleza katika ripoti ya Kamati sisi hatutakuwa wa kwanza kuifanya lugha yetu ya taifa kuwa lugha ya kisheria. Nchi mbalimbali zimekwisha fanya hayo na ikawezekana mabadiliko yanachukua muda na gharama lakini naamini faida kubwa tutakazozipata za kiuchumi na hata za haki na usawa katika nchi hii zita-*justify* matumizi mazima ya lugha yetu ya Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo kwa kusema haya naomba Bunge hili Tukufu lipitishe mabadiliko haya ya sheria. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Edward Olelekaita atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Tadayo, Mheshimiwa Salome Makamba ajiandae.

MHE. EDWARD K. OLEKAITA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii na kama walivyosema wenzangu niwape pole sana Wabunge kwa msiba wa Mbunge mwenzetu *Engineer Nditiye*, tunamuombea Mwenyezi Mungu ailaze mahala pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda ni mdogo sana naomba nichangie hoja hii kwa kusema hivi llani ya Chama cha Mapinduzi 2020/2025 imetaja Kiswahili mara 39 namna tunavyotaka kutumia Kiswahili kwa mustakabali wa Taifa letu. Ukurasa wa 17, 130, 167, 168, 184, 185, 186, 244, 246, 247, 268, 286,287 na 288. Ukitiwa llani ya Chama cha Mapinduzi uitaona Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli alivyofafanua namna tunavyotaka kutumia Kiswahili, kwa Muswada huu utatusaidia kama Taifa kuanza kubadilisha sheria zetu kwa lugha ya Kiswahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na nnikinukuu tu kwa ruhusa yako ukurasa wa 167; "Kuongeza uwelewa wa wananchi kuhusu sheria mbalimbali kwa kutafsiri sheria 157 kutoka lugha kiiingereza kwenda ya lugha ya Kiswahili." Kwa hiyo, takwa hili la kubadilisha sheria kwenda Kiswahili ni kwa mujibu ya llani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama walivyokwisha kutangulia wengine Kiswahili kwa Taifa letu inatambulisha Taifa, Kiswahili kimetumika katika ujenzi wa Taifa letu hata wakati tunatafuta uhuru Kiswahili kinaleta utamaduni wa Taifa letu. Kiswahili ni sawa sawa na uzalendo, ukombozi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiswahili ni tunu ya Taifa letu. Kwa hiyo, tumpongeze sana Mheshimiwa Rais ni wakati sasa wa muafaka tuanze kuzungumza Kiswahili kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti nyingi zinaonesha nchi nyingi sana Finland, Ireland, Bangladesh, Malaysia, Hong Kong, Hong Kong ilifika mahala wakaanza kuandamana nchi nzima wanakataa kiingereza kisitumike kwa sababu waliokuwa wengi Hong Kong wanazungumza *chinese* sasa sisi tumeanza hata hata kabra ya Watanzania hawajaanza kuandamana.

Lakini sababu nyingine kimsingi sana ya kisheria ni haki ya mtu kufahamu lugha ya mashitaka kwa kiingereza wanaita *due process*, huwezi kumshitaki mtu ukaleta hati ya mashitaka kwa lugha ya kigeni, haelewei.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nyingine kuna kitu kinaitwa kwa kisheria uhalali wa lugha inayotumia (*legitimacy*) Watanzania wengi wanaongea Kiswahili kuendelea kuwa na sheria zilizoandikwa kwa lugha za kigeni ni kukosesha *legitimacy* sheria zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa na lugha ya Kiswahili kwenye sheria zetu, kwanza inajenga uelewa, vilevile inaleta watu kuheshimu sheria kwa sababu wanafahamu sheria kwa Kiswahili, wanafahamu lugha tulioandikia sheria. Lakini ukileta sheria zilizoandikwa kwa lugha za kigeni tutakuwa tunawasumbua Watanzania wasipo fuata sheria kwa sababu lugha hiyo imeandikwa ni ya kigeni. Kwa hiyo inaleta *obedience*, inaleta *respect* kama unaelewa lugha hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada ulio mbele ya Bunge umeandikwa kwa kiingereza na kanuni zetu zinachanganya *by the way* na hukumu zetu sasa kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati zimeshaanza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili, kwa hiyo mabadiliko ya sheria yatarahisisha sana kazi hii ya tafsiri ya sheria zetu ziende kwa lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama walivyokwisha kusema wengine nchi zinazozungumza Kiswahili sasa ni Rwanda, Uganda, Burundi, South Sudan, sehemu ya Mawali, Somali, Zambia, Mzumbiji, DRC na Visiwa vya Comoro. Kwa hivyo Kiswahili tayari kina soko kubwa sana ni zaidi ya watu milioni mia mbili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Tadayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Makamba, Mheshimiwa Dkt. Abdullah Mwinyi ajiandae.

MHE. JOSEPH A. TADAYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niipongeze Serikali kwa kutuletea Muswada huu katika wakati huu ambao ni muafaka. Naomba nieleze kabisa hapo kwamba mimi nimekuwa Wakili wa Kujitegemea kwa takribani miaka 25 sasa, kwa hiyo, nimeshuhudia hizi changamoto zinazozungumziwa juu ya ugumu wa kupata haki au wa kufikia haki kwa kutumia lugha ambayo si ya mhusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakimu wetu na Majaji na Waendesha Mashtaka wamepata taabu kidogo katika kuendesha mashauri wakati ambapo sheria inataka yawe kwa kiingereza. Kwa hiyo, wanasiliza kwa Kiswahili, wanaandika kwa Kiingereza baadaye wanaandika hukumu kwa kiingereza, lakini wanapata taabu tena kuanza kuwatafsiria watu na mtu anasomewa shitaka inabidi

litasiriwe kwanza. Kwa hiyo, kwa kweli imekuwa ikileta changamoto kubwa. Niwapongeze Mahakimu wetu, Majaji na wadau wengine wamejitalidi sana katika kwenda katika ugumu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka mwaka 2007 Mahakama za Kazi zilishatutangulia, ziliundwa zile *Labour Court Rules* (Kanuni za Sheria za Mahakama za Kazi za mwaka 2007) ambazo ziliruhusu matumizi ya Kiswahili. Kwa hiyo, Mahakama zetu zimefanya juhudhi kubwa, na zipo hukumu nydingi za kuanzia wakati wa Mheshimiwa Marehemu Jaji Mwaipopo, Jaji Rweyemamu na hata Jaji Samatta katika hukumu ile ya Kesi ya Dibagula, ile kesi maarufu iliyotokea Morogoro, walijitalidi kufanya hivyo. (*Makofii*)

Sasa tunapofikia mahali pa kuwatungia sheria nadhani tunairahisisha hii kazl, itafanyika vizuri na ninaamini sasa Serikali itawekeza, kwa hiyo, hata ile shida, changamoto walizokuwa wanapata zitapungua na haki itatendeka kwa vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeandikwa kwa Kiswahili na Kiingereza, lakini kwa kutambua umuhimu wa Kiswahili kama lugha ya wengi, imeelekezwa kwamba panapokuwa na mgongano basi ile tafsiri ya Kiswahili ndiyo ambayo itazingatiwa. Sasa umefika wakati kwa sheria zetu ambazo zinatungwa chini ya mamlaka ya Katiba hiyo nazo pia zitungwe kwa Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo tukumbuke kwamba katika mihimili mitatu ambayo inaundwa chini ya Katiba yetu; Serikali, Bunge na Mahakama, mihimili miwili tayari inatumia lugha ya Kiswahili, umebakia Mhimili mmoja tu wa Mahakama. Nadhani sababu ya kutumia Kiswahili katika mihimili hii miwili ni kuwezesha huduma yake kufika kirahisi na wale wahudumiwa/wananchi, waweze kuifikia hii mihimili. Mahakama imebaki peke yake, wakati umefika sasa mahakama nayo itumie Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Taarifa ya Kamati ilivyoeleza ni kwamba kile kifungu cha 84(1) kinaelekeza kwamba lugha ya Mahakama zetu na vyombo vingine vya kutoa haki iwe Kiswahili na hiyo ni kwa sababu ya kuwahudumia walio wengi. Lakini kifungu hiki cha 84(2) kinazungumzia sasa haki za wale walio wachache kwamba endapo watu watakuja Mahakamani na wanapenda kesi yao iende kwa Kiingereza basi wanaruhusiwa pia kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusipofanya hivyo tukakamilisha huu Muswada kama ulivyoletwa nadhani tutaingia kwenye tatizo, wanaharakati wanaweza siku moja wakajitokeza hata wakatushtaki kwamba tunaingia kwenye lile kosa, sasa unisamehe kwamba lazima nitumie Kiingereza kuna kitu wanaita *class legislation*, kwamba tunatunga sheria ambazo zinahangaika na tabaka moja tu.

Lakini katika kutibu hilo kuna kitu wanaita *reasonable classification* ambacho ndicho kilichofanyika hapa; kwamba tunawahudumia wale walio wengi lakini pia wale walio wachache nao pia wanapata nafasi ndani ya sheria hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni wa kihistoria, kwa hiyo ni vizuri tukaupitisha kwa umakini wote. Lakini pia naamini Serikali itawekeza ipasavyo katika *ku-manage* hiki kipindi cha mpito ili sheria hizi zitafsiriwe vizuri na tufikie mahali ambapo tutaendesha mashauri yetu kwa lugha ya Kiswahili bila kuathiri haki za watu na bila kuwapa ugumu utakaokwamisha utoaji haki wale ambao wanahuksika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ukienda kwenye mpango ambao tumemaliza kuujadili siku ya leo, unasisitiza juu ya suala la utawala bora. Utawala bora utafikiwa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana.

MHE. JOSEPH A. TADAYO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Abdullah Mwinyi, Mheshimiwa Noah Mollel ajiandae.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie Muswada huu muhimu wa kubadilisha lugha za kisheria na Mahakama katika nchi yetu kuwa Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ieleteweke kwenye Bunge lako tukufu kwamba hakuna mtu anayepinga kutumia lugha ya Kiswahili kwenye mahakama; hakuna na hata sheria yenye inayobadilishwa, *Cap 1* ilisema kabisa. Kifungu cha 84 nitajitahidi kutumia Kiswahili kwa sababu tunabadilisha Kiswahili. Kifungu cha 84 kinasema kugha ya sheria za Tanzania itakuwa Kiingereza au Kiswahili au vyote; kwa hiyo hakuna anayepinga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, isipokuwa, kikubwa ambacho mimi nataka nishauri; Mwalimu Nyerere mwaka 1983 alitamani lugha iwe Kiswahili tu. Na baada ya kufanya hivyo, pamoja na mamlaka aliyokuwa nayo hakukimbilia kusema wote tuzungumze Kiswahili mahakamani. Alikwenda kwenye kubadilisha kamusi, tupate kamusi ya Kiswahili yenye maneno ya kisheria, itakayotumika kwenye sheria. Akaenda tukajaribu kufanya hivyo na mpango ule uli-*fail*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ambacho mimi nataka nishauri Bunge hili tukufu; ni lazima tujitathmini, kwa hatua ya sasa, je, tupo tayari kubadilisha lugha ya Mahakama na lugha ya sheria iwe Kiswahili peke yake? Hasa ikizingatiwa kuwa tunayo changamoto kubwa sana ya namna ya kutohoa maneno ya Kiswahili ili yaweze ku-*fit* kwenye lugha ambayo tunaitumia ya Kiingereza ambayo imeshapimwa,

imeshakuwa *tested and well...*, imeshapimwa na ikathibitika kwamba maneno yale yako sahihi. Najaribu kutumia maneno mazuri ya Kiswahili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna changamoto kubwa, changamoto ya kwanza ni kwamba Tanzania siyo kisiwa na hatuwezi kusema tunaweza kusimama kama kisiwa. Mimi nilipokwenda kwenye Kamati niliwauliza; hivi ni nchi gani ambayo inatumia lugha yake ya asili katika mambo haya ya kimahakama? Sasa mifano ambayo tunapewa kwenye Kamati wanasema kuna nchi kama Finland, Ireland na Hong Kong.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi nchi *population* yake ni chini ya milioni 10. Wana uwezo hata wa kuwaajiri watu wake wote na wasipate ombwe la ajira. Sisi tunalazimisha tutumie Kiswahili halafu tumejadili hapa wiki nzima tuna changamoto ya ajira ndani ya Tanzania, tunataka tutumie Kiswahili kwenye mahakama zetu.

Sasa hivi tu tunatumia Kiingereza kwenye Mahakama, Mawakili wetu *Chief Justice* anasema hawajui Kiingereza kwenda kwenye Mahakama nyingine za nje. Sasa pata picha tumetumia Kiswahili mwanzo mwisho. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mitaala yetu tunafundishwa kwa Kiingereza, kuanzia *form one* mpaka chuo kikuu ni lazima usome Kiingereza. Ukifika kwenye Mahakama kwenye *ku-practice* unaambiwa utumie Kiswahili. Ni lazima tufanye maandalizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yenye we imekiri walijaribu kutafsiri sheria ziende Kiswahili *wame-fail*. Kamati yenye we inakiri *Law Revision Commission* (Tume ya Mabadiliko ya Sheria) kwa mara ya mwisho imefanya kazi mwaka 2002, miaka 19 iliyopita, hawajafanya...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba, kuna Taarifa. Mheshimiwa Agness Mathew Marwa. Zima kwanza hiyo ya mwanzo uliyokuwa umebonyeza.

TAARIFA

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampa taarifa muongeaji kwamba anasema Kiswahili kinalazimishwa kubadilishwa, je, wapiga kura wake walimpigia kura kwa Kiingereza? (*Kicheko/Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba niendelee na hii ndio changamoto tuliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sheria kuna kitu kinaitwa *jurisprudence of law*. Tunao majaji ambao wanatoa hukumu nzuri kweli kweli ambazo zinatumika kwenye *common law*, kwenye nchi mbalimbali. Hukumu hizi zinapokwenda kutumika kule zinakuza tasnia ya sheria katika nchi yetu. Sisi tumekomaa tunataka hizi hukumu zitoke za Kiswahili. Sasa tunataka tusonge mbele kwenye tasnia ya sheria kiuchumi, wakati huo huo tunataka tukuze Kiswahili kwa sababu ni uzalendo, tunu za taifa, yaani hatujui tunataka nini kwenye nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua ukiwa mzalendo halafu hauna uchumi, ni sawasawa na kuwa mwanaume mwenye ndevu halafu haumiliki uchumi, yaani hauna hela. Unakuwa tu kama Mzee Kambale, yaani una ndevu, una masharubu lakini mwisho wa siku haumiliki uchumi wa dunia. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Taarifa.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, leo China inaheshimiwa kwa sababu uchumi wake uko imara, kila mtu anang'ang'ania...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: ...kujifunza Kichina kwa sababu kujua Kichina ni uchumi.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, muda wako umekwisha Mheshimiwa Salome Makamba, ahsante sana.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa, naomba mkae wote wawili, muda wake umekwisha.

Mheshimiwa Dkt. Abdullah Mwinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa Noah Mollel, Mheshimiwa Hadija Taya ajiandae.

MHE. ABDULLAH ALI MWINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote ninapenda na mimi kutoa pole zangu kwa wafiwa wa Mheshimiwa Nditiye na tunawaombea wapendwa wake wote subira katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa wasaa huu nami kuchangia mawili/matatu katika mada hii muhimu na nyeti sana. Walionitangulia hasa Mheshimiwa Olelekaita na Mheshimiwa Tadayo, wameyazungumza mengi ambayo kwa kiasi kikubwa wamenifilisi yale ambayo nilitaka kuyasema, lakini ninapenda tu kusema hakuna mtu ye yeyote mwene akili timamu anayeweza kubisha umuhimu wa mchakato wa kutoa haki kuwa katika lugha ambayo wengi wetu ndani ya nchi wanaifahamu. Hilo halina mjadala wa aina yoyote. Sasa lazima tuseme hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumetokea kidogo hofu katika tasnia ya sheria kwa wale ambao walishazoea na walishapata mafunzo kwa lugha ya Kiingereza. Mabadiliko ya aina yoyote lazima yatakuwa yana ugumu wake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1973 sisi kama Tanzania tuliamua kufanya Dodoma uwe Mji Mkoo. Tukachukua hatua za awamu hadi awamu lakini ile azma yenye haikufika ikatokea Awamu ya Tano na Rais, Dkt. Magufuli, akafanya maamuzi ya kuhamisha mji kufika Dodoma; tuko hapa. Tulilalamika hivi hivi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika katika lugha ya Kiswahili katika mihula yote miwili na sehemu kubwa huu muhula wa mahakama Kiswahili kinatumika. Lakini kuna hofu ya kwamba tukifanya kwa haraka pengine tutaleta athari ikatufanya sisi kama kisiwa. Hiyo hofu ipo lakini msiwe na wasiwasi. Sheria hii imegusia hayo, imeweke bayana kwamba lugha ya Mahakama ni lugha ya Kiswahili, lakini pale haki itakapohitajika kutendeka kwa kutumia lugha nyingine ruksa. Sasa msiwe na wasiwasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Salome ana wasiwasi huo, *jurisprudence* sijui kwa Kiswahili itakuwaje, nadhani itakuwa jurisprudensi, itajijenga upya kwa lugha ya Kiswahili na tutatafsiri na Jumuiya ya Madola itatuelewa. Lakini umuhimu wa kwanza ni kwa wananchi wetu na umuhimu wa kwanza wa misingi ya haki za binadamu na utawala bora inatulazimisha sisi kuhakikisha lugha ya kutoa haki ni lugha ile ambayo wengi wetu wanaielewa. (*Makofi*)

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mchengerwa kwa kifupi.

TAARIFA

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa msemaji kwamba kamusi ya kwanza iliyotafsiri lugha ya kisheria kutoka lugha ya kisheria ya Kiingereza kuwa lugha ya sheria ya Kiswahili ilisainiwa na aliyekuwa Waziri Mkuu, Mzee wetu Kawawa mwaka 1968 na iliandaliwa na Kitivo cha Sheria Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Abdullah Mwinyi, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. ABDULLAH ALI MWINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea tena kwa shangwe kubwa sana. Inaonesha bayana kwamba huu mchakato haukuanza leo, toka mwaka

1962 ulikuwepo na hatua hadi hatua mpaka tumefika kilele hiki cha leo cha kutunga hii sheria. (*Makofii*)

Sasa sheria hii na mabadiliko haya yamezingatia mambo yote ambayo ni ya msingi na ninapenda kuwaomba wenzangu kuiunga mkono na mimi pia naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Noah Mollel, atafuatiwa na Mheshimiwa Hadija Taya, Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana ajiandae.

MHE. NOAH L. S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia muswada huu. Lakini na mimi niungane na wenzangu kutoa pole sana kwa familia ya ndugu yetu ambaye ametangulia mbele ya haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakwenda moja kwa moja kujielekeza kwenye kuunga mkono muswada huu wa kuweka Kiswahili kitumike kwenye sheria zetu na sababu yenye ni kwamba ili lugha yoyote iweze kuwa na uhalali, lazima watumiaji wake wawe ni kwa kiwango kikubwa katika sehemu husika.

Kwa minajili hiyo, Kiswahili Tanzania kinazungumzwa na zaidi ya wazungumzaji asilimia karibu 90; asilimia 10 iliyobaki ndiyo inazungumza hiyo lugha nyingine ya kigeni. Kwa hiyo tayari imeshajihalalisha kwamba Kiswahili ni halali kitumike Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni ufanisi wake, kama tutazungumza lugha ya kigeni na ufanisi wake hauwezi kukaa vizuri mionganoni mwa jamii tunayoiongoza, tutakuwa hatujatenda haki.

Lakini pia haki za binadamu zinatutaka pia tuhakikishe wananchi wetu wanapata haki za binadamu dhidi ya mazungumzo, kwa sababu unapozungumza lugha usiyoijua

inakuwa ni utata na hatimaye unaathirika. Kwa hiyo, hayo ni mambo ambayo tunatakiwa tuyaangalie...

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umetubana sana, hii itakuwa ni taarifa ya mwisho, Mheshimiwa Salome Makamba, sekunde 30.

TAARIFA

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba sheria ilivyo sasa hivi kabla hatujabadilisha kwenye muswada huu inasema lugha ya Mahakama ni Kiswahili na Kiingereza au vyote viwili.

Kwa hiyo hakuna sehemu inayosema lugha ya Mahakama ni Kiingereza, ni *attitude* za watu wetu wanaopracticesheria ndio wanaotumia Kiingereza peke yake. Kwa hiyo, nadhani tunatakiwa tubadilishe mtazamo wa watu wanaofanya kazi za sheria kuliko kusema kwamba Kiswahili hakitumiki.

NAIBU SPIKA: Haya, ahsante sana; Mheshimiwa Noah Mollel, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. NOAH L. S. MOLLEL: *Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei taarifa hiyo na siipokei kwa sababu pia mtoa taarifa ni tabia zao za kutokuwa na heshima, kwa hiyo nadhani siipokei taarifa hiyo. [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Noah Mollel, hilo neno la kutokuwa na heshima liondoe halafu umalizie mchango wako.

MHE. NOAH L. S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, nafuta, ahsante sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee, hizi hofu kwanza kabisa za kusema kwamba Tanzania tunakwenda kuji-*isolate* siyo kweli kwa sababu Tanzania kama Tanzania lazima tuwe na haki ya kumiliki lugha yetu, hiyo ndiyo sifa yetu, ndiyo itatutangaza duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini kama wenzangu walivyosema, Hong Kong kwa mfano, wananchi walipopiga kelele Serikali ilikuja na muswada wakasema tunahitaji Kichina kiwekwe kwenye sheria zetu. Mwaka 1995 Jaji wa Kwanza wa Kichina alitoa hukumu ya Kichina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini tarehe 11 Machi, 1996 Mahakama zote nchini China zilitoa hukumu kwa lugha ya Kichina kuanzia makosa yote ya jinai na madai, kwa nini sisi Tanzania tunakuwa na hofu? Kazi hii ya kutumia Kiswahili illanza muda mrefu. Mwaka 2001 kulikuwa na shauri ambalo lilitolewa la Hamisi Rajab Dibagula dhidi ya Jamhuri, 2001 na lilizungumzwa kwa Kiswahili. Kwa nini tunakuwa na hofu?

Pia sheria hii ilibainisha wazi kwamba pale ambapo haki inatakiwa kutendeka, *parties* kwa maana ya pande mbili zitaamua zitumie lugha gani, sasa tunataka nini? Tunataka kuenzi vyta wageni, vyta wakoloni? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hadija Taya atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana.

MHE. HADIJA S. TAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuzungumza leo mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikupe pole wewe pamoja na Bunge lako Tukufu na Wabunge wote kwa kuondokewa na kipenzi chetu, rafiki yetu, Mheshimiwa Nditiye.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa mbele kuzungumza juu ya hii sheria ambayo imekuja kuhusu kutumia Kiswahili katika Mahakama zetu. Mimi naona umuhimu wa hili. Nitashangazwa sana kama kuna mtu ataona hakuna umuhimu katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa msanii kwa muda mrefu sana na katika tasnia ya sanaa, kikubwa sana kilichokuwa kinatufanya tupoteze haki zetu ni kwa sababu ya kutokujua lugha ya Kiingereza ambayo ndiyo ilikuwa inaandikwa katika mikataba yetu mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi sana wamepoteza haki zao, wengi sana wamepoteza uwezo, mpaka sasa ambapo tumeweza kuwa na uwezo wa kumiliki Wanasheria. Kwa muda huo tulikuwa hatuna uwezo wa kuwa na Mwanasheria, fedha hizo tulikuwa hatuna. Kwa hiyo, nafahamu umuhimu wa kutumia Kiswahili katika hizi Mahakama zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongee jambo lingine kwamba tulipopata safari ya kwenda China kupata mafunzo ya Chama cha Mapinduzi, nilipendezwa sana na tabia za Wachina. Vile vikao vilikuwa vinaendeshwa kwa lugha ya Kichina japokuwa wanajua kuzungumza Kiingereza. Wanazungumza Kichina, anatokea mkalimani anazungumza Kiingereza, halafu sisi mwenzetu anazungumza Kiingereza halafu anatafsiri kwa Kiswahili. (*Makofii*)

Mheshimiwa naibu Spika, kwa hiyo, tunatakiwa tutambue umuhimu wa hii lugha kwa sababu itatuletea heshima kama Watanzania. Watanzania wengi wanakwenda China wanafanya biashara na Wachina wengi wanakuja Tanzania wanafanya biashara pamoja na kutokujua lugha lakini wanafanya biashara. Kwa hiyo, naomba Bunge hili Tukufu liunge mkono hoja hii kwa kutambua umuhimu wa uzalendo wa nchi yetu na Mheshimiwa Rais ameonyesha uzalendo wa nchi yetu kwa kuzungumza Kiswahili katika vikao vyake vyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hii hatua ambayo tunakwenda kutumia Kiswahili katika Mahakama zetu ni heshima kubwa sana kwa Tanzania. Kama kuna mtu ambaye hawesi kufahamu hili, namshangaa kwa nini amekuja kuwa Mbunge kwa ajili ya kuwawakilisha wananchi wake ambao wanazungumza Kiswahili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lugha ambayo tunatumia hapa Bungeni ni Kiswahili, nasi ndiyo watunzi wa hizi sheria. Kwa hiyo, nashangaa kwa nini mtu hawesi kuona umuhimu wa kutumia sheria ya Kiswahili au kutumia Kiswahili katika Mahakama zetu kwa ajili ya kutoa haki? Hatujakataza kutumia Kiingereza, endapo kutakuwa na uhitaji wa kutumia Kiingereza watatumia, lakini bado itatafsiriwa kwa Kiswahili ili iweze kutusaidia baadaye kwa ajili ya *records*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naunga mkono hoja hii ilioletwa na Mheshimiwa Waziri, kama Mwanakamati wa Katiba na Sheria na Mwanasheria mpya sasa. Nashukuru sana kwa kuchangia leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana atafuatiwa na Mheshimiwa Twaha Mpembewi.

Waheshimiwa Wabunge, kabla Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana hajaanza kuongea, mtakubaliana na Mheshimiwa Spika anavyowarudisha kule mlilotoka mkikata kati ya Mbunge na Kiti hapa. Mheshimiwa Waziri Mkuu amefika na amekaa pembeni ili yule Mbunge amalizie kuzungumza. Kwa hiyo, tunaendelea kukumbushana, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushukuru kwa kuonyesha mfano mzuri. (*Makof*)

MHE. DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nianze kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania kutoa pole kwa mwenzetu ambaye ametangulia mbele ya haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja nianze kwa kuunga mkono hoja. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, hivi karibuni katuonyesha mfano wa umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika maamuzi ya Mahakama. Mheshimiwa Rais amempandisha cheo Mheshimiwa Jaji aliyetoa hukumu kwa lugha ya Kiswahili. Kwa kweli huu ni mfano wa kuigwa na ni maboresho ambayo ni muhimu sana. Nami najiuliza, ilikuwaje siku za nyuma hili hatukuliona? Kimsingi jambo hili liliipaswa kuja mapema, lakini sasa limekuwa wakati muafaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Nina sababu nyingi kwa nini naunga mkono kwamba lazima sasa tutumie lugha ya Kiswahili. Tunapotumia Kiswahili, hiki kifungu cha 84 kama kinavyoeleza katika Muswada huu wa Marekebisho Kimesema pale, *"The language of the laws of the United Republic of Tanzania shall be Kiswahili."* Napigia mstari neno "shall" and not "may". Ni muhimu sana tuzungumze Kiswahili. Watanzania takribani milioni 60 lugha yetu ya Taifa ni Kiswahili. Wanawake katika idadi ya watu ni takribani asilimia 51 ya idadi ya watu na vijana ni takribani asilimia 60, wote hawa wanajieleza vizuri sana kwa lugha ya Kiswahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo faida za kutumia Kiswahili. Unapotumia lugha ya Kiswahili, kuna sheria, kwa mfano, tunapoambiwa huruhusiwi kushika nyara za Serikali halafu nyara zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza, masuala ya *Government trophy*, unaambiwa ngozi ya nguchiro ni nyara za Serikali, hiki na hiki ni kosa la jinai, halafu iko kwa Kiingereza. Hivi hawa wananchi wa kule Njombe, Iringa, Ludewa wanaelewa? Kwa hiyo, hilli ni jambo la kupongezwa sana kutumia lugha ya Kiswahili. Hii lugha ya Kiswahili kwanza itapunguza hata uhalifu kwa sababu mtu akisoma anajua kumbe hii ni nyara ya Serikali. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

MHE. DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ni kengele ya msemaji aliyepita ya kwangu bado.

NAIBU SPIKA: Ni ya kwako mwenyewe Mheshimiwa.

MHE. DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni ya kwangu? Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Twaha Mpembenwe dakika tatu halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Ulega.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii nami kuwa mchangiaji siku ya leo. Awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kukupa pole wewe pamoja na Bunge letu Tukufu kwa kuondokewa na mwenzetu, kipenzi chetu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia Muswada huu, naomba niseme neno moja tu kama siyo mawilli. Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wakati anaingia madarakani mwaka 2015, kauli yake kubwa sana ilikuwa ni kwamba yeye ndiye Rais wa wanyonge na hayo yamethibitika. Ameweza kulipigania hilo katika kuhakikisha mwananchi wa kawaida anakwenda kutetewa hali yake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la mambo ya kisheria sisi kama Wawakilishi wa Wananchi yanatukuta kule chini katika Mahakama za Mwanzo na Mahakama za Wilaya. Lugha inayotumika kule ni Kiingereza. Anakuja mwananchi ameshinda kesi, lakini hajui kama ameshinda kwa sababu lugha iliyokuwa imetumiwa mle ni “yes”, “no”. Kwa hiyo, hii inakuwa ni shida kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi niseme tu Muswada huu ulioletwa umeletwa hapa, namshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Vilevile nampongeza Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mwenyekiti na timu yake nzima ya Kamati ya Sheria. Muswada huu ni sahihi, umekuja katika kipindi kinachofaa kabisa ili sisi Wawakilishi wa Wananchi twende kule chini tukawatetee wananchi wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, Kiswahili ni lugha ambayo inastahiki iendelee kutumika kwa sababu kubwa moja ya kulinda tamaduni zetu. Watoto wetu hawa sasa hivi wanaingia katika mitandao hii, kuna mambo mengi yanafanyika kule. Tutakapokuwa tunaitumia lugha yetu ya Kiswahili, ndiyo tutakapoweza kulinda tamaduni zetu hasa mambo haya ya kisasa; ndoa hizi za wenyewe kwa wenyewe, sijui rika moja, mwanaume kamuoia mwanaume, mwanamke inakuwa shida. Mambo haya yanarithiwa kwa sababu ya kutumia lugha za watu. Mheshimiwa Rais ameonyesha uzalendo na amepambana sasa hivi Kiswahili kinatumika kule SADC kama moja ya lugha ambayo inatumika katika mikutano yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena nishukuru, lakini nimpongeze tena Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba pamoja na Kamati yote kwa ujumla, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Abdallah Ulega, atafuatiwa na Mheshimiwa Geofrey Mizengo Pinda na mtoa hoja atafuatia.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kwa kukupa pole nyingi kwa msiba wa ndugu yetu Mheshimiwa Eng. Nditiye.

Mheshimiwa Naibu Spika, njielekeze katika kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais, mtunukiwa wa tuzo ya juu ya Kiswahili katika nchi yetu, tuzo ya Shabani Robert ambapo wanapewa watu mahususi, watu mashuhuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nitoe pongezi na shukrani nyingi sana kwa Wizara yetu ya Katiba na Sheria, kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba hongera sana

na Kamati yetu; kaka yangu Mheshimiwa Mchengerwa, hongereni sana kwa kazi kubwa na nzuri mliyoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuhakikisha Mahakama inatumia lugha ya Kiswahili ni jambo jema na zuri sana. Wengi wamesema juu ya kuhakikisha tunawasaidia Watanzania ili waweze kupata huduma kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii mabenki ambayo yanakopesha Watanzania mpaka yale madogo madogo kwa lugha ya Kiingereza “*microfinances*” mikataba yote wanayopewa ni kwa lugha za Kiingereza. Mama yule anayekwenda kupata mkopo ule anapewa mkataba kwa lugha ya Kiingereza. Mwanzo mliouanza kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu ni mzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, huduma zetu za Bima, Uhamiaji na huduma nyingine zote hutolewa kwa lugha ya Kiingereza. Hili ni jambo zuri mlilolianzisha na Kiswahili ni biashara kubwa. Juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anajibu swali hapa siku ya Alhamisi alisema kwamba Serikali inajielekeza katika kuhakikisha Kiswahili kinakwenda kuwa biashara kubwa katika dunia na hata kufungua vituo. Ikiwa kama Wazungu, Waarabu, Wareno na wengineo wameweza kufungua vituo katika nchi mbalimbali duniani ikiwemo nchi yetu, nasi ni lazima tuanze.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia hofu ya baadhi ya Waheshimiwa Wabunge akiwemo Mheshimiwa Makamba juu ya kwamba Kiswahili bado hakijajitosheleza, ni lazima tuanze. Jambo lolote linahitaji kuanza. Kulikuwa na hofu hapa ya kuhamia Dodoma, kulikuwa na hofu hapa ya kutengeneza *SGR* lakini sasa tunakwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Jambo ni jema, ni zuri, tusonge mbele. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Geofrey Mizengo Pinda, halafu mtoa hoja, ajiandae.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kupata nafasi hii nami kama Naibu Waziri wa Katiba na Sheria nipate nafasi ya kuchangia kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wote, kwanza ndugu zangu ambaeo ni Wawakilishi wa Wananchi, kama kuna eneo ambalo tulikuwa tumeliacha likiendelea kutawaliwa ni hili la utoaji haki. Kwa sababu mwanzo wa matumizi ya Kiingereza katika utoaji haki ulianzia kwa Wakoloni. Nchi yetu imepata uhuru kamili na sasa tuna miaka ya kutosha kabisa katika uhuru wetu. Kwa hiyo, utaona namna ambayo kuchelewa kutumia lugha ya Kiswahili katika utoaji haki ilikuwa ni kuendelea kukandamizana katika maeneo ya maisha yetu ya kila siku. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, itambulike tu kwamba sheria ndiyo msingi wa maisha. Sheria ni makubaliano ya jamii kuishi katika mfumo fulani na kuuheshimu. Sasa huwezi kuleta zile sheria na miundo hiyo kwa lugha ambayo wewe mwenyewe hujui. Waingereza walileta lugha hii kwa sababu ndiyo walikuwa wanatutawala. Sasa hata baada ya kutawaliwa, tuendelee tu kusimama kwenye eneo lao? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachotaka kusema ni nini? Kiswahili kinaheshimika sana kote duniani na mtakubliaiana nami kwamba kwa sasa hivi Mataifa mengi sana yamefungua TV za Kiswahili. Ukienda Ujeruman, Korea, Japan, BBC wote hawa wanatuenzi Watanzania ambaeo hatujajitambua thamani yetu. Sisi tunathaminika sana duniani, lakini sisi wenyewe hatujajithamini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ufike na kila jambo linahitaji uthubutu. Mheshimiwa Rais asingekuwa mthubutu tungeendelea kuimba wimbo wa kuhamia Dodoma hata miaka 500 ingepita bila kufika hapa Dodoma. Sasa ifike wakati, tunataka kubadilisha miundo ya maisha yetu ili wananchi wetu ambaeo ndiyo wanufaika wakubwa waweze kunufaika na lugha yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingi sana nimeshuhudia akina dada, akiwa mjamzito Tanzania anataka kwenda kuzalia Ulaya ili aandikishe uraia wa Ulaya. Sasa sijui ni mawazo tu ambayo mtu anakuwa nayo ya kuathirika kisaikolojia, lakini ukweli Tanzania yetu ni Tanzania ya Kiswahili. Kwa hiyo, sheria zetu zikibadilika zitawasaidia sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi migogoro ni mingi. Hapa nina *judgment* zilizotolewa kwenye Mahakama karibia sijui *copy* ngapi, wananchi hawajui namna ya kuzitafsiri, wanatafuta Mkalimani awatafsirie. Acha hao Waingereza watafute mtafsiri wa Kiswahili, siyo kazi yetu sisi tulio wengi kutafuta watafsiri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini wazi mawazo ya Waheshimiwa Wabunge ambayo yamelenga katika kukubaliana na wazo la Wizara, ni vizuri mkayapa nguvu ili muweze kufika mahali tuweze kukubaliana na hii hoja iliyowasilishwa na Wizara ili tuweze kufikia muafaka wa lugha ya Taifa kutumika mahali popote pale kwa ujasiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nimwite sasa mtoa hoja, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Katiba na Sheria aje ahitimishe hoja yake.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa nafasi hii na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa hoja walizotoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni moja ya hoja ambayo kwa kweli hatukupaswa hapa Bungeni kugawanyika kwa sababu jambo tunaloongelea lina miongozo mikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Kiswahili ni lugha ya Taifa letu na Sheria Mama ya Nchi yetu ambayo ni Katiba imeliweka wazi kwamba lugha itakayotumika ni Kiswahili; na pale ambapo pana mzozo katika eneo ambalo lugha

nyingine imetumika, itakayaoshika hatamu ni Kiswahili.
(Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, baada ya kuwa Mheshimiwa Rais wetu, mbeba maono ameona kuna upungufu katika jambo hili la kutumia lugha ya Kiingereza katika uendeshaji wa shughuli zetu akaanza ye ye mwenyewe kutolea mfano na hajakwama popote, sanasana amesaidia kunusuru hata fedha zilizokuwa zinapotea kwa watu kupata shida katika kuwasiliana wanapojadili mambo ya mikataba na hata kusaini mikataba. Akaanzisha ye ye kuwa mfano kila anapokuwa na shughuli ya Kiserikali anatumia Kiswahili na hili jambo limewezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasi kama Wizara tukasema tutafuata nyendo hiso hiso, twende kwenye utaratibu wa kutumia Kiswahili. Itashangaza sana Mwakilishi wa Wananchi ambaye ametumwa na wananchi, anawajua wananchi walivyo, anakuja kusema kwamba "unajua tukitumia Kiswahili wale watu wa nje hawataelewa tulichokiongea." Hivi sheria tunamtungia nani? *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wengi wanaumia, wanakosa haki kwa vile tu sheria na yale mambo wanayokatazwa yameandikwa kwa lugha wasiyolelewa na hata anapohukumiwa, anahukumiwa kwa lugha ambayo haielewi. Sasa wakija na wale wengine amba wanatamani wapate biashara kwa ajili ya kumtetea mtu, yule ambaye hajasoma kile kilichoandikwa huenda angeridhia hata asingekata rufaa lakini anaambiwa tu unajua usipokata rufaa sasa kwa yule shughuli inaishia hapo, anaridhia tu kwamba basi endelea nalo lakini hajui wanachoendelea nacho ni kipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge hata kabla hatujaanza mchakato huu, Mahakama walishaanza utaratibu huu. Mwenye mhimili (Jaji Mkuu) hata kabla hatujapitisha sheria alishasema miutasari yote ya hukumu itaanza kutolewa kwa Kiswahili, maana yake ni kwamba hiki ni kitu kinachowezekana. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine sheria zote zitakwenda kutafsiriwa kwa lugha yetu. Tuna wataalam na tumeshajaribisha kwenye ngazi nyingine Serikali za Mitaa walishaanza uandishi huo hata Mahakama zingine zile za mwanzoni kule walishaanza kufanya namna hiyo, hili ni jambo ambalo linawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Jaji Mkuu ambaye ni kiongozi wa mhimili alichokuwa anasema kifanyike ni kwanza tubadilishe sheria ambayo inasema lugha ya sheria na ya Mahakama itakuwa Kiswahili ili Hakimu ye yote yule anayetaka kuandika kwa Kiswahili asiwe anavunja sheria. Hawa ndio wanaofanya shughuli hizo wanaasema jambo hili linawezekana, mwingine ambaye hafanyi shughuli hizo ambaye anatetea wale ambao hawako hapa anasema unajua tukifanya hivi tutawakwaza. Hatutungi sheria kwa ajili ya mataifa mengine wala wananchi wa mataifa mengine, tunatunga sheria kwa ajili ya wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata nilipoongea na marafiki wa Majaji walikuwa wananiambia, wakasema unajua Majaji tunawapa kazi kubwa sana. Wanawasiliza watuhumiwa wanapofika pale wanapo jieleza kwa Kiswahili, wanawahoji kwa Kiswahili, wanawasiliza mashahidi na kuandika mashahidi walichokuwa wanasema kwa Kiswahili na mpaka wanafika hatua zile zingine zote kwa Kiswahili, wanaenda kupata shida kwa sababu unapotafsiri kile kinachoandikwa kwa Kiswahili ili wewe ukipeleke Kiingereza wanapata shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano mmoja alikuwa ananiambia kwa mfano mtu yuko na kasi yake ya kuongea, wewe unatakiwa uibadilishe upeleke kwenye Kiingereza, anasema wal nichoma singe, unaanza kutafuta hii wal nichoma singe maana yake, inabidi tu uandike neno singe uende kuanza kutafuta kamusi ili uibadilishe upeleke kwenye Kiingereza. Sasa utumwa wote huu wa nini yaani wewe mwenyewe Ms wahili, unayemhoji ni kwa Kiswahili na makosa yake ni Kiswahili, hata unapolala unaota Kiswahili halafu unajifungia tu mahali ili umridhishe nani? Unaenda

kuanza kuhangaika kujipa utumwa kuandika kwa Kiingereza.
(Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa hili anatulindia uhuru wa Taifa letu. Tuache ule utumwa wa kuwaza kizamani. Lugha ya Kiswahili ililikomboa Taifa letu pamoja na mbinu zingine za kutumia kama timu ya Yanga hivi, lugha ya Kiswahili ndiyo iliyokuwa inawaunganisha Watanzania katika kupigania uhuru wakiongozwa na Mwalimu Nyerere. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa nimetoa ufanuzi huu, niwatoe hofu sisi Wizara tutaandaa utaratibu pamoja na kushirikiana na mhimili katika utekelezaji wa jambo hili. Hapatakuwepo na matatizo yoyote kwenye utekelezaji, tutaweka utaratibu mzuri. Mahakama wameshaanza tayari kubadilisha Kanuni zao, wataweka utaratibu mzuri. Tutaweka kipindi cha mpito ambacho ni kizuri wakati tunatafsiri sheria ambazo ni rejea katika majukumu haya yote. Hili jambo litafanyika kikamilifu na kwa sababu hatubadilishi hili kwa ajili ya wiki moja, ni jambo la kudumu, kule tunakokwenda baadaye hata hatutakuwa na matatizo ya aina hii lakini ilikuwa lazima tuwe na mahali pa kuanzia. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishawapongeza Simba basi niwatakie na Namungo ambaao nao wanawakilisha Taifa wakacheze kwa viwango vyta uchumi wa kat. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naomba kutoa hoja. *(Makof)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sijaona wakisimama kuunga mkono hoja.

WABUNGE FULANI: Hajatoa hoja.

NAIBU SPIKA: Ametoa hoja.

Waheshimiwa Wabunge, tuwe tunasikilizana. Ukiiongea sana unakuwa huna fursa ya kusikiliza wenzako.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono, tutaendelea na utaratibu wetu, Katibu.

NDG. NENELWA WANKANGA – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2021 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Bill, 2021*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae. Katibu.

Ibara ya 1

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya BungeZima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 2

Ibara ya 3

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya BungeZima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 4

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwenye Ibara hii naomba kuongeza kifungu kidogo cha (4) ambapo kifungu kidogo cha (2) na (3) kinasema lugha itakayotumika kwenye Miswada wakati tunafanya marekebisho ni Kiswahili na kwa ajili ya kutenda haki lugha ya Kiingereza inaweza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kifungu kidogo cha (4) nachotaka kuongeza na nimeomba iandikwe hivi: “Without prejudice to the provisions of subsection (2) and (3) laws translated in either English or Kiswahili language as the

case may be in the case of conflict or doubt as to the meaning of any word or expression, the version of the language in which the law was enacted shall take precedence.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yangu ni kwamba kama imetokea, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwamba tutabadiilisha sheria zetu nyngi ambazo ziko kwa Kiingereza ziende kwenye Kiswahili, ikitokea kuna mgongano kati ya ile tafsiri na ile sheria basi lugha ya asili iliyotumika kwenye utungaji wa sheria ile ndiyo ambayo itashika hatamu, nimesikia neno jipya Mheshimiwa Waziri, yaani ndiyo itakayosimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nashauri hivyo.
(Makofii)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jinsi tulivyolijadili jambo hili na tulivyojadiliana na Kamati, anachokisema Mheshimiwa Mbunge kinalingana na tulichokisema kwamba kwa sababu lugha ambayo itakuwa inatumika kama lugha ya sheria na lugha ya Mahakama itakuwa ni Kiswahili mazingira yale ambayo anayaangalia kwa sura tofauti tuliyaacha sisi kuyawekea kwenye sheria kwa sababu tuliacha mazingira kwamba inaweza ikatokea kwa maslahi mapana tu ya Kitaifa jambo hilo linaloamuliwa halitumii lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwa maana ya mhimili umejiridhisha kwamba kwa ajili ya maslahi mapana ya Taifa kwenye jambo hilo kukawa na maridhiano, Kanuni zitatungwa kwenye mazingira ya aina hiyo ili kuweza kufanikisha lile linalolengwa, lugha inayoweza kutumika ikawa nyngine kwenye kile kipengele tulichoacha kwamba kuna mazingira yanaweza yakatokea inayotumika ni hii. Tukaona tuiache wazi kwa sababu ukisema tena lugha ambayo itashika hatamu itakuwa iliyotumika kwenye kutungia maana yake itakuwa inapingana na hicho tulichoweka kwamba

yanaweza yakatokea mazingira ambayo yanaweza yakaruhusu lugha nyingine kutumika. Kwa hiyo, sisi tukaona pale ambapo tutakuwa tumesema kuna mazingira yanatakiwa itumike lugha fulani maana yake kama kuna utata ndiyo inakuwa sababu iliyofanya kutumike lugha fulani. Kwa maana hiyo katika mazingira yale ile lugha ambayo iliruhusiwa kufuatana na mazingira yale ndiyo ambayo inatakiwa itumike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mazingira ya aina hii ambayo yanaweza yakajitokeza, tuliona tusifunge kabisa kabisa kwa sababu wenyewe mhimili wameshauri hivi kwa kuzingatia mazingira wanayokutana nayo kazini. Tukisema itatumika iliyotumika kutungia sheria maana yake tufute hiki kipengele, kwa lugha rahisi maana yake tufute kabisa uwezekano kwamba kuna eneo yanaweza yakaja mazingira hayo kwa sababu tutakuwa tumeshasema kwa vyovyyote vile sisi tutatumia ile ile. Tuliweka mlango mmoja kwamba inaweza ikatokea kwa maslahi mapana tu ya sheria na wenyewe wanajua na maslahi mapana ya Taifa ikawa imetumika hivyo.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Salome.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunatunga sheria na sheria lazima iwe *clear* na *precise*. Hizo *assumption* ambazo Mheshimiwa Waziri anazitengeneza hata tuliopo humu ndani tukijaribu kuzi-*imagine* hatuzipati.

Mheshimiwa Naibu Spika, *point* yangu ni nini? Sheria zote zilizoko humu ndani tumezitunga kwa Kiingereza na tumezijadili kwa siku na siku na kuumiza akili, sasa zinakwenda kutafsiriwa na watu wachache kwa muda mfupi. Inawezekana wakati wanatafsiri wakawa wametengeneza tafsiri ambayo siyo ilikuwa imedhamiriwa na Bunge wakati tunatunga sheria hiyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu kwenye kifungu hiki...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salome, ngoja tusaidiane vizuri. Ile sheria yenyewe inayobadilishwa, unayo hapo?

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo.

NAIBU SPIKA: Kama unayo, hicho kifungu unachotaka wewe kuongeza kipo tayari kama namba (3) na (4). Sasa hiki kifungu cha 84 ndicho kinachobadilishwa hapa lakini haya mabadiliko yanayowekwa hayaondoi huo uwezekano ambao wewe unausema sasa hivi. Ukitoma kifungu kidogo cha (3) na cha (4) yaani hiki unachopendekeza kiwepo hapo maana yake vifungu vitakuwa vimejirudiarudia kwa sababu haya mabadiliko hayajaondoa hicho kifungu chenyewe halisi. Kwa hiyo nadhani utakipitia hapo taratibu. (*Makofii*)

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, twende polepole kidogo. Hii sheria yenyewe *general rule* ni kwamba lugha ya kisheria ni Kiswahili, *general rule*. Sasa...

MWENYEKITI: Ngoja, ngoja. Hapa sasa tutachukua muda mrefu, hebu nenda kwenye (c) ya huu Muswada tunaoujadili.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kinasema *renumbering subsection (2) and (3) as subsection (4) and (5) respectively*.

MWENYEKITI: Ina maana gani? Si ina maana unavibadilisha hivi hapa ambapo maana yake bado kipo ama kuna mahali umesoma kinafutwa?

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana. Nachokitaka mimi, utanielewesha kama nakosea, naomba kuongeza kifungu kipyaa.

MWENYEKITI: Sawa, kifungu kipyaa hatutaweza kukiongeza kwa sababu muktadha wake uko tayari kwenye hii sheria ambayo huu Muswada hauifuti. Ndiyo maana

nimesema uipitie taratibu vile vifungu vy a ile sheria yenewe halafu uone inavyosema.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, muktadha ambao mimi nauongelea wa kulazimisha inapotokea kwamba sheria imetafsiriwa halafu ile tafsiri ama iwe ya Kiswahili au ya Kiingereza inakinzana na sheria asilia ya sheria ile...

MWENYEKITI: Ngoja nikusomee Mheshimiwa.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, sawa.

NAIBU SPIKA: Ili tuendelee, muda wetu unakimbia kidogo.

"Where any written law is translated from one language into another and published in both languages, then in the case of conflict or doubt as to the meaning of any word or expression the version of the language in which the law was enacted shall take precedence. (Makof)

Nadhani hapo tunaweza kuendelea.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 5

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Concept* ya marekebisho yangu ya kwanza inakwenda kwenye kifungu hiki. Kwenye kifungu hiki naongelea mwenendo wa kesi na hukumu. Kama kutatokea mgongano kati ya lugha iliyotumika kwenye mwenendo wa kesi na hukumu *versus* lugha ilio tafsiriwa kwenye mwenendo ule wa kesi. Kesi iliendeshwa Kingereza mwanzo mpaka mwisho halafu ikaja ikatafsiriwa Kiswahili pakatokea mgongano hapo kati ya tafsiri ya lugha au muktadha basi

lugha asili ya mwenendo wa kesi na hukumu ile ndiyo isimame.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo msingi wangu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa hoja ya marekebisho ya Mheshimiwa Salome Makamba ni maudhui. Anachosema kwamba kifanyike ndicho kilichosemwa kwenye 84A inayotungwa. Sasa ukisema kama ikitokea sheria ya mwanzo ilikuwa kwa lugha ya Kiingereza na sasa sheria ile kwa maana ya *ku-prevail* kati ya sheria ya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza itumike lugha ile, msingi mzima wa hili lote tunalolifanya linakuwa ni kaazi bure. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pale 84 wamesema kama kutatokea katika utoaji wa haki ili kuhakikisha kwamba haki imetolewa itahitajika kutumika lugha ya Kiingereza, Kiingereza kitatumika. Ukishafanya hivyo umeshaondoka kwenye tatizo lote lile ambalo linampa mashaka.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Salome Makamba.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, unless Mheshimiwa Simbachawene alikuwa anamaanisha mwenendo wa kesi na hukumu basi nitapokea hivyo lakini pamoja na maelezo yako, kwenye mwenendo wa kesi hapo hapo anaposema kwa *interest of justice* tumeamua tuachane na Kiswahili, mwenendo wa kesi uwe kwa Kiingereza na hukumu itoke kwa Kiingereza labda kwa sababu *parties* ni watu ambao wanazungumza Kiingereza basi hukumu itatoka kwa Kiingereza. Ikitoka kwa Kiingereza sasa huo msingi wa 84(A)(1) unasema lazima itafsiriwe kwa Kiswahili. Sasa hoja yangu baada ya kutafsiri unaweza ukaleta mgongano...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salome, umepata marekebisheso ya Serikali tunayoyasema hapa? Maana kifungu hiki kina marekebisheso ya Serikali na ya kwako, ya Serikali umeyapata? Hebu angalia kwenye kishkwambi naambibiwa mmeshawekewa, hebu angalia kwenye kishkwambi chako.

Waheshimiwa Wabunge, hiki kifungu anachokisema Mheshimiwa Salome kwamba kiongezwe nakiona kwenye namba 4 kwenye marekebisheso ya Serikali. Nadhani wote mmeshayapata, nadhani yako hapo. (*Makofi*)

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisheso yake)*

Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zillipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

NDG. NENELWA WANKANGA – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

(Bunge Lilitrudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja Taarifa.

TAARIFA

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2020, napenda kutoa Taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Marekebisheso ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2021, Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na marekebisheso yake yaliyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2021 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2021*] kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(*Makofî*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji kuhusu kuridhia Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2021 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2021*] kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

NAIBU SPIKA: Walioafiki wameshinda, Katibu. (*Makofî*)

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali zipatazo tatu kwa lengo la kuondoa matumizi ya Lugha ya Kingereza kama Lugha ya Sheria na Lugha ya Mahakama na badala yake Kutumia Lugha ya Kiswahili (*A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws in order to Declare Kiswahili as the Language of the Laws of the Country and the Language to be used in Administration and Dispensation of Justice,*

(*Kusomwa Mara ya Tatu*)

(*Muswada wa Sheria wa Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa na Bunge*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa sehemu yetu tumeshamaliza utaratibu wa kutunga hii sheria ama mabadiliko haya ya sheria mbalimbali, kama yalivyoletwa. Kwa hivyo, nichukue fursa hii kuipongeza sana Serikali kwa jambo hili kubwa ililolileta na Waheshimiwa Wabunge kwa michango mbalimbali mliyoitoa na mingine imeonesha dhahiri kwamba katika Muswada huu mawazo yenu Waheshimiwa Wabunge mliyoyatoa kwenye ngazi ya Kamati yalizingatiwa. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kusikiliza mawazo ya Waheshimiwa Wabunge lakini pia tunawashukuru Wabunge kwa namna mlivyoshiriki zoezi hili zima la kuhakikisha tunakienzi Kiswahili chetu kila mahali ambapo tunatumia lugha kuwasiliana. Kwa hiyo, ni jambo jema Mahakama zetu kuanza kutoa haki kwa lugha ya Kiswahili lakini pia sisi Wabunge kuanza kutunga sheria kwa lugha yetu adhimu kabisa. (*Makof*)

Kwa utaratibu tulionao baada ya kupitisha sasa Muswada huu utaelekea kwa Mheshimiwa Rais, kwa mujibu wa Katiba yetu Ibara ya 97(1), Mheshimiwa Rais na yeye atafanya kwa sehemu yake. Kwa hiyo, tunawatakia kila la heri katika utekelezaji, hasa Wizara ya Katiba na Sheria kwa sababu, Mahakama inapitia huko. Kwa hiyo, tunawatakia kila la kheri na tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake kwenye jambo hili. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo mawili hapa, lakini kabla ya matangazo niwakumbushe kidogo, Kanuni ya 175 tukaisome vizuri. Kipindi hiki tulinyamaza kidogo lakini Mheshimiwa Spika akishatoa pole anakuwa ametoa kwa niaba ya Bunge lote na Wabunge wote. Kwa hiyo, Mbunge akisimama hatarajiwi tena kuanza na yeye kutoa pole zake peke yake, Mheshimiwa Spika anakuwa ameshasema kwa niaba yetu na ndivyo Kanuni zinavyosema. Tena imeandikwa hairuhusiwi, ili utunze muda wako wa hoja usiutumie kwenye kuzungumza jambo ambalo Mheshimiwa Spika ameshalitolea maelekezo. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge ninayo matangazo mawili. Tangazo la kwanza ni kupokelewa kwa Gazeti la Zanzibar

Leo (Toleo Maalum), ambalo linaelezea kazi ambazo amezifanya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, katika siku 100 baada ya kuingia madarakani. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, wote mtagawiwa Toleo hili Maalum kuendelea kuona kazi nzuri zinazofanyika Zanzibar lakini juhudhi kubwa anazozichukua Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kuhakikisha nchi yetu inasonga mbele. Mnatarajiwa katika kipindi hiki mtakuwa mnapitia na wengi wenu bado mnajifunza, kwa hiyo, wote tunaendelea kujifunza namna ya kufanya kazi. (*Makofii*)

Lipo pia tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge kuhusu warsha mbalimbali zinazotolewa kwa njia ya mtandao na Umoja wa Mabunge ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Madola (*Commonwealth Parliamentary Association – CPA*). Katibu anawatangazia kwamba, kozi hizi zitaanza tarehe 23 - 08 Machi, 2021. Warsha hizi zipo katika maeneo yafuatayo:-

(i) *National Action Towards Climate Change: Role of Parliaments and Parliamentarians of the Commonwealth.*

(ii) *Promote and Respect for International Humanitarian Law: Placing Humanity First*

(iii) *Social media: A curse or a Blessing.*

(iv) *Leading the Way: How the Commonwealth can empower persons with Disability.*

(v) *Youth quakes: Rising Youth Activism in the Commonwealth.*

Waheshimiwa Wabunge, wote ambao watapenda kushiriki wanaweza kujunga kupitia, sasa hapa tena pameandikwa *link*, sasa hii *link* sjui hatuna kwenye Kiswahili hii, kupitia *link* ambayo imewekwa kwenye vishkwambi vyenu na katika, eeh *website*, haya mtandao wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani mmesikia kwa hiyo, mtapitia huko halafu kila Mbunge atawea kujiandikisha anataka kushiriki kozi ipi.

Baada ya matangazo haya, nimkaribishe sasa Mheshimiwa Spika kwa ajili ya kuendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Hapa Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

SPIKA: Katibu.

NDG. NENELWA WANKANGA – KATIBU MEZANI:

TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE

SPIKA: Taarifa ya Katibu wa Bunge.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 35(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kutoa Taarifa kwamba shughuli zote zilizowekwa kwenye Orodha ya Shughuli za Mkutano wa Pili wa Bunge, sasa zimemalizika.

SPIKA: Ahsante sana Katibu kwa Taarifa hiyo muhimu. Sasa naomba nimuite Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa ajili ya kutoa Hotuba ya Kuahirisha Bunge. Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu sana. (*Makofii*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutujalia afya njema hadi leo hii tunapohitimisha shughuli zote zilizopangwa katika Mkutano huu wa Pili wa Bunge la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, naungana tena na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za pole kwa Bunge lako Tukufu kwa familia za waliokuwa Wabunge wenzetu: Mheshimiwa Martha Umbula, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara; na Mheshimiwa

Eng. Atashasta Nditiye, aliyejekwa Mbunge wa Muhamwe Mkaoni Kigoma, waliotangulia mbele za haki wakiwa wanaendelea na kutumikia Taifa. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azipumzishe roho zao kwa amani.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwapa pole Watanzania wenzangu waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki na wengine kusababishiwa madhara mbalimbali kutokana na ajali za barabarani na matukio mengine. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atupe subra na awape nafuu majeruhi wetu wapone haraka.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana wewe binafsi, Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kusimamia kwa umahiri mkubwa majadiliano ya hoja kuhusu kujadili Hotuba ya Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyoitoa tarehe 13 Novemba, 2020 wakati akifungua Bunge la Kumi na Mbili sambamba na Mpango wa Taifa wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge kwa pongezi zenu kwa Serikali na kwa michango yenu yenye dhamira ya dhati kabisa ya kuboresha mipango na kazi zilizokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika kipindi chote cha miaka mitano. Mjadala huu umeendelea kuthibitisha uimara wa Bunge letu katika kutekeleza wajibu wake wa Kikatiba wa kuishauri na kuisimamia Serikali kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge 164 na Waheshimiwa Mawaziri saba (7) walichangia hoja ya kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyoitoa tarehe 13 Novemba, 2020 wakati akifungua Bunge la Kumi na Mbili. Aidha, Waheshimiwa Wabunge 126 nao pia walipata nafasi ya kuchangia Mpango wa Taifa wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, jumla ya maswali 125 ya msingi na mengine 289 ya nyongeza yaliulizwa

na Waheshimiwa Wabunge na kupatiwa majibu na Serikali. Kadhalika, maswali 14 ya papo kwa papo yaliulizwa na kujibiwa na Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, natambua kuwa shughuli za utangulizi za Mkutano huu zilianza tarehe 18 hadi 31 Januari, 2021 kwa vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge sambamba na Chaguzi za Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge. Hivyo, nitumie fursa hii kwanza kuwapongeza wajumbe wote kwa kufanikisha upatikanaji wa viongozi wa Kamati hizo ambao wameaminiwa na kuchaguliwa kuongoza Kamati zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matarajio yangu kwamba tutatumia nafasi hizo vizuri katika kuleta ushirikiano, mshikamano na kufanya kazi pamoja kama wawakilishi wa wananchi na kutekeleza majukumu yetu kwa kuisimamia na kuishauri Serikali. Serikali kwa upande wake, itaendelea kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Kamati hizo ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuhakikisha kwamba tunaboresha utendaji kazi na uwajibikaji hususan wakati huu tunapoelekea kwenye maandalizi ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, vilevile, nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Naibu Mawaziri kwa kujibu vizuri pamoja na kutoa ufanuzi wa kina kuhusu hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2021 uliowasilishwa na Serikali katika Mkutano huu. Aidha, Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu, Wakaguzi wa Hesabu wa Mwaka 2021 (*The Accountants and Auditors (Registration) (Amendment) Act, 2021*) pamoja na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2021 (*The Written Laws (Miscellaneous*

Amendments) (No.2) Act, 2021) iliyosomwa kwa mara ya kwanza katika Mkutano huu.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri wakati wa kujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2021 ambao kwa msingi wake ulikusudia kufanya marekebisho katika Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1; Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11; na Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216. Lengo la marekebisho hayo ni kuweka msingi wa lugha ya Mahakama, Mabaraza na vyombo vingine vyenye jukumu la kutoa haki kuwa ni Kiswahili badala ya Kiingereza kwa sababu Kiswahili ndiyo lugha ya Taifa, lugha ambayo inaeleweka na inatumika katika shughuli zote za kijamii na za maendeleo hapa nchini kwetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya yataimarisha mfumo wa upatikanaji haki kwa wananchi ambao sasa wanakusudiwa kuzitumia sheria husika. Serikali itafanyia kazi maoni na ushauri uliotolewa nanyi Waheshimiwa Wabunge kwa lengo la kuhakikisha utekelezaji wake unawanufaisha wananchi wote hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu pia, moja ya agenda iliyochukua nafasi kubwa ni hoja ya Serikali ya kujadili hotuba ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hoja hiyo tuliihitimisha vizuri na kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa iliyoko mbele yetu ni kutekeleza yale tuliyoyakusudia kama wajibu wetu. Hivyo basi, nitumie tena nafasi hii kuliahidi Bunge lako Tukufu kwamba michango ya Waheshimiwa Wabunge na maoni yao yatazingatiwa kwa utekelezaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Taifa wa Maendeleo. Katika mkutano huu wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kujadili kuhusu tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ulioanza mwaka

2016/2017 - 2020/2021; kujadili na kuidhinisha Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kutoka 2021/2022 - 2025/2026; pamoja na kutoa maoni na ushauri kuhusu Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, kipekee, naomba nimshukuru Mheshimiwa Dkt.Philip Isdor Mpango, Mbunge, Waziri wa Fedha na Mipango vilevile na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Mbunge, Waziri wa Katiba na Sheria kwa kuwasilisha vizuri Mpango mbele ya Bunge lako kwa pamoja na Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis, Mbunge, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, pamoja na Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa ufanuzi mzuri walioutoa wakati wa kuhitimisha hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe dokezo la Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali ya Mwaka unaoendelea sasa wa 2020/2021 ambapo ni Nusu ya Kwanza kuanzia mwezi Julai - Desemba, 2020.

Mheshimiwa Spika, mwezi Juni, 2020 Bunge lako Tukufu liliidhinisha shilingi trilioni 34.88 ikiwa ni bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021. Kiasi hicho kinajumuisha, shilingi trilioni 22.1 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi trilioni 12.78 kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2020, ridhaa ya matumizi iliyotolewa ilikuwa shilingi trilioni 13.12 sawa na asilimia 82.8 ya lengo. Kati ya kiasi kilichotolewa, shilingi trilioni 10.52 ni fedha za Matumizi ya Kawaida sawa na asilimia 95.2 na shilingi trilioni 2.6 ni fedha za maendeleo sawa na asilimia 54.2.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za maendeleo, kiasi cha shilingi bilioni 730.7 kutoka kwa washirika wa maendeleo zilipelekwa moja kwa moja kwenye utekelezaji wa miradi na hivyo kufanya utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kufikia asilimia 69.4. Kadhalika, kiasi cha shilingi

bilioni 254.6 kilitumika kulipa malimbikizo ya madai yaliyohakikiwa ya watumishi wa umma, wakandarasi na watoa huduma.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la mfumuko wa bei. Mfumuko wa bei nchini umeendelea kuwa tulivu na kubakia katika viwango vya chini. Kwa mfano, mfumuko wa bei kwa mwezi Desemba 2020 ulikuwa asilimia 3.2 ikilinganishwa na asilimia 3.8 ya mwezi Desemba 2019. Kwa hiyo, katika kipindi cha nusu mwaka ya mwaka 2020/2021, mfumuko wa bei ulikuwa wa wastani wa asilimia 3.2, ndani ya lengo la muda kati ya asilimia 5. Kiwango hicho cha mfumuko wa bei kilitokana na upatikanaji wa chakula cha kutosha katika masoko ya ndani na nchi jirani, bei ndogo ya mafuta kwenye soko la dunia, utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani na sarafu nyingine duniani, na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wakati wa Mkutano huu, Bunge lako Tukufu lilipokea na kujadili mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2021/2022 pamoja na Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, wakati tukiendelea na maandalizi ya utekelezaji wa mipango hiyo kwa kipindi cha mwaka 2021/2022, nami nitumie nafasi hii kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wananchi wote baadhi ya mambo makubwa na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha wa 2020/2021 kuanzia Juni mpaka Desemba 2020.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miezi sita ya kwanza ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021, yaani Julai hadi Desemba 2020, yapo mafanikio mengi yaliyopatikana. Kadhalika, zipo changamoto zilizoibuka na kuifanya Serikali kuja na mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo katika kipindi cha miezi

sita ya pili ya mwaka ili kufikia malengo yaliyowekwa kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, niruhusu japo kwa uchache nieleze baadhi ya mafanikio machache yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2020/2021. Aidha, baadhi ya mafanikio ni muendelezo wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mafanikio hayo ni pamoja na Serikali kugharamia kwa mara ya kwanza Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 kwa kutumia fedha za ndani ambapo shilingi bilioni 268.5 zilitumika. Serikali pia ililipa shilingi bilioni 254.6 madeni yaliyohakikiwa ya wazabuni na watumishi; shilingi trilioni 3.64 mishahara ya watumishi; shilingi bilioni 124.8 kwa ajili ya kugharamia sera ya elimumsingi bila ada na shilingi bilioni 105.1 kwa ajili ya kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na uimarishaji wa vyuo vya ufundi stadi na kukuza ujuzi kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kuendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati kama ifuatavyo: -

i. Ujenzi wa Reli ya Kati Kwa Kiwango cha Kimataifa (*Standard Gauge Railway*) ambapo ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (kilometra 300) umefikia asilimia 90 na kipande cha Morogoro – Makutupora (kilometra 422) umefikia asilimia 49.2. Aidha, tayari Serikali imesaini mkataba wa ujenzi wa kipande cha Mwanza - Isaka (kilometra 341) wenye thamani ya shilingi trilioni 3.07; na kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa vipande vya Makutupora – Tabora (kilometra 294) na Tabora – Isaka (kilometra 133). Shilingi bilioni 274.1 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/2021. Baada ya kukamilika matengenezo hayo, tutaanza kuunganisha vipande vya Tabora - Kigoma na Tabora – Mpanda. (*Makofii*)

ii. Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (megawati 2,115): Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 25.8

ambapo shilingi bilioni 128.9 zimetumika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/2021.

iii. Kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania: Serikali imekamilisha malipo ya mwisho ya ununuzi wa ndege aina ya Bombadier Dash 8-Q400 na Boeing 787-8 Dreamliner na malipo ya awali ya ununuzi wa ndege tatu, ambapo ndege mbili ni aina ya Airbus A220-300 na moja ni Dash 8-Q400 De-Havilland na hivyo kuwezesha Serikali kuwa na ndege mpya 11 kutoka ndege moja iliyokuwepo mwaka 2015 na kuifanya ATCL kuwa na jumla ya ndege 12 ambapo ndege tatu zinatarajiwa kuwasili wakati wowote katika mwaka huu wa fedha ili ziweze kutoa huduma. Shilingi bilioni 2.8 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/2021.

iv. Mradi wa nne ni mradi wa viwanja vya ndege na rada; kukamilika kwa jengo la tatu la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (*JNIA*) chenye uwezo wa kuhudumia abiria milioni sita kwa mwaka; kuendelea na ujenzi wa viwanja vya Geita (asilimia 86), Songea (asilimia 91) na Mtwara (asilimia 49.0); kukamilika kwa maandalizi ya mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato ambao utagharimu dola za Marekani milioni 330, sawa na shilingi bilioni 759; uzinduzi wa ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Shinyanga, Kigoma, Tabora na Sumbawanga vinavyogharimu *Euro* milioni 50 sawa na shilingi bilioni 136.85; kuanza kwa ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege Musoma; kukamilika kwa ukarabati wa karakana ya matengenezo ya ndege na kununuliwa kwa magari mapya matatu ya zimamoto yenye uwezo wa kubeba lita za maji 10,000 katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (*KIA*); kupanuliwa kwa barabara ya kuruka na kutua ndege katika kiwanja cha ndege cha Dodoma; kufungwa kwa mifumo ya kuongoza ndege (*AGL*) katika viwanja vya ndege vya Dodoma, Tabora na Mwanza; lakini pia kupanuliwa na kukarabatiwa kwa viwanja vya ndege vya Bukoba, Mwanza, Arusha, Nachingwea na Iringa. Shilingi bilioni 4.5 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/2021.

v. Mradi wa tano ni mradi wa usambazaji wa umeme vijiji na kuitia mradi kabambe wa kusambaza umeme vijiji na makao makuu ya wilaya (*REA - III*). Hadi Desemba 2020, jumla ya vijiji 10,018 kati ya vijiji 12,317 sawa na asilimia 81.3 vilikuwa vimeunganishiwa umeme ambapo katika kipindi cha nusu ya kwanza ya 2020/2021 shilingi bilioni 171.9 zimetolewa na kazi hiyo ya kukamilisha vijiji vilivyobaki inaendelea;

vi. Mradi wa sita ni mradi wa kuboresha usafiri wa abiria na mizigo katika Maziwa Makuu; Ziwa Victoria; kukamilika kwa ukarabati wa meli mbili za New Butiama Hapa Kazi Tu na New Victoria Hapa Kazi Tu; kuendelea na ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza Hapa kazi Tu yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo; kukamilika kwa ujenzi wa chelezo cha kujengea na kukarabati meli katika Bandari ya Mwanza; kupatikana kwa mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa meli za MV Umoja na MV Serengeti; kukamilika ukarabati wa meli za MV Clarias na ML Wimbi kazi hiyo imekamika na meli zinaanza kufanya kazi na nyingine zinatengenezwa

Ziwa Tanganyika; kukamilika kwa mikataba kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 600 na tani 400 pamoja na ukarabati wa meli ya MV Liemba; na ukarabati wa meli ya MT Sangara kwenye Ziwa Tanganyika ambapo katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/2021 shilingi bilioni 12.8 zimetumika. Tumeboresha bandari za Kibirizi, Sibwesa, Kagunga, Kabwe, Kasanya na sasa tunajenga bandari Kalema ambapo shilingi bilioni 86.4 zimetumika;

Shughuli nyingine zilizokamilika ni ujenzi wa magati ya Lushamba, Ntama, Nyamirembe, Magarine na Gati la majahazi Mwigobero; ununuzi wa vifaa vya kuhudumia mizigo na meli; ukarabati wa majengo na ofisi za bandari za Ziwa Victoria; kuboresha eneo la kushukia abiria *Mwanza North* na ukarabati wa *link span* ya bandari ya *Mwanza South*.

Ziwa Nyasa; kukamilika kwa ujenzi wa matishari mawili yenye uwezo wa kubeba tani 1000 kila moja; na ujenzi wa meli moja mpya ya MV Mbeya II yenye uwezo wa kubeba

abiria 200 na mizigo tani 200 umekamilika na imeanza kufanya kazi. Shilingi bilioni 1.5 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/2021. (*Makof*)

vii. Ujenzi wa barabara na madaraja makubwa; kujengwa kwa mtandao wa barabara kwa kiwango cha lami wenye urefu wa kilometa 3,537 (barabara kuu na za mikoa kilometa 2,208.62 na barabara za halmashauri kilometa 1,328) na hivyo kufanya mtandao wa barabara uliojengwa kwa kiwango cha lami hadi mwaka 2019/2020 kufikia kilometa 13,044 ambapo kilometa 10,939 ni barabara kuu na kilometa 2,105 ni barabara za mikoa. Ujenzi huu umeongeza uwiano wa mtandao wa barabara za lami nchini kutoka asilimia 6.8 mwaka 2015/2016 hadi asilimia 8.9 mwaka 2019/2020.

viii. Uendelezaji wa Mji wa Serikali Mtumba - Dodoma; Serikali imeanza maandalizi ya awamu ya pili ya ujenzi wa majengo ya ofisi katika Mji wa Serikali Mtumba yatakayotosheleza watumishi wote. Katika mwaka 2019/2020, Serikali imekamilisha usanifu wa majengo husika. Aidha, mradi wa ujenzi wa barabara (kilometa 51.2) kwa kiwango cha lami katika Mji wa Serikali utakaogharimu jumla ya shilingi bilioni 89.13 unaendelea, ambapo malipo ya awali ya shilingi bilioni 13.21 yamefanyika na ujenzi umefikia asilimia 56. (*Makof*)

ix. Miradi ya vivuko; kukamilisha ujenzi wa vivuko vipyta vya Kigongo - Busisi (Mwanza), Bugolora – Ukara (Mwanza) na Kayenze – Bezi (Mwanza). Aidha, ujenzi wa kivuko kipyta cha Nyamisati – Mafia (Pwani) na Chato – Nkome (Geita) umekamilika. Vilevile, ujenzi wa boti mpya tano za uokozi kwa ajili ya kisiwa cha Ukerewe (Ilugwa, Nafuba na Gana), kivuko cha Magogoni – Kigamboni na Lindi – Kitunda unaendelea. Pia, ukarabati mkubwa wa MV Kigamboni umekamilika na ukarabati wa kivuko MV Sengerema umefikia asilimia 90.

x. Mifugo; kujenga kiwanda kipyta cha *Kilimanjaro International Leather Industries Company Ltd.* chenye uwezo wa kuzalisha jozi na soli za viatu 1,200,000 kwa mwaka na kuchakata ngozi futi za mraba 13,000,000 kwa mwaka; kuimarisha kituo cha Taifa cha Uhimilishaji cha *NAIC* kilichopo

USA River, Arusha kwa kununua kifaa (*chiller*) kwa ajili ya mtambo wa kuzalisha kimiminika cha naitrojeni; kujengwa kwa viwanda vipyta vya kimkakati vya nyama vya *Tanchoice* (Pwani), *Elia Food Oversees Limited* (Arusha) na *Binjiang Company Limited* (Shinyanga); kujengwa kwa kiwanda cha maziwa cha *Galaxy Food and Beverage Company Limited* (Arusha); kujengwa kwa kiwanda cha kuzalisha chanjo cha *Hester Bioscience Africa Limited* (Pwani) chenye uwezo wa kuzalisha chanjo aina 37; na kuendelea kuboresha huduma za malisho ya mifugo na majosho. (*Makof*)

xi. Sekta ya uvuvi; kuongezeka kwa uzalishaji/uvunaji wa samaki katika maji ya asili kutoka tani 362,645 zenyе thamani ya shilingi trilioni 1.48 mwaka 2015/2016 hadi tani 497,567 za samaki zenyе thamani ya shilingi trilioni 2.34 mwaka 2019/2020; kuongezeka kwa usindikaji wa minofu ya samaki aina ya sangara kutoka tani 23,000.58 mwaka 2015/2016 hadi tani 27,596.27 mwaka 2019/2020; kuongezeka kwa huduma za usafirishaji wa mazao ya uvuvi kwenda masoko ya Ulaya ambapo katika mwaka 2019/2020, jumla ya kilo 777,750 za mabondo zilisafirishwa; kuongezeka kwa mauzo ya samaki na mazao ya uvuvi nje ya nchi kutoka mauzo yenye thamani ya shilingi bilioni 379.25 mwaka 2015/2016 hadi shilingi bilioni 506.24 mwaka 2019/2020; na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa bandari ya uvuvi (Mbegani) katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/2021 shilingi milioni 606.7 zimetumika.

xii. Miradi ya maji; kukamilika kwa miradi 1,423 ya maji iliyotekeliza mijini na vijijini. Baadhi ya miradi iliyotekeliza na hatua zilizofikiwa ni kukamilika kwa miradi ya maji katika miji ya Geita, Njombe na Songwe na kuendelea kwa ujenzi wa mradi wa maji katika mji wa Kigoma umefikia asilimia 90; utekelezaji wa mradi mkubwa wa Maji wa Ziwa Victoria kwenda katika miji ya Isaka, Tinde, Kagongwa, Tabora, Igunga, Uyui na Nzega umefikia asilimia 98; kukamilika kwa asilimia 76 ya ujenzi wa mradi wa maji katika Jiji la Mwanza; kukamilika kwa asilimia 62 ya ujenzi wa mradi wa maji katika Jiji la Arusha; na kuendelea na ujenzi wa mradi wa maji wa Same – Mwanga – Korogwe ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 65.

Aidha, katika eneo linalohudumiwa na DAWASA (mikoa ya Dar es Salaam na Pwani) utekelezaji wa miradi umekamilika kwa zaidi ya asilimia 90 na umehusisha maeneo ya Kibamba hadi Kisarawe, Mlandizi hadi Chalinze, Kisarawe - Pugu - Ukonga, Mkuranga - Vikindu, Jet - Buza, Kisarawe, Kigamboni, Mkuranga, Chalinze, Mbezi Luis hadi Kiluvya, Tegeta, Wazo, Madale, Mivumoni, Mabwepande na Bagamoyo katika maeneo ya Vikawe, Zinga, Mapinga na Kerege. (*Makofi*)

Kwa ujumla miradi yote iliyotekelizwa imewezesha wananchi zaidi ya milioni 25 kupata huduma ya maji ambapo wastani wa idadi ya watu wanaopata huduma ya maji safi na salama imeongezeka kutoka asilimia 74 mwaka 2015 hadi asilimia 84 mwaka 2020 kwa mijini na kutoka asilimia 47 mwaka 2015 hadi asilimia 70.1 mwaka 2020 kwa vijijiini. Aidha, kwa Jiji la Dar es Salaam upatikanaji wa maji safi umeongezeka kutoka asilimia 72 mwaka 2015 hadi asilimia 90 Desemba, 2020. Shilingi bilioni 226.7 zimetumika katika nusu ya kwanza ya 2020/2021. Kazi ya usambazaji maji vijijiini inaendelea kwa kasi. (*Makofi*)

xiii. Sekta ya afya; Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya sekta ya afya ambayo imefikia hatua mbalimbali ikiwemo asilimia 98 ya ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa Mwananyamala; Ujenzi wa jengo la maabara katika Hospitali ya Rufaa kule Njombe umefikia asilimia 73; ujenzi wa jengo la mama na mtoto, upasuaji, radiolojia na maabara katika Hospitali ya Rufaa Simiyu umefikia asilimia 50. Shilingi bilioni 64.6 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/2021 kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya afya, ununuzi wa vifaa, vitendanishi, dawa na chanjo.

xiv. Miradi ya kimkakati ya kuongeza mapato katika Halmashauri; katika kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaongeza mapato kwa kutumia fursa zilizopo katika maeneo yao, Serikali ilitoa shilingi bilioni 91.4 kwa ajili ya kugharamia miradi 26. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 50.6 zilitolewa mwaka 2019/2020. Miradi ya ujenzi iliyotekelizwa

ni pamoja na; stendi za mabasi tisa, machinjio mbili, viwanda vidogo vitatu, maegesho ya malori mawili, masoko tisa na ghalia la mazao moja. Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya 2020/2021, Serikali imetoea shilingi bilioni 19.9 kwa ajili ya kugharamia miradi ya kimkakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, licha ya mafanikio hayo makubwa ambayo nimejaribu kueleza kwa uchache, vilevile katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali kwa nusu ya kwanza ya mwaka 2020/2021, zipo changamoto kadhaa zilizojitokeza. Changamoto hizo ni pamoja na uharibifu wa miundombinu ya barabara uliosababishwa na mafuriko, kupungua kwa shughuli za kibiaashara duniani kutokana na athari za mlipuko wa homa kali ya mapafu, kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi na ukwepajji kodi kwa baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu, hususan kuitia biashara za magendo, kutokutoa na kudai stakabadhi za klelektroniki wakati mauzo yanapofanyika na kasi ndogo ya ukusanyaji wa kodi ya majengo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari hadi Juni 2021, Serikali itaendelea kuchukua hatua na kutekeleza mikakati mbalimbali kwa lengo la kuongeza mapato na kuimarisha usimamizi wa matumizi ili kufikia malengo kwa kipindi kilichobaki cha mwaka 2020/2021. Mionganoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na kuendelea kuchukua hatua za tahadhari dhidi ya majanga na kufanya ukarabati wa miundombinu iliyoharibiwa na mafuriko na kuimarisha ukaguzi wake.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika, Serikali itaendelea kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima; kuhakikisha nakisi ya bajeti haizidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa na hivyo, kuendana na makubaliano ya Jumuia ya Afrika Mashariki, lakini kuelekeza fedha kwenye maeneo ya kipaumbele yatakayochochea ukuaji wa uchumi, kuhakikisha miradi inayoendelea inapewa kipaumbele kabla ya miradi mipyaa; kudhibiti ulimbikizaji wa madai; na kuongeza kasi ya matumizi ya TEHAMA katika miamala na shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, Serikali itatekeleza mikakati mahususi ya kuongeza mapato kwa kufanya yafuatayo:-

Mosi, kuimarisha mifumo ya usimamizi kwa kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wote wanatumia mashine za kutolea risiti za kielektroniki (*EFD*).

Pili; kuimarisha ushirikiano kati ya mamlaka zinazokusanya mapato ya Serikali na vyombo vyta ulinzi na usalama katika kufanya doria maeneo ya mipaka ya nchi kavu, baharini na kwenye maziwa ili kudhibiti biashara za magendo.

Tatu, kukasimisha jukumu la kukusanya kodi ya majengo kwa Halmashauri na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa kuibua hoja ambazo zilifanya mjadala wetu humu Bungeni kuwa wa kina na wenye kutoa msisimko wa kiwango cha juu. Yote hayo, yalitokana na ukweli kwamba Waheshimiwa Wabunge waliibua hoja na kuchangia kwa umakini mkubwa kwa lengo kujenga na kusaidia taifa letu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine kuititia hoja na michango yao, Waheshimiwa Wabunge wamegusia masuala muhimu ikiwemo elimu, kilimo, uwezeshaji, uwekezaji, viwanda na miundombinu ambayo yamekuwa kitovu cha mjadala na michango ya Waheshimiwa Wabunge. Kwa msingi huo, naomba nitumie fursa hii adhimu kutolea ufanuzi baadhi ya masuala muhimu yaliyoibiliwa na Waheshimiwa Wabunge kwenye mjadala wetu.

Mheshimiwa Spika, kwenye sekta ya elimu; kuititia Mkutano huu wa Pili wa Bunge lako tukufu, Waheshimiwa Wabunge wameibua hoja nyingi kuhusu changamoto ya miundombinu ya shule hususan sekondari, suala la ujuzi na mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Nyingi ya changamoto hizi zinatokana na utekelezaji mzuri wa sera ya

elimu bure bila malipo sambamba na ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya shule na vyuo ambao umechangia kuongezeka kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza na hata darasa la kwanza kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa samani na miundombinu, Serikali imeweka mikakati mbalimbali ikiwemo ya muda mfupi na muda mrefu. Lengo la Serikali ni kuhakikisha wanafunzi wote waliofaulu mtihani wa darasa la saba wanajiunga na kidato cha kwanza bila kujali ni chaguo la kwanza au la pili na kuhakikisha miundombinu yote na samani zote kwa ajili ya kuwapokea wanafunzi hawa inakamilika ifikapo tarehe 28 Februari, 2021.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Dunia iliidhinisha mkopo wa kiasi cha dola za Marekani millioni 500 sawa na takriban shilingi za Tanzania trillioni 1.2 kwa ajili ya mradi wa maboresho ya elimu ya sekondari yaani (*Secondary Education Quality Improvement Programme - SEQUIP*). Mradi huo, uliidhinishwa mwaka jana licha ya kelele nyingi kutoka kwa watu wasiokuwa na uzalendo na nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mradi huo, utakaotekelezwa kwa muda wa miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021 - 2025/2026 utakuwa ni mwarobaini kwa changamoto ya miundombinu ya shule za sekondari kwani shule mpya 1,026 zitajengwa kote nchini. Kati ya shule hizo, shule mpya 26 zitakuwa za bweni zenye uwezo wa kupokea wanafunzi kati ya 1,000 hadi 1,500 kwa kila mkoa na zitajengwa kwa awamu tatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kadhalika shule mpya 1,000 za kutwa zitajengwa zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 400 kwa kila shule. Shule hizo zitajengwa kwenye kata 718 zisizo na sekondari za kata na kwenye maeneo yaliyoelemewa na idadi kubwa ya wanafunzi. Hivyo basi, nitumie nafasi hii kuwaelekeza viongozi na watendaji wa Serikali za Mitaa wasimamie kikamilifu utekelezaji wa mradi huu ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka huu 2020/2021 Serikali imetoa mikopo kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza 55,287 ambapo wanafunzi 28,041 sawa na asilimia tano wamehitimu elimu ya sekondari katika shule mbalimbali za binafsi. Serikali itaendelea kuzingatia kigezo pekee cha uhitaji wa mwombaji sanjari na kurahisisha matumizi ya mtandao katika uombaji na utoaji wa mikopo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza ufanisi wa utoaji na urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu, Serikali imefanya maboresho ya kisheria, kimfumo na kiutendaji kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita kutoka mwaka 2015/2016 – 2019/2020. Matunda ya maboresho hayo ni pamoja na kuongezeka kwa makusanyo kutoka wastani wa shilingi bilioni 28.9 mwaka 2016/2017 hadi kufikia wastani wa shilingi bilioni 192 mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafarijika na inapokea kwa mikono miwili michango yenye afya na tija kuhusu hatma ya mikopo inayotolewa na Serikali baada ya miaka 15 ya uwepo wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, nilihakikishie Bunge lako tukufu kwamba Serikali kwa upande wake ipo tayari kuendelea kujifunza kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote nchini kuhusu namna bora zaidi ya kuufanya mfuko huu uwe endelevu na wenye manufaa katika ujenzi wa uchumi wa nchi yetu. (*Makofii*)

Hivyo basi, katika kuufanya mfuko huo uwe endelevu na himilivu, nitumie fursa hii kuelekeza mambo yafuatayo:-

Moja, ninaitaka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ishirikiane na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ili kuboresha huduma zake na kurahisisha urejeshwaji wa mikopo kwa wanufaika waliojiari katika sekta binafsi, ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu haki na wajibu wa mnufaika na mwajiri. (*Makofii*)

Pili, ninawasihi wanufaika wote wa mikopo ya elimu ya juu, ambao bado hawajajitokeza na kuanza kurejesha, wafanye hivyo mara moja.

Mwisho, ninawataka waajiri wote nchini katika sekta binafsi na sekta ya umma watoe kipaumbele kwa makato ya mikopo ya elimu ya juu kama ilivyo kwenye makato mengine ya kisheria ili kuwezesha kuongeza idadi ya wanufaika kwa kipindi kinachokuja.

Mheshimiwa Spika, ukuzaji ujuzi ni mionganoni mwa hoja iliyoungwa mkono na Wabunge wengi wakati wa kuchangia hoja mbalimbali hususan ya elimu wakati wa mukutano huu. Hivyo, na mimi nitumie nafasi hii kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Januari, 2021 vijana 10,178 wamepatiwa mafunzo na kutathminiwa ujuzi wallioupata nje ya mfumo rasmi wa mafunzo nchi nzima ambapo vijana 9,736 wamefaulu na kupatiwa vyeti na Mamlaka ya Mafunzo na Ufundu Stadi (*VETA*).

Mheshimiwa Spika, vyeti hivyo vinawawezesha kutambulika, kuijiendeleza kiujuzi, kujiajiri pamoja na kupata kazi katika taasisi na kampuni mbalimbali. Vijana hao ni wenye ujuzi katika fani za uashi, useremala, ushonaji, ufundu bomba, uchomeleaji na uungaji vyuma, ufundu magari, ufundu umeme, ukarabati wa bodi za magari, upishi na uhudumu katika hoteli. Aidha, vijana 36 wamegharamiwa na Serikali kwa ajili ya kuhudhuria mafunzo ya kilimo cha kisasa nchini Israel.

Mheshimiwa Spika, katika nusu ya pili ya mwaka 2020/2021 vijana wapatao 4,616 watapatiwa mafunzo na kurasimishwa ujuzi walionao kupitia mfumo huu. Aidha, mwezi Januari 2021, vijana 1,203 wa vyuo vya elimu ya juu na kati wamehitimu mafunzo ya uzoefu wa kazi kupitia kampuni mbalimbali kulingana na fani walizosomea; na wahitimu 2,037 wamewezeshwa na wanaendelea kupata mafunzo ya uzoefu wa kazi katika taasisi binafsi na za umma ambayo yatachukua muda wa kipindi cha mwaka mmoja. (*Makofii*)

Vilevile wahitimu 2,421 wanaandaliwa kwa ajili ya kuanza mafunzo mwezi Machi, 2021 katika fani za ushonaji nguo, useremala, uashi, uchorongaji vipuri, ufundi magari, umeme, bomba, terazo, upishi na utoaji huduma za mahotelii, utengenezaji wa simu, majokofu, viyoyozi, upakaji rangi, uandishi wa alama, utengenezaji wa umeme wa magari, utengenezaji wa nywele na utanashati, uchoraji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limechangiwa sana ni la barabara; kumejitokeza mjadala mkubwa unaohitaji uboreshaji miundombinu ya barabara za mijini na hasa za vijijini. Vyombo vyetu vya *TANROADS* na *TARURA* vimefanyia kazi na sasa tunakusudia kuongeza uwezo wa vyombo hivyo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tumepokea ushauri wenu na tutaufanyia kazi ili tuweze kufanya maboresho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo; hali ya kilimo katika msimu huu wa kilimo; katika msimu wa mvua wa mwaka 2020/2021 mvua za vuli zilizoanza mapema mwezi Septemba zimeendelea kunyesha kwa kiwango cha juu ya wastani katika maeneo mengi hasa ya Kanda ya Ziwa Victoria. Katika maeneo mengine ya Pwani ya Kaskazini na Kanda ya Kaskazini Mashariki, mvua zilichelewa kuanza (Novemba) na zimeendelea kunyesha hadi katika mwezi Januari, 2021.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Januari, mwenendo wa unyeshaji wa mvua hizo umeendelea kwa kiwango cha juu ya wastani katika maeneo mengi. Mwelekeo unaonesha kuwa mvua hizi zitachangia upatikanaji wa chakula katika kipindi cha mwezi Februari na kuendelea kabla ya mavuno mengine kuanzia mwezi Mei, 2021. Vilevile hali ya malisho ya mifugo na upatikanaji wa maji umeendelea kuwa mzuri katika maeneo yote nchini.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha kilimo cha umwagiliaji ni moja ya ajenda; katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020 Serikali imefanikiwa kujenga na kukarabati skimu za umwagiliaji 179 ambazo zimeongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 461,000 mwaka 2015 hadi hekta 694,715 mwaka

2020 sawa na ongezeko la asilimia 50.7. Hii ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2018 yaani *Revised National Irrigation Master Plan - RNIMP 2018* ambao umeainisha hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imekamilisha ujenzi wa maghala 14 ya kuhifadhia mavuno katika skimu za umwagiliaji za Ngana na Makwale (Kyela), Magozi na Tungamalenga (Iringa), Mbuyuni-Kimani, Ipatagwa, Kongolo-Mswisi na Motombaya (Mbarali), Lekitatatu (Arusha), Mombo (Tanga), Uturo (Mbeya), Bagamoyo (Pwani), Mkindo na Mkula (Morogoro).

Mheshimiwa Spika, katika hatua ya kuongeza mnyororo wa thamani kwenye uzalishaji wa mazao ya kilimo, kati ya maghala hayo, maghala sita yamewekewa na vinu vyatukio vya kukobolea mpunga.

Mheshimiwa Spika, nimeamua kusema haya ili Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujuma wafahamu kwamba tunatambua umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji na tunachukua hatua kadhaa kuhakikisha kuwa kilimo hiki kinapata manufaa kwa wanaoshiriki kilimo.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa pembejeo za kilimo na uzalishaji wa mbegu; Serikali imeweka mikakati ya kuhakikisha pembejeo zinawafikia wakulima kwa wakati ambayo ni pamoa na kupata mahitaji halisi ya pembejeo za kilimo kutoka kila mkoa kabla ya msimu wa kilimo kuanza na kuwasiliana na makampuni ya pembejeo na kuyahimiza kusambaza pembejeo hizo mapema kulingana na mahitaji ya kila mkoa.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali inaboresha mifumo ya uzalishaji, uagizaji na uthibiti wa mbegu bora na viuatilifu hapa nchini ikiwemo kuimarisha uzalishaji wa pembejeo hizo ndani ya nchi ili kukidhi mahitaji na upatikanaji wake kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, katika kufikia malengo, Serikali itaongeza eneo la ASA la uzalishaji wa mbegu kutoka hekta 4,925 (2019/2020) hadi hekta 6,923 ifikapo 2025 na eneo la TAR/kutoka hekta 1,033.2 hadi hekta 3,663.24 ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, huduma za ugani ni maeneo ambayo yanaboreshwah; uzalishaji na tija katika kilimo, pamoja na mambo mengine huchangiwa na maarifa na ujuzi unaotolewa na Maafisa Ugani kwa wakulima. Kwa mantiki hiyo, Serikali inalenga kuhakikisha kuwa kila kijiji, mtaa na kata vinakuwa na Afisa Ugani angalau mmoja ili kuwawezesha wakulima kupata maarifa na ujuzi wa kuzalisha mazao kwa ufanisi na tija. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, idadi ya Maafisa Ugani waliopo nchini sasa ni 6,704 ikilinganishwa na mahitaji 20,538. Aidha, katika kukabiliana na changamoto ya uhaba wa Maafisa Ugani, Wizara inaendelea kusomesha Maafisa Ugani tarajali katika ngazi ya cheti na diploma ambapo kuanzia mwaka 2015 hadi 2020 jumla ya wataalamu wa kilimo 8,657 walihitimu katika vyuo vya mafunzo ya kilimo ngazi ya cheti na diploma.

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji wananchi kiuchumi; kama niliviotangulia kueleza, suala la uwezeshaji wananchi iwe kwenye sekta ya kilimo au ujasiriamali na biashara ndogo na za katni mionganoni mwa hoja zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge. Suala hilo pia limejitokeza waziwazi kwenye hotuba ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa tarehe 13 Novemba, 2020 wakati akifungua Bunge la Kumi Mbili.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hiyo, Mheshimiwa Rais alielekeza Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kuwa inaimarisha uratibu na usimamizi wa mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi ili Watanzania waifahamu ilipo, vigezo vya kutolea mikopo na aina ya mikopo iliyopo. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa wananchi wananaufaika na mikopo hiyo ili kuinua vipato vyao, kupunguza umaskini na tatizo la ajira.

Mheshimiwa Spika, licha ya changamoto zinazokabili mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi, katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2015 hadi 2020, mifuko na programu za uwezeshaji za Serikali zimefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani zaidi ya shilingi triliioni 2.22, kunufaisha zaidi ya watu milioni 4.9 na taasisi 5,499. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile kupitia mifuko ya uwezeshaji wa makundi maalumu ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu iliopo, Halmashauri 185 zimefanikiwa kutoa shilingi bilioni 93.3. Fedha hizo zimewezesha upatikanji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa vikundi 32,553 kote nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha malengo hayo yanafikiwa napenda kiliarifu Bunge lako tukufu kwamba tumeanza kuchukua hatua zenyе kulenga kuboresha huduma za mifuko na programu ya uwezeshaji. Tarehe 17 Novemba, 2020 tulianza zoezi la tathmini ya utendaji wa programu na mifuko takribani 20. Aidha, tayari taarifa ya awali kutoka ngazi ya wataalamu imekamilika na kuwasilishwa kwenye mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, tarehe 9 Februari 2021 nilifungua wiki ya maonesho ya nne ya mifuko na programu za uwezeshaji kwa Kanda ya Kaskazini yaliyofanyika kwenye viwanja vya Sheikh Amri Abeid, kule Jijini Arusha. Ni matumaini yangu kwamba kupitia maonesho hayo wananchi wa mkoa wa Arusha, mikoa ya Kanda ya Kaskazini pamoja na wananchi kutoka sehemu mbalimbali nchini watapata uelewa mpana kuhusu shughuli za mifuko na programu za uwezeshaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wakati tukiendelea na mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge walieleza kwa kina kuhusu changamoto mbalimbali zinazowakabili wakulima na wafanyabiashara wetu hususan wadogo katika shughuli zao za kiuchumi na kujiongezea kipato hususan masuala ya uzalishaji, masoko, ufungashaji bora wa bidhaa, huduma za fedha, elimu ya ujasiriamali, teknolojia na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba mchango wa sekta ya fedha hususan mabenki na mifuko ya hifadhi za jamii kwenye kilimo bado ni mdogo kwani hadi sasa upo kwenye asilimia 8.5 sawa na shilingi triliioni 1.65. Kwa msingi huo Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na mabenki na mifuko ya hifadhi ya jamii kuona namna ambayo watachangia katika shughuli za kilimo na mnyororo mzima wa thamani.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na kuthamini sana mchango mkubwa unaotolewa na wafanyabiashara wadogo (wamachinga) katika kukuza uchumi, kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja, kuondoa umaskini na kuleta maendeleo endelevu nchini. Sekta hii ya wafanyabiashara wadogo nchini inakadirwa kuwa na wajasiriamali wapatao milioni 3.1 ambaو wameajiriwa sawa na takribani asilimia 23.4 ya nguvu kazi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wadau wa sekta hii wanaendesa shughuli zao bila kubughudhiwa, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliamua kugawa vitambulisho vya wajasiriamali wadogo. Hata hivyo, licha ya mafanikio makubwa ya vitambulisho hivyo, vimeonesha kuwa na changamoto mbalimbali ambazo zinahitaji maboresho hususan katika kuwasadia kupata mikopo na mitaji kutoka kwenye taasisi za fedha ili waweze kuendesa shughuli mbalimbali za ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, katika kuwasadia wajasiriamali hawa wadogo kupata mitaji kwa urahisi kupitia taasisi za fedha, Serikali imeanza taratibu za kuboresha vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo kwa mwaka 2021. Vitambulisho hivyo vitakuwa vya kielektroniki na vitaboreshwu zaidi hatua kwa hatua ili viwawezeshe wafanyabiashara wadogo kukopa kutoka taasisi za fedha ikiwemo programu na mifuko ya uwezeshaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 28 Januari, 2021 nilipata fursa ya kufungua Kongamano la Wafanyabiashara Wadogo, maarufu wamachinga lililofanyika Jijini Dar es Salaam. Lengo

la kongamano lile pamoja na mambo mengine lilikuwa ni kuwashirikisha wadau hao kuhusu namna nzuri zaidi ya kuboresha vitambulisho vya wafanyabiahara wadogo (wamachinga) ili waweze kuvitumia kupata mitaji au mikopo kutoka kwenye mabenki na taasisi za fedha ikiwemo na mifuko.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwapongeza wafanyabiashara wadogo (wamachinga) kwa kutekeleza vyema jukumu la usambazaji wa bidhaa nchini kwa bei nzuri wanazozimudu wananchi hasa wale wa kipato cha chini. Aidha, nitoe rai kwa machinga wote kuepuka kushirikiana na wafanyabiashara wakubwa wanaowatumia kukwepa kodi, kwa kuwapa bidhaa nyingi bila kutoa risiti za kielektroniki zenye kiwango halisi cha bei ya kununulika bidhaa hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wakati tunaendelea na zoezi la kuboresha vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo, naagiza viongozi na watendaji wa Serikali za Mitaa washirikiane na viongozi wa wafanyabiashara wadogo (wamachinga) kwenye maeneo yao ili kupata orodha yao na kuwaandalia maeneo mazuri ya kufanya biashara zao.

Mheshimiwa Spika, sekta ya michezo; katika kipindi cha hivi karibuni nchi yetu imepata mafanikio mbalimbali hususan katika mpira wa miguu. Nitumie nafasi hii kutoa pongezi zangu kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kwa mafanikio makubwa yanayojiteza kwa upande wa soka na michezo mingine kama ngumi hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mathalani, katika kipindi hiki tumeshuhudia Tanzania ikishiriki fainali za mashindano ya Afrika ya Mpira wa Miguu kwa wachezaji wanaocheza ligi ya ndani (*CHAN*) ambayo yamekamilika hivi karibuni huko Cameroon. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nizipongeze pia timu za Taifa za umri wa chini ya miaka 20 na 17 ambazo zimefuzu kushiriki katika mashindano ya Fainali za Bara la Afrika kwa mwaka 2021. Timu hizi zitakwenda kushiriki katika fainali za michuano hiyo katika nchi za Morocco kwa U-17 na Mauritania kwa timu ya U-20. Vilevile naipongeza timu ya wanawake U-17 kushinda kombe la COSAFA kwa mashindano yaliyofanyika Afrika Kusini, Novemba 2020. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakuongeza dakika. (*Makofi/Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa soka la vilabu, naipongeza *Namungo FC* kwa kufanikiwa kuvuka hatua mbili za awali kuelekea kwenye makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika na pia niwatakie kila la heri kwenye mchezo wao utakaochezwa kesho Jumapili huko nchini Angola. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ingawa timu hiyo mpaka sasa inashikiliwa na Jeshi la nchi ya Angola ikiwa ni siasa za kwenye michezo. Sisi kama Tanzania kuititia Wizara ya Mambo ya Nje inalifanyia kazi jambo hilo ili timu hiyo iweze kushiriki michezo na irudi nyumbani nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Mabingwa wa Soka Tanzania, timu ya *Simba Sports Club* kwa kufanikiwa kufuzu kuingia hatua ya makundi katika Mashindano ya Klabu Bingwa Afrika na jana kushinda mchezo wake wa kwanza katika hatua ya makundi wakiwa ugenini dhidi ya Klabu ya AS Vita huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. (*Makofi*)

Nitumie nafasi hii kumpongeza Mtendaji Mkuu wa timu hiyo, mwanadada Barbra Gonzalez kwa ubunifu na kushirikisha Wizara ya Maliasili na Utalii na hivyo kulipa heshima Taifa letu kwa kulitangaza Taifa hili kuititia jezi yao kwa

maneno *Visit Tanzania*. Huu ni uzalendo wa hali ya juu ambao unapaswa kupongezwa na kuigwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mchambuzi maarufu wa michezo nchini Bwana Ali Kamwe, kupitia ukurasa wake wa *Instagram* ameeleza vizuri maana ya matumizi ya neno hili *Visit Tanzania* na namna nchi yetu itakavyonufaika na ubunifu huo. Kwa mujibu wa maelezo yake neno *Visit Tanzania* linakadiriwa kutazamwa na wapenzi wa soka takribani milioni 500 kutoka sehemu mbalimbali duniani. (*Makofi*)

Wapenzi hao wa mpira kupitia vituo vya televisheni vya *Canal Algérie*, *BelN Sports*, *Eurosport*, *ESPN*, *Arryadia*, *GTV* ya Ghana, *MENA belN Sports* na *West Africa Canal+* wameshuhudia mchezo wa jana. Kwa lugha nyingine ni kwamba neno *Visit Tanzania* liliopo sehemu ya kifuani mwa jezi ya Klabu ya Simba litaonekana kupitia channel/hizo kwa kila dakika 90 ambazo Simba itashuka dimbani iwe dhidi ya Al-Ahly (Misri), El-Merreikh (Sudan) au dimba la nyumbani kwa Mkapa (Tanzania). Tutavuta watalii wengi kuifuatilia nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kung'ara pia kwenye medani ya masumbwi; kwa upande huo wa masumbwi, nawapongeza mabondia Mfaume Mfaume kwa kufanikiwa kutetea ubingwa wa *East and Central Africa* mwezi Desemba, 2020; Bondia Ibrahim Class Mgendera kwa kushinda Ubingwa wa *World Boxing Federation Intercontinental Lightweight (WBF)*. Vilevile nawapongeza Bondia Tonny Rashidi aliyesanikiwa kutetea mkanda wake wa *African Boxing Union (ABU)* na Bondia Shabani Hamadi Jongo aliyeshinda Ubingwa wa *WBF International Cruiserweight* mwishoni mwa Januari, 2021. Bila kuwasahau mabondia maarufu walioonesha uwezo mkubwa wa kina Hassan Mwakinyo kutoka Tanga, Twaha Kiduku pamoja na Dulla Mbabe ambaye atapanda ulingoni tarehe 26 Februari, 2021. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nihitimishe hotuba yangu sasa kwa kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yenu muhimu mliyoitoa kwa lengo la kuboresha

maisha ya wananchi wetu. Nimshukuru Katibu wa Bunge, wasaidizi wake na watumishi wote wa Bunge kwa huduma nzuri na msaada mkubwa ambao wamekuwa wakitupatia kwa kipindi chote tulichokuwa tukitekeleza majukumu yetu ya Mkutano wa Pili wa Bunge la Kumi na Mbili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia viongozi na watendaji wa Serikali na taasisi zake ambao wameendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi, umahiri na ufanisi mkubwa. Hongereni sana kwani juhudini zenu zimekuwa chachu ya kufanikisha shughuli zilizopangwa kwenye Mkutano huu wa Pili wa Bunge la Kumi na Mbili. Vilevile nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo sitowashukuru wanahabari kwa uchambuzi mzuri wa hoja na mwenendo mzima wa Bunge na kuwahabarisha wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile nivishukuru vyombo vyaa ulinzi na usalama kwa huduma ambazo wamekuwa wakizitoa kwa washiriki wa Bunge hili. Pia niwashukuru madereva wote waliotuhudumia wakati wote tukiwa hapa Bungeni na ninawataki heri katika safari ya kurejea majumbani kwetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu liahirishwe hadi tarehe 30 Machi, 2021 siku ya Jumanne, saa tatu kamili asubuhi katika ukumbi huu hapa Jijini Dodoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM M. MAJALIWA (MB.),
WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA,
WAKATI AKIAHIRISHA MKUTANO WA PILI WA BUNGE LA KUMI
NA MBILI TAREHE 13 FEBRUARI, 2021 - KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya

njema hadi leo hii tunapohitimisha shughuli zote zilizopangwa katika Mkutano huu wa Pili wa Bunge la Kumi na Mbili.

2. Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa naungana tena na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za pole kwa Bunge lako Tukufu na kwa familia za waliokuwa Wabunge, Mheshimiwa Martha Umbula Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara na Mheshimiwa Atashasta Nditiye, Mbunge wa Muhammadi walitangulia mbele za haki wakati wakiendelea kulitumikia Taifa. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azipumzishe roho zao kwa amani.

3. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwapa pole Watanzania wenzangu waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki na wengine kusababishiwa madhara mbalimbali kutokana na ajali za barabarani na matukio mengine. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atupe subra na awape nafuu majeruhi wetu wapone haraka.

4. Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana wewe binafsi, Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kusimamia kwa umahiri mkubwa majadiliano ya hoja kuhusu kujadili Hotuba ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitao tarehe 13 Novemba, 2020 wakati akifungua Bunge la Kumi na Mbili sambamba na Mpango wa Taifa wa Maendeleo.

5. Mheshimiwa Spika, ninawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge kwa pongezi zenu kwa Serikali na kwa michango yenu yenye dhamira ya dhati kabisa ya kuboresha mipango na kazi zilizokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika kipindi chote cha miaka mitano. Mjadala huu umeendelea kuthibitisha uimara wa Bunge katika kutekeleza wajibu wake wa Kikatiba wa kuishauri na kusimamia Serikali kikamilifu.

SHUGHULI ZA BUNGE Maswali na Majibu

6. Mheshimiwa Spika, wakati wa mkuu huu, Waheshimiwa Wabunge **164 na Mawaziri saba** walichangia hoja ya kujadili

Hotuba ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa tarehe 13 Novemba, 2020 wakati akifungua Bunge la Kumi na Mbili. Aidha, Waheshimiwa Wabunge **126** walichangia Mpango wa Taifa wa Maendeleo.

7. Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu jumla ya maswali **125** ya msingi na mengine **289** ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kupatiwa majibu na Serikali. Kadhalika, maswali **14** ya papo kwa papo yaliulizwa na kujibiwa na Waziri Mkuu.

Kamati za Kudumu za Bunge

8. Mheshimiwa Spika, natambua kuwa shughuli za utangulizi za Mkutano huu zilianza tarehe 18 hadi 31 Januari 2021 kwa vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge sambamba na Chaguzi za Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge. Hivyo, nitumie fursa hii kuwapongeza wajumbe wote kwa kufanikisha upatikanaji wa viongozi wa Kamati hizo ambao wameaminiwa na kuchaguliwa kuongoza Kamati zetu.

9. Mheshimiwa Spika, ni matarajio yangu kwamba tutatumia nafasi hizo vizuri katika kuleta ushirikiano, mshikamano na kufanya kazi pamoja kama wawakilishi wa wananchi na kutekeleza majukumu yetu kwa kuisimamia na kuishauri Serikali.

10. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa upande wake, itaendelea kutoa ushirikiano wa kutosha kwa kamati hizo ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuhakikisha tunaboresha utendaji kazi na uwajibikaji hususan wakati huu tunapoelekea kwenye maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2021/2022.

11. Mheshimiwa Spika, vilevile, nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Naibu Mawaziri kwa kujibu vizuri pamoja na kutoa ufanuzi wa kina kuhusu hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge.

Miswada ya Serikali

12. Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2021 uliowasilishwa na Serikali katika Mkutano huu.

Aidha, Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa Mwaka 2021 (*The Accountants and Auditors (Registration) (Amendment) Act, 2021*) pamoja na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2021 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Act, 2021*) ilisomwa kwa mara ya kwanza katika Mkutano huu.

13. Mheshimiwa Spika, niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri wakati wa kujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2021 ambao kwa msingi wake ulikusudia kufanya marekebisho katika Sheria ya Tafsiri ya Sheria (Sura ya 1), Sheria ya Mahakama za Mahakimu (Sura ya 11) na Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi (Sura ya 216). Lengo la marekebisho hayo ni kuweka msingi wa lugha ya Mahakama, Mabaraza na vyombo vingine vyenye jukumu la kutoa haki kuwa ni Kiswahili badala ya Kiingereza kwa sababu Kiswahili ndiyo lugha ya Taifa, lugha ambayo inaeleweka na inatumika katika shughuli zote za kijamii na za maendeleo nchini.

14. Mheshimiwa Spika, marekebisho haya yataimarisha mfumo wa upatikanaji haki kwa wananchi ambao wanakusudiwa kuzitumia sheria husika. Serikali itafanyia kazi maoni na ushauri uliotolewa nanyi Waheshimiwa Wabunge kwa lengo la kuhakikisha utekelezaji wake unawanufaisha wananchi wote hapa nchini.

Mjadala wa Hotuba ya Rais

15. Mheshimiwa Spika, katika mkutano huu moja ya agenda iliyochukua nafasi kubwa ni hoja ya Serikali ya kujadili hotuba ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hoja hiyo tuliihitimisha vizuri na kwa mafanikio makubwa.

16. Mheshimiwa Spika, kazi kubwa iliyoko mbele yetu ni kutekeleza yale tuliyokusudia kama wajibu wetu. Hivyo basi, nitumie tena nafasi hii kuliahidi Bunge lako tukufu kwamba michango ya Waheshimiwa Wabunge na maoni yao yatazingatiwa kwa utekelezaji.

Mpango wa Taifa wa Maendeleo

17. Mheshimiwa Spika, katika mukutano huu wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kujadili kuhusu tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017-2020/2021), kujadili na kuidhinisha Mapendekezo ya Mpango wa Tatoo wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022-2025/2026) pamoja na kutoa maoni na ushauri kuhusu Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

18. Mheshimiwa Spika, kipekee, naomba nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango (Mb.), Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb.), Waziri wa Katiba na Sheria kwa kuwasilisha vizuri Mpango mbele ya Bunge lako pamoja na Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis (Mb.) Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, pamoja na Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa ufanuzi mzuri walioutoa wakati wa kuhitimisha hoja hii.

UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI YA MWAKA 2020/2021 KATIKA NUSU YA KWANZA JULAI – DESEMBA 2020

19. Mheshimiwa Spika, Juni, 2020 Bunge lakotukufu liliidhinisha shilingi **triliioni 34.88** ikiwa ni bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021. Kiasi hicho kinajumuisha, shilingi **triliioni 22.10** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **triliioni 12.78** kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

20. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2020, ridhaa ya matumizi iliyotolewa ilikuwa shilingi **triliioni 13.12** sawa na **asilimia 82.8** ya lengo. Kati ya kiasi kilichotolewa, shilingi **triliioni 10.52** ni fedha za matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 95.2** na **shilingi triliioni 2.60** ni fedha za maendeleo sawa na **asilimia 54.2**.

21. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za maendeleo, kiasi cha **shilingi bilioni 730.7** kutoka kwa washirika wa maendeleo zilizopelekwa moja kwa moja kwenye utekelezaji wa miradi na hivyo kufanya utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kufikia **asilimia 69.4**. Kadhalika, kiasi cha shilingi **bilioni 254.6** kilitumika kulipa malimbikizo ya madai yaliyohakikiwa ya watumishi, makandarasi na watoa huduma.

Mfumuko wa Bei

22. Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei nchini umeendelea kuwa tulivu na kubakia katika viwango vya chini. Kwa mfano, mfumuko wa bei kwa Desemba 2020 ulikuwa asilimia 3.2 ikilinganishwa na asilimia 3.8 Desemba 2019. Kwa hiyo, katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2020/2021, mfumuko wa bei ulikuwa wa wastani wa asilimia 3.2, ndani ya lengo la muda wa katil la asilimia 5.0.

23. Mheshimiwa Spika, kiwango hicho cha mfumuko wa bei kilitokana na upatikanaji wa chakula cha kutosha katika masoko ya ndani na nchi jirani, bei ndogo ya mafuta kwenye soko la dunia, utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani na sarafu nyngine duniani, na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti.

Mafanikio, Changamoto na Mikakati katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa nusu ya kwanza ya mwaka 2020/2021

24. Mheshimiwa Spika, wakati wa mkutano huu, Bunge lako tukufu lilipokea na kujadili mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2021/2022 pamoja na Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026.

25. Mheshimiwa Spika, wakati tukiendelea na maandalizi ya utekelezaji wa mipango hiyo kwa kipindi cha mwaka 2021/2022, nami nitumie nafasi hii kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wananchi wote baadhi ya mambo makubwa na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha wa 2020/2021.

26. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miezi sita ya kwanza ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021 (yaani Julai hadi Desemba 2020) yapo mafanikio mengi yaliyopatikana. Kadhalika, zipo changamoto zilizoibuka na kuifanya Serikali kuja na mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo katika kipindi cha miezi sita ya pili ya mwaka ili kufikia malengo yaliyowekwa kwa mwaka 2020/2021.

27. Mheshimiwa Spika, niruhusu japo kwa uchache nieleze baadhi ya mafanikio machache yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2020/2021. Aidha, baadhi ya mafanikio ni muendelezo wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

28. Mheshimiwa Spika, mafanikio hayo ni pamoja na Serikali kugharamia kwa mara ya kwanza Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 kwa kutumia fedha za ndani ambapo shilingi **bilion 268.5** zilitumika. Serikali pia ililipa shilingi **bilion 254.6** madeni ya wazabuni na watumishi yaliyohakikiwa; shilingi **trillion 3.64** mishahara ya watumishi; **shilingi bilioni 124.8** kwa ajili ya kugharamia sera ya elimumsingi bila ada na **shilingi bilioni 105.1** kwa ajili ya kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, uimarishaji wa vyo ufunzi stadi (VETA) na kukuza ujuzi kwa vijana.

29. Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kuendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati kama ifuatavyo: -

i. **Ujenzi wa Reli ya Kati Kwa Kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge Railway)** ambapo ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (km 300) umefikia asilimia 90 na kipande cha Morogoro – Makutupora (km 422) umefikia asilimia 49.2. Aidha, tayari Serikali imesaini mkataba wa ujenzi wa kipande cha Mwanza - Isaka (km 341) wenye thamani ya **shilingi trillion 3.07**; na kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa vipande vya Makutupora – Tabora (km 294) na Tabora – Isaka (km 133). **Shilingi bilioni 274.1** zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/2021. Baada ya kukamilika

matengenezo hayo, tutaanza kuunganisha vipande vya Tabora - Kigoma na Tabora – Mpanda.

ii. Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (Megawati 2,115): Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 25.8 ambapo **shilingi bilioni 128.9** zimetumika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/2021;

iii. Kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania: Serikali imekamilisha malipo ya mwisho ya ununuzi wa ndege aina ya Bombadier Dash 8-Q400 na Boeing 787-8 Dreamliner na malipo ya awali ya ununuzi wa ndege tatu (3), ambapo ndege mbili (2) ni aina ya Airbus A220-300 na moja (1) ni Dash 8-Q400 De-Havilland na hivyo kuwezesha Serikali kuwa na ndege mpya 11 kutoka ndege moja (1) iliyokuwepo mwaka 2015 na kuifanya ATCL kuwa na jumla ya ndege 12 ambapo ndege tatu (3) zinatarajjiwa kuwasilli mwaka 2021/2022 ili ziweze kutoa huduma. **Shilingi bilioni 2.8** zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/2021;

iv. Viwanja vya Ndege na Rada: Kukamilika kwa jengo la tatu la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) chenye uwezo wa kuhudumia abiria milioni sita kwa mwaka; kuendelea na ujenzi wa viwanja vya Geita (asilimia 86), Songea (asilimia 91) na Mtwara (asilimia 49.0); kukamilika kwa maandalizi ya mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato ambaao utagharimu dola za Marekani milioni 330, sawa na shilingi bilioni 759; uzinduzi wa ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Shinyanga, Kigoma, Tabora na Sumbawanga vinavyogharimu Euro milioni 50 sawa na shilingi bilioni 136.85; kuanza kwa ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege Musoma; kukamilika kwa ukarabati wa karakana ya matengenezo ya ndege na kununuliwa kwa magari mapya matatu (3) ya zimamoto yenye uwezo wa kubeba lita za maji 10,000 katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA); kupanuliwa kwa barabara ya kuruka na kutua ndege katika kiwanja cha ndege cha Dodoma; kufungwa kwa mifumo ya kuongoza ndege (AGL) katika viwanja vya ndege vya Dodoma, Tabora na Mwanza; na kupanuliwa na

kukarabatiwa kwa viwanja vya ndege vya Bukoba, Mwanza, Arusha, Nachingwea na Iringa. **Shilingi bilioni 4.5** zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/2021;

v. **Usambazaji wa Umeme Vijiji kuitia mradi kabambe wa kusambaza umeme vijiji na makao makuu ya wilaya (REA - III):** Hadi Desemba 2020, jumla ya vijiji 10,018 kati ya vijiji 12,317 sawa na asilimia 81.3 vilikuwa vimeunganishiwa umeme ambapo katika kipindi cha nusu ya kwanza ya 2020/21 **shilingi bilioni 171.9** zimetolewa na kazi inaendelea;

vi. **Kuboresha usafiri wa abiria na mizigo katika Maziwa Makuu:**

Ziwa Victoria: Kukamilika kwa ukarabati wa meli mbili za *New Butiama Hapa Kazi Tu* na *New Victoria Hapa Kazi Tu*; kuendelea na ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza Hapa kazi Tu yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo; kukamilika kwa ujenzi wa Chelezo cha kujengea na kukarabati meli katika Bandari ya Mwanza; kupatikana kwa mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa meli za MV Umoja na MV Serengeti; kukamilika ukarabati wa meli za MV. Clarias na ML. Wimbi.

Ziwa Tanganyika: kukamilika kwa mikataba kwa ajili ya Ujenzi wa Meli Mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 600 na tani 400 pamoja na ukarabati wa meli ya MV Liemba; na ukarabati wa meli ya MT Sangara kwenye Ziwa Tanganyika ambapo katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/2021 shilingi **bilioni 12.8** zimetumika. Tumeboresha bandari za Kibirizi, Sibwesa, Kagunga, Kabwe, Kasanya na sasa tunajenga bandari Kalema ambapo shilingi bilioni 86.4 zimetumika;

Shughuli nyingine zilizokamilika ni: Ujenzi wa magati ya Lushamba, Ntama, Nyamirembe, Magarine na Gati la majahazi Mwigobero; ununuzi wa vifaa vya kuhudumia mizigo na meli; ukarabati wa majengo na ofisi za bandari za Ziwa Victoria; kuboresha eneo la kushukia abiria Mwanza North; na ukarabati wa 'Link Span' ya bandari ya Mwanza South;

Ziwa Nyasa: Kukamilika kwa ujenzi wa matishari mawili (2) yenye uwezo wa kubeba tani 1000 kila moja; na ujenzi wa meli moja mpya ya MV Mbeya II yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na mizigo tani 200 umekamilika na imeanza kufanya kazi. **Shilingi bilioni 1.5** zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/2021;

vii. **Ujenzi wa Barabara na Madaraja Makubwa:** Kujengwa kwa mtandao wa barabara kwa kiwango cha lami wenye urefu wa kilomita 3,537 (barabara kuu na za mikoa kilomita 2,208.62 na barabara za halmashauri kilomita 1,328) na hivyo kufanya mtandao wa barabara uliojengwa kwa kiwango cha lami hadi mwaka 2019/2020 kufikia kilomita 13,044 ambapo kilomita 10,939 ni barabara kuu na kilomita 2,105 ni barabara za mikoa. Ujenzi huu umeongeza uwiano wa mtandao wa barabara za lami nchini kutoka asilimia 6.8 mwaka 2015/2016 hadi asilimia 8.9 mwaka 2019/2020;

viii. **Uendelezaji wa Mji wa Serikali Mtumba - Dodoma:** Serikali imeanza maandalizi ya awamu ya pili ya ujenzi wa majengo ya ofisi katika Mji wa Serikali Mtumba yatakayotosheleza watumishi wote. Katika mwaka 2019/2020, Serikali imekamilisha usanifu wa majengo husika. Aidha, mradi wa ujenzi wa barabara (km 51.2) kwa kiwango cha lami katika Mji wa Serikali utakaogharimu jumla ya shilingi bilioni 89.13 unaendelea, ambapo malipo ya awali ya shilingi bilioni 13.21 yamefanyika na ujenzi umefikia asilimia 56;

ix. **Miradi ya Vivuko:** Kukamilisha ujenzi wa vivuko vipyta vya Kigongo - Busisi (Mwanza), Bugolora – Ukara (Mwanza) na Kayenze – Bezi (Mwanza). Aidha, ujenzi wa kivuko kipyta cha Nyamisati – Mafia (Pwani) na Chato – Nkome (Geita) umekamilika. Vilevile, ujenzi wa boti mpya tano (5) za uokozi kwa ajili ya kisiwa cha Ukerewe (Ilugwa, Nafuba na Gana), kivuko cha Magogoni – Kigamboni na Lindi – Kitunda unaendelea. Pia, ukarabati mkubwa wa MV Kigamboni umekamilika na ukarabati wa kivuko MV Sengerema umefikia asilimia 90;

- x. **Mifugo:** Kujenga kiwanda kipywa cha *Kilimanjaro International Leather Industries Company Ltd* chenye uwezo wa kuzalisha jozi na soli za viatu 1,200,000 kwa mwaka na kuchakata ngozi futi za mraba 13,000,000 kwa mwaka; kuimarisha kituo cha Taifa cha Uhimilishaji cha NAIC kilichopo USA River, Arusha kwa kununua kifaa (Chiller) kwa ajili ya mtambo wa kuzalisha kimiminika cha naitrojeni; kujengwa kwa viwanda vipywa vyta kimkakati vyta nyama vyta *Tanchoice* (Pwani), *Elia Food Oversees Limited* (Arusha) na *Binjiang Company Limited* (Shinyanga); kujengwa kwa kiwanda cha maziwa cha *Galaxy Food and Beverage Company Limited* (Arusha); kujengwa kwa kiwanda cha kuzalisha chanjo cha *Hester Bioscience Africa Limited* (Pwani) chenye uwezo wa kuzalisha chanjo aina 37; na kuendelea kuboresha huduma za malisho ya mifugo na majosho.
- xi. **Uvuvi:** Kuongezeka kwa uzalishaji/uvunaji wa samaki katika maji ya asili kutoka tani 362,645 zenyet thamani ya shilingi trillioni 1.48 mwaka 2015/2016 hadi tani 497,567 za samaki zenyet thamani ya shilingi trillioni 2.34 mwaka 2019/2020; kuongezeka kwa usindikaji wa minofu ya samaki aina ya Sangara kutoka tani 23,000.58 mwaka 2015/2016 hadi tani 27,596.27 mwaka 2019/2020; kuongezeka kwa huduma za usafirishaji wa mazao ya uvuvi kwenda masoko ya Ulaya ambapo katika mwaka 2019/2020, jumla ya kilo 777,750.0 za mabondo zilisafirishwa; kuongezeka kwa mauzo ya samaki na mazao ya uvuvi nje ya nchi kutoka mauzo yenye thamani ya shilingi bilioni 379.25 mwaka 2015/2016 hadi shilingi bilioni 506.24 mwaka 2019/2020; na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa bandari ya uvuvi (Mbegani). Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/2021 **shilingi milioni 606.7** zimetumika;

- xii. **Miradi ya Maji:** Kukamilika kwa miradi 1,423 ya maji iliyotekelizwa mijini na vijiji. Baadhi ya miradi iliyotekelizwa na hatua zilizofikiwa ni: kukamilika kwa miradi ya maji katika miji ya Geita, Njombe na Songwe na kuendelea kwa ujenzi wa mradi wa maji katika mji wa Kigoma (asilimia 90); utekelezaji wa mradi mkubwa wa Maji wa Ziwa Victoria kwenda katika miji ya Isaka, Tinde, Kagongwa, Tabora, Igunga, Uyui na Nzega umefikia asilimia 98; kukamilika kwa

asilimia 76 ya ujenzi wa mradi wa maji katika Jiji la Mwanza; kukamilika kwa asilimia 62 ya ujenzi wa mradi wa maji katika Jiji la Arusha; na kuendelea na ujenzi wa mradi wa maji wa Same – Mwanga – Korogwe ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 65. Aidha, katika eneo linalohudumiwa na DAWASA (mikoa ya Dar es Salaam na Pwani) utekelezaji wa miradi umekamilika kwa zaidi ya asilimia 90 na umehusisha maeneo ya Kibamba hadi Kisarawe, Mlandizi hadi Chalinze, Kisarawe-Pugu-Ukonga, Mkuranga-Vikindu, Jet-Buza, Kisarawe, Kigamboni, Mkuranga, Chalinze, Mbezi Luis hadi Kiluvya, Tegeta, Wazo, Madale, Mivumoni, Mabwepande na Bagamoyo (maeneo ya Vikawe, Zinga, Mapinga na Kerege).

Kwa ujumla miradi yote iliyotekeliza imewezesha wananchi zaidi ya milioni 25 kupata huduma ya maji ambapo wastani wa idadi ya watu wanaopata huduma ya maji safi na salama imeongezeka kutoka **asilimia 74** mwaka 2015 hadi **asilimia 84** mwaka 2020 kwa mijini na kutoka **asilimia 47** mwaka 2015 hadi **asilimia 70.1** mwaka 2020 kwa vijijini. Aidha, kwa Jiji la Dar es Salaam, upatikanaji wa maji safi umeongezeka kutoka **asilimia 72** mwaka 2015 hadi **asilimia 90** Desemba, 2020. Shilingi **bilioni 226.7** zimetumika katika nusu ya kwanza ya 2020/2021. Kazi ya usambazaji maji vijijini inaendelea;

xiii. **Afy**: Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya sekta ya afya ambayo imefikia hatua mbalimbali ikiwemo: asilimia 98 ya ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa Mwananyamala; Ujenzi wa jengo la maabara katika Hospitali ya Rufaa Njombe umefikia asilimia 73; ujenzi wa jengo la mama na mtoto, upasuaji, radiolojia na maabara katika Hospitali ya Rufaa Simiyu umefikia asilimia 50. **Shilingi bilioni 64.6** zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/2021 kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya afya, ununuzi wa vifaa, vitendanishi, dawa na chanjo; na

xiv. **Miradi ya Kimkakati ya Kuongeza Mapato Katika Halmashauri**: Katika kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaongeza mapato kwa kutumia fursa zilizopo katika maeneo yao, Serikali ilitoa shilingi bilioni 91.4 kwa ajili ya kugharamia miradi 26. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni

50.6 zilitolewa mwaka 2019/2020. Miradi ya ujenzi iliyotekelawa ni pamoja na; stendi za mabasi (9), machinjio (2), viwanda vidogo (3), maegesho ya malori (2), masoko (9) na ghala la mazao (1). Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya 2020/2021, Serikali imetua shilingi **bilioni 19.9** kwa ajili ya kugharamia miradi ya kimkakati;

30. Mheshimiwa Spika, licha ya mafanikio hayo makubwa ambayo nimejaribu kueleza kwa uchache, vilevile, katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali kwa nusu ya kwanza ya mwaka 2020/2021, zipo changamoto kadhaa zilizojitezea. Changamoto hizo ni pamoja na uharibifu wa miundombinu ya barabara uliosababishwa na mafuriko; kupungua kwa shughuli za kibiashara duniani kutokana na athari za mlipuko wa homa kali ya mapafu; kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi; na ukwepajji kodi kwa baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu, hususan kuititia biashara za magendo, kutotoa na kudai stakabadhi za kielektroniki wakati mauzo yanapofanyika na kasi ndogo ya ukusanyaji wa kodi ya majengo.

31. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari hadi Juni 2021, Serikali itaendelea kuchukua hatua na kutekeleza mikakati mbalimbali kwa lengo la kuongeza mapato na kuimarisha usimamizi wa matumizi ili kufikia malengo kwa kipindi kilichobaki cha mwaka 2020/2021. Mionganoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na kuendelea kuchukua hatua za tahadhari dhidi ya majanga na kufanya ukarabati wa miundombinu iliyoharibiwa na mafuriko na kuimarisha ukaguzi wake.

32. Mheshimiwa Spika, halikadhalika, Serikali itaendelea kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima; kuhakikisha nakisi ya bajeti haizidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa na hivyo, kuendana na makubaliano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; kuelekeza fedha kwenye maeneo ya kipaumbele yatakayochochea ukuaji wa uchumi; kuhakikisha miradi inayoendelea inapewa kipaumbele kabla ya miradi mipya; kudhibiti ulimbikizaji wa

madai; na kuongeza kasi ya matumizi ya TEHAMA katika miamala na shughuli za Serikali.

33. Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, Serikali itatekeleza mikakati mahususi ya kuongeza mapato kwa kufanya yafuatayo:-

Mosi: Kuimarisha mifumo ya usimamizi kwa kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wote wanatumia mashine za kutolea risiti za kielektroniki (EFD);

Pili: Kuimarisha ushirikiano kati ya mamlaka zinazokusanya mapato ya Serikali na vyombo vya ulinzi na usalama katika kufanya doria maeneo ya mipaka ya nchi kavu, bahrini na kwenye maziwa ili kudhibiti biashara za magendo;

Tatu: Kukasimisha jukumu la kukusanya kodi ya majengo kwa Halmashauri na Serikali za Mitaa.

34. Mheshimiwa Spika, niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa kuibua hoja ambazo zilifanya mjadala wetu humu Bungeni kuwa wa kina na wenyewe kutoa msisimko wa kiwango cha juu. Yote hayo, yalitokana na ukweli kwamba Waheshimiwa Wabunge, waliiuba hoja na kuchangia kwa umakini mkubwa kwa lengo kujenga na kusaidia taifa letu.

35. Mheshimiwa Spika, kwa upande mwininge kuititia hoja na michango yao, Waheshimiwa Wabunge wamegusia masuala muhimu ikiwemo elimu, kilimo, uwezeshaji, uwekezaji, viwanda na miundombinu ambayo yamekuwa kitovu cha mjadala na michango ya Waheshimiwa Wabunge. Kwa msingi huo, naomba nitumie fursa hii adhimu kutolea ufanuzi baadhi ya masuala muhimu yaliyoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge.

ELIMU

Miundombinu ya Elimu

36. Mheshimiwa Spika, kuititia Mkutano huu wa Pili wa Bunge lako tukufu, Waheshimiwa Wabunge wameibua hoja nyingi

kuhusu changamoto ya miundombinu ya shule hususan sekondari, suala la ujuzi na mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Nyingi ya changamoto hizi, zinatokana na utekelezaji mzuri wa sera ya Elimumsingi Bila Malipo sambamba na ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya shule na vyuo ambao umechangia kuongezeka kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza na hata darasa la kwanza kila mwaka.

37. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa samani na miundombinu, Serikali imeweka mikakati imbalimbali ikiwemo ya muda mfupi na muda mrefu. Lengo la Serikali ni kuhakikisha wanafunzi wote waliofaulu mtihani wa Darasa la Saba wanajiunga na kidato cha kwanza bila kujali ni chaguo la kwanza au la pili na kuhakikisha miundombinu yote na samani zote kwa ajili ya kuwapokea wanafunzi hawa inakamilika ifikapo tarehe 28 Februari, 2021.

38. Mheshimiwa Spika, Benki ya Dunia iliidhinisha mkopo wa kiasi cha Dola za Marekani milioni 500 sawa na takriban shilingi za Tanzania trillioni 1.2 kwa ajili ya mradi wa maboresho ya elimu ya sekondari yaani (*Secondary Education Quality Improvement Programme - SEQUIP*). Mradi huo, uliidhinishwa mwaka jana licha ya kelele nyingi kutoka kwa watu wasiokuwa na uzalendo na nchi hii.

39. Mheshimiwa Spika, mradi huo, utakaotekelawa kwa muda wa miaka mitano (2020/2021 - 2025/2026) utakuwa ni mwarobaini kwa changamoto ya miundombinu ya shule za sekondari kwani shule mpya **1,026** zitajengwa kote nchini. Kati ya shule hizo, shule mpya **26** zitakuwa za Bweni zenye uwezo wa kupokea wanafunzi kati ya **1,000** hadi **1,500** kwa kila mkoa na zitajengwa kwa awamu tatu.

40. Mheshimiwa Spika, kadhalika, Shule mpya **1,000** za kutwa zitajengwa zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **400** kwa kila shule. Shule hizo zitajengwa kwenye kata **718** zisizo na sekondari za kata na kwenye maeneo yaliyoelemewa na idadi kubwa ya wanafunzi. Hivyo basi, nitumie nafasi hii kuwaelekeza viongozi na watendaji wa Serikali za Mitaa

wasimamie kikamilifu utekelezaji wa mradi huu ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mikopo ya Elimu ya Juu

41. Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo ya elimu ya juu, kwa mwaka huu 2020/2021 Serikali imetoa mikopo kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza **55,287** ambapo wanafunzi **28,041** sawa na **asilimia 5** wamehitimu elimu ya sekondari katika shule mbalimbali za binafsi. Serikali itaendelea kuzingatia kigezo pekee cha uhitaji wa mwombaji sambamba na kurahisisha matumizi ya mtandao katika uombaji na utoaji wa mikopo.

42. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza ufanisi wa utoaji na urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu, Serikali imefanya maboresho ya kisheria, kimfumo na kicutendaji kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita (**2015/2016 – 2019/2020**). Matunda ya maboresho hayo ni pamoja na kuongezeka kwa makusanyo kutoka wastani wa **shilingi 28.9 billioni** mwaka **2016/2017** hadi kufikia wastani wa **shilingi 192 billioni** mwaka **2019/2020**.

43. Mheshimiwa Spika, Serikalini inafarijika na inapokea kwa mikono miwili michango yenye afya na tija kuhusu hatma ya mikopo inayotolewa na Serikali baada ya miaka 15 ya uwepo wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

44. Mheshimiwa Spika, nilihakikishie Bunge lako tukufu kwamba Serikali kwa upande wake, ipo tayari kuendelea kujifunza kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote nchini kuhusu namna bora zaidi ya kuufanya mfuko huu uwe endelevu na wenye manufaa katika ujenzi wa uchumi wa nchi yetu. Hivyo basi, katika kuufanya mfuko huo uwe endelevu na himilivu; nitumie fursa hii kuelekeza mambo yafuatayo;

Kwanza: Ninaitaka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ishirikiane na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ili kuboresha huduma zake na kurahisisha urejeshwaji wa mikopo kwa wanufaika waliojari katika sekta binafsi, ikiwa ni

pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu haki na wajibu wa mnufaika na mwajiri.

Pili: Ninawasihi wanufaika wote wa mikopo ya elimu ya juu, ambao bado hawajajitokeza na kuanza kurejesha, wafanye hivyo mara moja;

Mwisho: Ninawataka waajiri wote nchini katika sekta binafsi na sekta ya umma, watoe kipaumbele kwa makato ya mikopo ya elimu ya juu kama yalivyo makato mengine ya kisheria; na

Ukuzaji Ujuzi

45. Mheshimiwa Spika, ukuzaji ujuzi ni mionganini mwa hoja iliyoungwa mkono na Wabunge wengi wakati wa kuchangia hoja mbalimbali hususan ya elimu wakati wa mkutano huu. Hivyo, nami nitumie nafasi hili kullarifu Bunge lako tukufu kwamba katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Januari, 2021 vijana **10,178** wamepatiwa mafunzo na kutathminiwa ujuzi walioupata nje ya mfumo rasmi wa mafunzo nchi nzima ambapo vijana **9,736** wamefaulu na kupatiwa vyeti na Mamlaka ya Mafunzo na Ufundu Stadi (VETA).

46. Mheshimiwa Spika, vyeti hivyo vinawawezesha kutambulika, kuijiendeleza kiujuzi, kujiajiri pamoja na kupata kazi katika taasisi na kampuni mbalimbali. Vijana hao ni wenye ujuzi katika fani za uashi, useremala, ushonaji, ufundu bomba, uchomeleaji na uungaji vyuma, ufundu magari, ufundu umeme, ukarabati wa bodi za magari, upishi na uhudumu katika hoteli. Aidha, vijana **36** wamegharamiwa na Serikali kwa ajili ya kuhudhuria mafunzo ya kilimo cha kisasa nchini Israel.

47. Mheshimiwa Spika, katika nusu ya pili ya mwaka 2020/2021 vijana wapatao **4,616** watapatiwa mafunzo na kurasimishwa ujuzi walionao kupitia mfumo huu. Aidha, mwezi Januari 2021, vijana **1,203** wa vyuo vya elimu ya juu na kati wamehitimu mafunzo ya uzoefu wa kazi kupitia kampuni mbalimbali kulingana na fani walizosomea, na Wahitimu **2,037** wamewezeshwa na wanaendelea kupata mafunzo ya

uzoefu wa kazi katika taasisi binafsi na za umma ambayo yatachukua muda wa kipindi cha mwaka mmoja. Vilevile, Wahitimu **2,421** wanaandaliwa kwa ajili ya kuanza mafunzo mwezi Machi, 2021 katika fani za ushonaji nguo, useremala, uashi, uchorongaji vipuri, ufundi magari, umeme, bomba, terazo, upishi, na utoaji huduma za mahoteli, utengenezaji wa simu, majokofu, viyoyozi, upakaji rangi, uandishi wa alama, utengenezaji wa umeme wa magari, utengenezaji wa nywele na utanashati, uchoraji, n.k.

Barabara

48. Mheshimiwa Spika, kumejitokeza mjadala unaohitaji uboreshaji miundombinu ya barabara za mijini na hasa za vijijiini. Vyombo vyetu vya TANROADS na TARURA vinafanyia kazi na sasa tunakusudia kuongeza uwezo wa vyombo hivyo. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge tumepokea ushauri wenu na tutaufanya kazi illi tuweze kufanya maboresho.

KILIMO

Hali ya Kilimo katika Msimu huu wa kilimo

49. Mheshimiwa Spika, katika msimu wa mvua wa mwaka 2020/2021, mvua za vuli zilizoanza mapema mwezi Septemba zimeendelea kunyesha kwa kiwango cha juu ya wastani katika maeneo mengi hasa ya Kanda ya Ziwa Victoria. Katika maeneo mengine ya Pwani ya Kaskazini na Kanda ya Kaskazini Mashariki, mvua zilichelewa kuanza (Novemba) na zimeendelea kunyesha hadi katika mwezi Januari, 2021.

50. Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Januari, mwenendo wa unyeshaji wa mvua hizo umeendelea kwa kiwango cha juu ya wastani katika maeneo mengi. Mwelekeo unaonesha kuwa mvua hizi zitachangia upatikanaji wa chakula katika kipindi cha mwezi Februari na kuendelea kabla ya mavuno mengine kuanzia mwezi Mei, 2021. Vilevile, hali ya malisho ya mifugo na upatikanaji wa maji umeendelea kuwa mzuri katika maeneo yote nchini.

Kuimarisha Kilimo cha Umwagiliaji

51. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020, Serikali imefanikiwa kujenga na kukarabati skimu za

umwagiliaji **179** ambazo zimeongeza eneo la umwagiliaji kutoka **hekta 461,000** mwaka 2015 hadi **hekta 694,715 mwaka 2020** sawa na ongezeko la **asilimia 50.7**. Hii ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2018 (yaani **Revised National Irrigation Master Plan - RNIMP 2018**) ambao umeainisha hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa kilimo cha Umwagiliaji.

52. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imekamilisha ujenzi wa maghala 14 ya kuhifadhi mavuno katika skimu za umwagiliaji za **Ngana** na **Makwale** (Kyela), **Magozi** na **Tungamalenga** (Iringa), **Mbuyuni-Kimani**, **Ipatagwa**, **Kongolo-Mswisi** na **Motombaya** (Mbarali), **Lekitatatu** (Arusha), **Mombo** (Tanga), **Uturo** (Mbeya), **Bagamoyo** (Pwani), **Mkindo** na **Mkula** (Morogoro).

53. Mheshimiwa Spika, katika hatua ya kuongeza mnyororo wa thamani kwenye uzalishaji wa mazao ya kilimo, kati ya maghala hayo, **maghala 6** yamewekewa na vinu vya kukobolea mpunga.

54. Mheshimiwa Spika, nimeamua kusema haya ili Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujuma wafahamu kwamba tunatambua umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji na tunachukua hatua.

Upatikanaji wa pembejeo za kilimo na uzalishaji wa mbegu

55. Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mikakati ya kuhakikisha pembejeo zinawafikia wakulima kwa wakati ambayo ni pamoja na kupata mahitaji halisi ya pembejeo za kilimo kutoka kila mkoa kabla ya msimu wa kilimo kuanza na kuwasiliana na Makampuni ya pembejeo na kuyahimiza kusambaza pembejeo hizo mapema kulingana na mahitaji ya kila mkoa.

56. Mheshimiwa Spika, pia, Serikali inaboresha mifumo ya uzalishaji, uagizaji na uthibiti wa mbegu bora na viuatilifu hapa nchini ikiwemo kuimarisha uzalishaji wa pembejeo hizo ndani ya nchi ili kukidhi mahitaji na upatikanaji wake kwa wakati.

57. Mheshimiwa Spika, katika kufikia malengo, Serikali itaongeza eneo la ASA la uzalishaji wa mbegu kutoka hekta 4,925 (2019/2020) hadi hekta 6,923 ifikapo 2025 na eneo la TARI kutoka hekta 1,033.2 hadi hekta 3,663.24 ifikapo 2025.

Huduma za Ugani

58. Mheshimiwa Spika, uzalishaji na tija katika kilimo, pamoja na mambo mengine huchangiwa na maarifa na ujuzi unaotolewa na Maafisa Ugani kwa wakulima. Kwa mantiki hiyo, Serikali inalenga kuhakikisha kuwa kila kijiji, mtaa na kata vinakuwa na Afisa Ugani angalau mmoja ili kuwawezesha wakulima kupata maarifa na ujuzi wa kuzalisha mazao kwa ufanisi na tija.

59. Mheshimiwa Spika, idadi ya Maafisa Ugani waliopo nchini ni 6,704 ikilinganishwa na mahitaji 20,538. Aidha, katika kukabiliana na changamoto ya uhaba wa Maafisa Ugani, Wizara inaendelea kusomesha Maafisa Ugani tarajali katika ngazi ya Cheti na Diploma ambapo kuanzia mwaka 2015 hadi 2020 jumla ya wataalamu wa kilimo 8,657 walihitimu katika vyuo vya mafunzo ya kilimo ngazi ya Cheti na Diploma.

UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

Mifuko na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

60. Mheshimiwa Spika, kama niliviotangulia kueleza, suala la uwezeshaji Wananchi iwe kwenye sekta ya kilimo au ujasiriamali na biashara ndogo na za katni miongoni mwa hoja zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge. Suala hilo, pia limejitokeza wazi wazi kwenye hotuba ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alioitoa tarehe 13 Novemba, 2020 wakati akifungua Bunge la 12.

61. Mheshimiwa Spika, katika hotuba hiyo, Mheshimiwa Rais allielekeza Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kuwa inaimarisha uratibu na usimamizi wa Mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi ili Watanzania waifahamu ilipo, vigezo vya kutolea mikopo na aina ya mikopo. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa wananchi wananaufaika na mikopo hiyo ili kuinua vipato vyao, kupunguza umaskini na tatizo la ajira.

62. Mheshimiwa Spika, licha ya changamoto zinazokabili mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi, katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2015/2016 hadi 2019/2020, mifuko na programu za uwezeshaji za serikali zimefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani zaidi ya shilingi **triliion 2.22**, kunufaisha zaidi ya watu **milioni 4.9** na taasisi 5,499.

63. Mheshimiwa Spika, vilevile, kupitia mifuko ya uwezeshaji wa makundi maalumu ya Vijana, Wanawake na Watu wenye Ulemavu **Halmashauri 185** zimefanikiwa kutoa shillingi **bilioni 93.3**. Fedha hizo, zimewezesha upatikanji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa **vikundi 32,553** kote nchini.

64. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha malengo hayo yanafikiwa napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba tumeanza kuchukua hatua zenye kulenga kuboresha huduma za mifuko na programu za uwezeshaji. Tarehe 17 Novemba, 2020 tulianza zoezi la tathmini ya utendaji wa programu na mifuko takriban 20. Aidha, tayari taarifa ya awali kutoka ngazi ya Wataalamu imekamilika na kuwasilishwa kwenye mamlaka husika.

65. Mheshimiwa Spika, tarehe 9 Februari 2021 nilifungua wiki ya maonesho ya nne ya mifuko na programu za uwezeshaji kwa kanda ya Kaskazini yanayofanyika kwenye viwanja vya Sheikh Amri Abeid, Arusha. Ni Matumaini yangu kwamba kupitia maonesho hayo wananchi wa mkoa wa Arusha, mikoa ya kanda ya Kaskazini pamoja na wananchi kutoka sehemu mbalimbali nchini watapata uelewa mpana kuhusu shughuli za mifuko na programu za uwezeshaji.

Mabenki na Mifuko ya Fedha Kuchangia Kilimo

66. Mheshimiwa Spika, wakati tukiendelea na mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge walieleza kwa kina kuhusu changamoto mbalimbali zinazowakabili wakulima na wafanyabiashara wetu hususan wadogo katika shughuli zao za kiuchumi na kujiongezea kipato hususan masuala ya uzalishaji, masoko, ufungashaji bora wa bidhaa, huduma za fedha, elimu ya ujasiriamali, teknolojia n.k.

67. Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba mchango wa sekta ya fedha hususan mabenki na mifuko ya hifadhi za jamii kwenye kilimo bado ni mdogo kwani hadi sasa upo kwenye **asilimia 8.5** sawa na shilingi **triliioni 1.65**. Kwa msingi huo, Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na Benki na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuona namna ambavyo watachangia katika shughuli za kilimo na mnyororo mzima wa thamani.

Uwezeshaji wa Wajasiriamali Wadogo (Machinga)

68. Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na kuthamini sana mchango mkubwa unaotolewa na wafanyabiashara wadogo (Wamachinga) katika kukuza uchumi, kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja, kuondoa umaskini na kuleta maendeleo endelevu nchini. Sekta hii ya wafanyabiashara wadogo nchini inakadirwa kuwa na wajasiriamali **milioni 3.1** ambaao wameajiriwa sawa na takriban **asilimia 23.4** ya nguvu kazi ya Taifa.

69. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wadau wa sekta hii wanaendesha shughuli zao bila kubughudhiwa, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliamua kugawa vitambulisho vya wajasiriamali wadogo. Hata hivyo, licha ya mafanikio makubwa ya vitambulisho hivyo, vimeonesha kuwa na changamoto mbalimbali ambazo zinahitaji maboresho hususan katika kuwasaidia kupata mikopo na mitaji kutoka kwenye taasisi za fedha ili waweze kuendesha shughuli mbalimbali za ujasiriamali.

70. Mheshimiwa Spika, katika kuwasadia wajasiriamali wadogo kupata mitaji kwa urahisi kuptitia taasisi za fedha, Serikali imeanza taratibu za kuboresha Vitambulisho vya Wafanyabiashara Wadogo kwa mwaka 2021. Vitambulisho hivyo vitakuwa vya kielektroniki na vitaboreshwa zaidi hatua kwa hatua ili viwawezesha wafanyabiashara wadogo kukopa kutoka taasisi za fedha ikiwemo programu na mifuko ya uwezeshaji.

71. Mheshimiwa Spika, tarehe 28 Januari, 2021 nilipata fursa ya kufungua Kongamano la Wafanyabiashara Wadogo

(maarufu Wamachinga) lillofanyika Jijini Dar es Salaam. Lengo la Kongamano hilo, pamoja na mambo mengine lilikuwa ni kuwashirikisha wadau hao kuhusu namna nzuri zaidi ya kuboresha vitambulisho vya wafanyabiahara wadogo (Wamachinga) ili waweze kuvitumia kupata mitaji au mikopo kutoka kwenye mabenki na taasisi za fedha.

72. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwapongeza wafanyabiashara wadogo (Wamachinga) kwa kutekeleza vyema jukumu la usambazaji wa bidhaa nchini kwa bei nzuri wanazozimudu wananchi hasa wale wa kipato cha chini. Aidha, nitoe rai kwa Machinga wote kuepuka kushirikiana na wafanyabiashara wakubwa wanaowatumia kukwepa kodi; kwa kuwapa bidhaa nyangi bila kutoa risiti za kielektroniki zenye kiwango halisi cha bei ya kununulia bidhaa husika.

73. Mheshimiwa Spika, wakati tunaendelea na zoezi la kuboresha vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo, naagiza viongozi na watendaji wa Serikali za Mitaa washirikiane na viongozi wa wafanyabiashara wadogo kwenye maeneo yao ili kupata orodha yao na kuwaandalia maeneo ya kufanya biashara zao.

MICHEZO

74. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha hivi karibuni nchi yetu imepata mafanikio mbalimbali hususan katika mpira wa miguu. Nitumie nafasi hii kutoa pongezi zangu kwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kwa mafanikio makubwa yanayojitokeza kwa upande wa soka na michezo mingine kama ngumi hapa nchini. Mathalan, katika kipindi hiki tumeshuhudia Tanzania ikishiriki fainali za mashindano ya Afrika ya Mpira wa Miguu kwa wachezaji wanaocheza ligi ya ndani (CHAN) ambayo yamekamilika hivi karibuni huko Cameroon.

75. Mheshimiwa Spika, nizipongeze pia timu za Taifa za umri wa chini ya miaka 20 na 17 ambazo zimefuzu kushiriki katika mashindano ya Fainali za Bara la Afrika kwa mwaka 2021. Timu hizi zitakwenda kushiriki katika fainali za michuano hiyo

katika nchi za Morocco kwa U-17 na Mauritania kwa timu ya U-20. Vilevile, naipongeza timu ya Wanawake U-17 kushinda kombe la COSAFA kwa mashindano yaliyofanyika Afrika Kusini, Novemba 2020.

76. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa soka la vilabu, naipongeza Namungo FC kwa kufanikiwa kuvuka hatua mbili za awali kuelekea kwenye makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika na pia niwatakie kila la heri kwenye mchezo wao utakaochezwa kesho Jumapili huko nchini Angola.

77. Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia mabingwa wa Soka Tanzania, timu ya Simba Sports Club kwa kufanikiwa kufuzu kuingia hatua ya makundi katika mashindano ya Klabu Bingwa Afrika, na jana kushinda mchezo wake wa kwanza katika hatua ya makundi wakiwa ugenini dhidi ya Klabu ya AS Vita huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Nitumile nafashi hii kumpongeza Mtendaji Mkuu wa timu hiyo, mwanadada Barbra Gonzalez kwa ubunifu na kushirikisha Wizara ya Maliasili na Utalii na hivyo kulipa heshima Taifa letu kwa kulitangaza kupitia jezi yao kwa maneno **VISIT TANZANIA** huu ni uzalendo wa hali ya juu ambo unapaswa kupongezwa na kuigwa.

78. Mheshimiwa Spika, mchambuzi maarufu wa michezo nchini Bw. Ali Kamwe, kupitia ukurasa wake wa **instagram**, ameeleza vizuri maana ya matumizi ya neno **VISIT TANZANIA** na namna nchi yetu itakavyonufaika na ubunifu huo. Kwa mujibu wa maelezo yake, neno **VISIT TANZANIA** linakadiriba kutazamwa na wapenzi wa soka takriban milioni 500 kutoka sehemu mbalimbali duniani. Wapenzi hao wa mpira kupitia vituo vya Televisheni vya Canal Algérie, BeIN Sports, Eurosport, ESPN, Arryadia, GTV ya Ghana, MENA beIN Sports na West Africa Canal+ wameshuhudia mchezo wa jana. Kwa lugha nyingine ni kwamba neno 'VISIT TANZANIA' liliopo sehemu ya kifuani mwa jezi ya Klabu ya Simba litaonekana kupitia chaneli hizo kwa kila dakika 90 ambazo Simba itashuka dimbani iwe dhidi ya Al-Ahly (Misri), El-Mereikh (Sudan) au dimba la nyumbani kwa Mkapa (Tanzania). Tutavuta watalii wengi kuifuatilia Nchi yetu.

79. Mheshimiwa Spika, nchi yetu imeendelea kung'ara pia kwenye medani ya masumbwi. Kwa upande huo wa masumbwi, nawapongeza mabondia Mfaume Mfaume kwa kufanikiwa kutetea ubingwa wa East and Central Africa mwezi Decemba 2020; Bondia Ibrahim Class Mgendera kwa kushinda Ubingwa wa *World Boxing Federation Intercontinental lightweight* (WBF). Vilevile, nawapongeza Bondia Tonny Rashidi aliyefanikiwa kutetea mkanda wake wa African Boxing Union (ABU) na Bondia Shabani Hamadi JONGO aliyeshinda ubingwa wa WBF International Cruiserweight mwishoni mwa Januari 2021. Bila kuwasahau Mabondia walioonesha uwezo mkubwa wa kina Hassan Mwakinyo, Twaha Kiduku na Dulla Mbabe ambaye atapanda ulingoni tarehe 26 Februari, 2021.

HITIMISHO

80. Mheshimiwa Spika, nihitimishe hotuba yangu kwa kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu muhimu mliyoitoa kwa lengo la kuboresha maisha ya wananchi wetu. Nimshukuru Katibu wa Bunge, wasaidizi wake na watumishi wote wa Bunge kwa huduma nzuri na msaada mkubwa ambao wamekuwa wakitupatia kwa kipindi chote tulichokuwa tukitekeleza majukumu yetu ya Mkutano wa Pili wa Bunge la 12.

81. Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia viongozi na watendaji wa Serikali na taasisi zake ambao wameendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi, umahiri na ufanisi mkubwa. Hongereni sana kwani juhudini zenu zimekuwa chachu ya kufanikisha shughuli zilizopangwa kwenye Mkutano huu wa Pili wa Bunge la 12. Vilevile, nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo sitowashukuru wanahabari kwa uchambuzi mzuri wa hoja na mwenendo mzima wa Bunge na kuwashabariwananchi.

82. Mheshimiwa Spika, vilevile, nivishukuru vyombo vyao ulinzi na usalama kwa huduma ambazo wamekuwa wakizitoa kwa washiriki wa Bunge hili. Pia, niwashukuru madereva wote waliotuhudumia wakati wote tukiwa hapa Bungeni na ninawatachia heri katika safari ya kurejea nyumbani.

83. Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu liahirishwe hadi tarehe 30 Machi 2021 siku ya **Jumanne saa tatu kamili** asubuhi katika ukumbi huu hapa Jijini Dodoma.

84. Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofii*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushikuru sana kwa hotuba yako muhimu, ahsante sana. (*Makofii*)

Sasa Waheshimiwa Wabunge alichofanya Waziri Mkuu ni kumalizia kwa kuweka hoja ambayo mmeiunga mkono, lakini Kikanuni napaswa kuwahoji ili hoja ikamilike.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Waliofiki wameshinda. Watu hawataki kuondoka Dodoma. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge na mimi nitoe shukrani nyingi sana kwenu nyote kwa kipindi hiki ambacho tumefanya kazi vizuri kweye Kamati zetu na ilikuwa ni mwanzo wa Kamati kufanya kazi, mmeshaanza kuzoeana na mmepata nafasi ya kuzijua Wizara ambazo mnafanya nazo kazi, miundo yao, majukumu yao, lakini pia tulipokuja hapa tumejadili vizuri hotuba ya Rais aliyoitoa wakati akifungua Bunge hili, lakini pia tumepata mawasilisho ya Mpango kwa Miaka Mitano na Mwaka Mmoja na tumejadiliana vizuri sana kwa wiki moja. (*Makofii*)

Tunawashukuru sana wenzetu Serikalini, Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri na wataalam wote kutoka

Wizara mbalimbali waliokuwa nasi ambao wametusikiliza kwa umakini mkubwa. Mawazo mengi yametolewa naamini kila Wizara mahala pake watajaribu kuyafanya kazi na yale ambayo yanahitaji kuingizwa katika bajeti basi katika mkutano unakuja ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu ametangaza hapa kwamba kuanzia tarehe 30 Machi, 2021 siku ya Jumanne tukutane hapa, basi labda baadhi yake tutaanza kuyaona yakiwemo kwenye bajeti inayokuja.

Kwa hiyo, niwashukuru sana nyote na niwatakie kila la heri, tutakapokuwa tunasafiri kutoka hapa kwenda tutakapoelekea kama ni majimboni ama mahali kwingine niwaombe sana madereva wetu au kama tunaendesha wenyewe basi tuendeshe kwa umakini mkubwa bila kukimbia kimbia bila sababu na pia kila mmoja wetu awe na umakini wa ziada na kuzingatia sana ushauri ambao tunapoewa na Serikali na kipekee Wizara ya Afya kuhusiana na afya zetu kwa ujumla wake.

Basi ni matarajio yetu kwamba Mungu atakuwa upande wetu kwamba wakati huo tutaweza kukutana sote kwa pamoa. Mwezi huo tutakaporudi tutakuwa na chaguzi chaguzi nyingi. Natumaini tutakuwa tumeshafahamiana vyakutosha, kwa hiyo, chaguzi za wakati huo zitaendelea kama kawaida. Hatutazifanya mapema, tutasogeza mbele kidogo angalau watu wajiandae vizuri ili ziweze kupita.

Basi baada ya matangazo hayo kama mnavyoju baada ya shughuli hii tunatakiwa saa 7.30 mchana ambao sio muda mrefu kuanzia sasa tuwe hapo nje tuweze kukaa kwenye maeneo yetu tuliyopangiwa ili ile shughuli nyingine inayofuata ya kumuaga ndugu yetu Mhandisi Atashasta Nditiye iweze kufuata.

Kwa jinsi hiyo basi niwashukuru sana vijana wetu wa Kwaya ya Bunge kwa jinsi ambayo mmekuwa mkifanya kazi nzuri sana, muendelee kujino, naamini kabisa Katibu wa Bunge anawaangalia vizuri na ataendelea kuwaangalia vizuri, ipo siku katika Mashindano yetu ya Michezo ya Mabunge tutaweza kushindanisha kwaya zetu, Bunge la

Uganda na Bunge la Kenya katika upande huo pia ili tuweze kuona mabingwa ni wapi. (*Makofi*)

Lakini kama nilivyowaambia siku moja ile Kwaya ya Mahakama walionesha nia ya kuimba na Kwaya ya Bunge katika viwanja vya Bunge ili kuona kwaya ipi ni mahiri zaidi ya nyingine. Kwa hiyo, muendelee kujipanga vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, kw amaneno hayo naomba tusimame ili Kwaya yetu ya Bunge iweze kuimba Wimbo wa Taifa.

Wimbo wa Taifa.

(Hapa Kwaya ya Bunge iliimba Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukiwa tungali tumesimama niwakumbushe tu kwamba kwa ratiba ilivyo ili tuanze Bunge tarehe 30 Machi maana yake ni kwamba Kamati tutazianza katikati ya mwezi Machi. Kwa hiyo, kati ya sasa mpaka tutakapokutana wakati wa Kamati ni kama mwezi mmoja tu, kwa hiyo mnapotoka hapa basiratiba zenu mziweke katika utaratibu huo na tunapokutana kuanzia katikati ya mwezi Machi ndio tunakwenda moja kwa moja mpaka tarehe 30 Juni, 2021. Kwa hiyo, tujipange kihivyo.

Kwa jinsi hiyo na kwa hatua hii naahirisha shughuli za Bunge sasa hadi tarehe 30 Machi, 2021 siku ya Jumanne, saa tatu kamili asubuhi.

(Saa 7.04 Mchana Bunge lilahirishwa hadi siku ya Jumanne, Tarehe 30 Machi, 2021 Saa Tatu Asubuhi)